

Ina Somo Tatuz
za Zaidi

Kutembea Pamoja na Yesu

Mafundisho ya msingi
kwa ajili ya waaminio
Kristo

Kiswahili

Utangulizi

Kwa mchungaji ama kiongozi wa kundi:

Kutembea Pamoja na Yesu inaweka msingi katika maisha ya kikristo kwa wale wote waliochagua kumfuata Yesu. Kuna tofauti kubwa kati ya mtu aendaye kanisani siku ya Mungu na mwanafunzi mkamilifu aliye na kiu na njaa ya Neno la Mungu akiwa pia mtu anaye muheshimu Mungu.

Yesu alipokuwa akitembea katika miji na vijiji vya Israeli, aliwaita watu waje kwake ili wawe wanafunzi wake. Kwa mda wa miaka mitatu ya huduma yake hapa duniani, aliwafundisha kanuni za kuishi katika ufalme wa Mungu.

Kanisa la Kristo lilifanyika ili liwe lenye kutembea, liongezekalo mara kwa mara, likiwafikia watu katika jamii na kutambuka mipaka ya mahali ili lifikiye mataifa. Mikononi mwako unacho kifaa kizuri kwa kuwafanya watu wawe wanafunzi, kitabu hiki ni mwongozo mzuri kwako na kwa kanisa lako pia. Kitawasaidia watu wako kuwaleta wengine kwa Yesu na kuendelea kuwafundisha ili wawe wanafunzi.

Kutembea Pamoja na Yesu imeandikwa ili ifundishwe na mchungaji ama kiongozi wa kundi akomaaye kiroho, anaye elewaye mafundisho ya msingi ya Biblia, na zaidi ya yote awe mtu aliye na moyo wa kuwafanya wengine wawe wanafunzi wa kweli wa Kristo.

Kutembea Pamoja na Yesu ina jumla ya somo 19 tofauti. Kila somo lina maandiko yanayo hitajika kutazamiwa na kusomewa kwa sauti ili kundi lote lisikilize. Kuna pia maswali ya kuzungumzia, yakusudiayo kuwe mazungumzo kati ya kundi, na kufikiri pamoja. Mwisho wa kila somo kuna andiko ambalo kila mmoja katika kundi anahitaji kujua kwa ufahamu.

Maombi yetu ni kwamba Roho Mtakatifu wa Mungu azungumze ukweli wa Mungu nanyi kwa nguvu kupitia mafundisho haya. Mungu akunehemishe na kukuelewesha ujifunzapo Neno Lake.

Biblia iliyu tumiwa katika mafundisho haya ni **Biblia Maandiko Makatifu, Kiswahili 1952**.

Unaruhusiwa kufanya nakala ya mafundisho haya na kuyagawanya jinsi unataka, tunacho hitaji kwako ni kuweka pia utangulizi wa kitabu hiki.

Hauna ruhusa ya kubadilisha maandiko ama maneno yaliyomo.

Ukitaka kutafsiri kitabu hiki kwa luga ingine tafazali uwasiliane na Young Ministry Group ili upewe ruhusa na mwelekeo.

Tunakutakia furaha ya Yesu Kristo katika maisha yako...

Mana Shemahamba Rostand (**RDC**), Julie Young (**USA**)
& Martin Baskerville (**UK**)

Namna ya Kutumia Mafundisho Haya

1. Somo – Chaguwa somo ambayo utakayo fundisha kundi lako. Ni vizuri zaidi kuanza na somo la 1 baadaye uendelee na somo zifuatazo.

Soma somo kwa sauti. Soma jinsi maneno yameandikwa katika somo. **USIBADILISHE** maneno yaliyo ndani ya somo ama kuongeza mengine yasiyo kuwemo. Soma somo kwa sauti kwa ajili ya kundi lako, soma jinsi somo limeandikwa, ukitumia maneno yaliyomo.

2. Matayarisho – Ujitarishe vizuri kabla ya kufundisha somo lolote. Ikiwa hauzowi mafundisho haya, ujifunze mwenyewe kwanza somo lile ukiomba Roho Mtakatifu akufundishe na kukuelewesha yale ambayo utakayo yafundisha.

- a. Soma kwanza somo ukichunguza Maandiko yote ya Bibilia yaliyomo.
- b. Uelewe vizuri somo na mada utakayo ifundisha.
- c. Ikiwezekana, uwatayarishiye mapema wanafunzi wako karatasi na kalamu watakazo zitumia kwa kuandika vesi ya ufahamu ya somo lililo pita.

3. Uombe – Uombe Mungu akupe hekima na kuelewa, na kukuwezesha kufundisha somo kwa namna ifaayo kwa kundi lako.

4. Biblia – Biblia zikiwa chache ndani ya kundi zisiwe chini ya 4 ama 6 na zigawe kwa wanafunzi mbalimbali, ili kundi lako liweze kujitafutia lenyewe maandiko (labda unaweza kuazima Biblia chache). Uwape moyo kundi lako ili wazoweye kusoma Biblia, wakitafuta maandiko na kuyasoma kwa sauti kwa ajili ya wengine walio ndani ya kundi. Ikiwa wamoja ndani ya kundi hawajuwi kusoma, uwaombe wakae karibu ya mtu anaye juu kusoma na anaye kuwa na Biblia.

5. Eleza kichwa cha somo mwanzoni – Unapoanza kufundisha, hakikisha kwamba umejulisha vizuri kichwa cha somo kwa kundi. **Mfano:** “Ninawakaribisha kwa mafundisho siku ya leo. Leo tutajifunza somo linalo husu ‘**Zambi na Wokovu**,’ somo hili ni somo la kwanza katika mafundisho ya ‘**Kutembea Pamoja na Yesu**’”

6. “Soma kwa sauti:”--Mahali ambapo somo laomba andiko la Biblia lisomewe kwa sauti, umuombe mmoja kati ya wanamemba wa timu aliyе na Biblia atafute andiko na kulisoma kwa sauti kwa ajili ya kundi. (Hakikisha kwamba ni mwanamemba wa kundi asomaye andiko kwa sauti, si mwalimu wa kundi). Baada ya kusoma uwape moyo kwa kusema maneno kama haya, “*Asante kwa kusoma*,” ama “*umesoma vizuri*.”

Usiwafanye kujisikia kuwa hawajuwi kitu ama kuwazarau. Uwe mtu apatiaye wanafunzi wako moyo.

7. “Maswali:” -- Omba kundi lifikiri kuhusu majibu ya kila swali. Wewe si mtu wa kujibu maswali, uwaombe wanafunzi wako wajibu maswali. Hii itawasaidia kuanza kufikiria kuhusu yale uliyo kuwa ukiwafundisha.

8. “Vesi kwa ufahamu”—Mwisho wa kila somo kuna vesi kwa ufahamu. Kundi lako lipewe moyo kuandika andiko hilo (utahitaji kalamu na karatasi kwa ajili ya hiyo). Kundi leweke kwa ufahamu kila vesi. Mtihani uwe mwanzo wa kila somo: “jee, mnakumbuka vesi kwa ufahamu ya somo *lililo pita?*”

9. Watu tofauti— Hakikisha kwamba umempa moyo kila mwana memba wa kundi lako kushiriki somo kupitia kujibu maswali, ama kwa kusoma maandiko kwa sauti.

Usiruhusu mtu mmoja pekee kuchukua nafasi ya kundi lote.

10. Kuwe kufurahiyana! – Somo liwe la ufurahivu. Ni vizuri kuwe kicheko cha furaha ndani ya kundi. Ni vizuri kuwe kuchangamka. Somo msimo kuwa ndani furaha husahaulika haraka.....

Kutembea Pamoja na Yesu - Waandishi



Mana Shemahamba Rostand (RDC)



Julie Young (USA)

Namna ya kuwasiliana nasi:

Ikiwa umefurahia mafundisho haya, tafazali utujulishe:
Wasiliana nasi kupitia e-mail na tutafurahi kukusikiliza.

Young Ministry Group International

e-mail: ymgrdc@aol.com

(Andika jina lako, kijiji/mji, na jina la jimbo unamo ishi.
Weka pia e-mail na namba ya simu)

ama tupigie simu **Simu: +243 997796099**

© 2015, Young Ministry Group.

Mawazo ya viongozi wa makanisa kuhusu kitabu hiki:

Kitabu hiki kinafaa sana, kufuatana na umuhimu wake ni vizuri makanisa yaaminiyo Yesu Kristo Kama vile Bwana na Mwokozi kukitumia kwa ajili ya kupanua Ufalme wa Mungu.

Amos Kavuye Ndondwa

Mchungaji wa Kanisa la CEPAC Uvira Kasenga

Kutembea Pamoja na Yesu ni kitabu kizuri kwa ajili ya viongozi walio na moyo wa kuwafanya watu kuwa wanafunzi, mafunzo yaliyomo katika Kitabu hiki yatasaidia kanisa la mahali kukomaa kiroho na kutembea katika nyayo za Kristo.

Célestin Modeste Rukenura

Représentant Légal Adjoint de L'Eglise Charismatique Emmanueliste

Kutembea Pamoja na Yesu ni Chakula kilicho tayari kwa kula, mwalimu hahitaji tena mda mrefu kwa ajili ya maandalizi. Waandishi wamewarahisishiya walimu kazi ya kufundisha. Kitabu hiki ni moja wapo wa mafundisho ya msingi, ni msaada mkubwa kwa walimu wanaokuwa na lengo pia nia nzuri ya kufundisha wakiwavuta watu kwa Yesu. Kitabu hiki ni msaada na mafundisho ya kumuwezesha mfuasi mzuri kujua kuishi vizuri na kwa amani pamoja na wengine katika jamaa, kanisa, jamii hata katika inchi. Kitabu hiki kina saidia pia kuleta maendeleo ya kiroho na kimwili.

Jean Bugoye

Mwalimu kwenye chuo kikuu cha teologia cha Université Libre Baptiste du Congo/Uvira

Hiki kitabu ni mojawapo wa vitabu tunavyo vihitaji, tulikuwa tukisumbuka sana kwa kuijiliza ni mpangilio gani wa mafundisho tunaweza kuwafundisha waamini wapya; kwa kuona mpangilio ya masomo yaliyomo katika kitabu hiki nina hakikisha kwamba kitasaidia makanisa yote kwa kuwafundisha waamini wapya. Kupitia mafundisho haya naamini kwamba atakaye weka katika matendo mafundisho haya atakuwa na tabia zifananazo na zile za Kristo.

Claude Dinga

Mchungaji wa Church of the Holy Spirit/Kamanyola

Somo zote 19 za kitabu hiki zina ushirika, somo la mbele linasaidia kuelewa vizuri somo lijalo, somo zote za zazungumzia kuhusu jinsi ya **Kutembea Pamoja na Yesu**. Ufupi wa kila somo na utajiri wake kimawazo na kimafundisho vime nivutia saana na kuzaa ndani yangu moyo wa kuwa mfupi na hakika katika maandalizi ya somo zangu na semina mbalimbali kanisani, kati ya ukarasa 4 ama 7. Kitabu hiki kimetufunza mtindo mpya wa kufundisha kanisani kwa kuwashirikisha wanafunzi kwa mafundisho ili watowe pia maoni yao, waulizwe maswali, wajibu na kwa maulizo,...

Jambo nzuri tena zaidi ni kuona mwisho wa kila somo kuna vesi ya kuweka kwa uframbo. Kitabu hiki kinajibu kwa mahitaji ya kiroho ya waamini wapya na wale wa zamani, mfano wale wanao endelea kuabudu sanamu wakijidai kuwa wao wameokoka. Kitabu hiki kitapatia makanisa mwelekeo na kuwasukuma wakristo kuchukua uamzi wa

Kutembea Pamoja na Yesu sawasawa na maandiko Matakatifu.

Simbi Saleh Emmanuel

Mchungaji wa 8^{ème} Sange Rutanga na Mwalimu kwenye chuo Kikuu cha teologia/UEA Bukavu

Mafundisho haya yametusaidia sana kwa kuwafundisha waamini wapya, yamesaidia katika matayarisho ya waamini wapya kwa ajili ya ubatizo, yamewasaidia sana waamini wapya kuchukua uamzi wa kumfuata Yesu kikamilifu, hata na sisi pia tunao husika kufundisha waamini wapya Kitabu hiki kimetujenga sana.

Amisi Numbi Aron Muinjilisti wa Patmos Temple/Mulongwe, Communauté Chrétienne pour la Réconciliation

Makanisa yetu yanakuwa na ukosefu kwa ngazi ya juu ya vitabu vya mafundisho, hii ina sababisha kuwa na wakristo wasio elewa maana ya ukristo, kitabu hiki kitasaidia makanisa yetu kujenga kwenye msingi ulio imara. Ninawapa moyo viongozi wenzangu kutumia kitabu hiki kwa kuwa ni mojawapo wa majibu ya Mungu kwa ajili ya mahitaji ya makanisa ambayo Mungu ametufanya sisi tuwe waangalizi.

Askofu Ilondelo Roger

Président des Eglises Indépendantes Uvira, Fizi, Walungu

Kutembea Pamoja na Yesu ni kifaa cha kimishonari ambacho nina linganisha na fimbo ya msafiri. Siku moja nikiwa nafundisha wanafunzi wa ubatizo kwa kutumia kitabu hiki, niliona machozi yakidondoka machoni mwa wanafunzi, wakati huo tulikuwa tukisoma kuhusu kazi ya Yesu aliyofanya kwa ajili yetu msalabani.

Muisilamu mmoja aliyefundishwa kuititia kitabu hiki na baadaye akabatizwa, anatowa mara kwa mara ushuhuda kanisani kuhusu mabadiliko ambayo mafundisho hayo yameleta maishani mwake.

Mimi mwenyewe kuititia kufundisha kwa kutumia kitabu hiki, nimetambua kwamba somo mbalimbali zime chaguliwa vizuri, na mafundisho ni mazuri kwa watu wote na yanaweza kusaidia pia hata waamini wapya na wale wa zamani.

Dr Kundo Peniel

wa Aumonerie Universitaire Protestante ya Uvira na Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Afya ISTM/Uvira

Hiki kitabu ni hazina, ni chakula kwa afya ya kiroho ya kuotesha imani, ni kitabu cha maisha yenye uzima tele kwa mkristo anayependelea daima **Kutembea Pamoja na Yesu** katika ulmwengu unao haribika na uovu na dhambi mbalimbali. Kitabu hiki kinajibu maswali ya mwanadamu aliye kata tamaa ya kuona kama hakusamehewa, ni kitabu ambacho kinajibu na kinahimiza walimu kwa kuimarisha wafuasi wa Bwana Yesu Kristo, ni chombo cha mafundisho ya ubatizo kwa waamini wapya, ni msaada na mwalimu kwa viongozi wa makundi mbalimbali, ni lulu katika lulu za Biblia. Kitabu hiki ni mana ya Mungu kwetu, ni msingi imara wa imani katika neno la Mungu.

Byochinda Luenga Victor

Mzee wa Kanisa la 8^{ème} CEPAC Mulongwe/Uvira

Kitabu hiki ni msaada sana kwa ajili ya kukuza waamini kimafundisho na kuwafanya wakomae katika imani, kanisa letu linawashukuru waandishi wa kitabu hiki kwa kazi kubwa na uvumilivu wao ili kitabu tuwe nacho mikononi mwetu.

Mulangi Mukiekie Keke

Mchungaji wa International Church of the Foursquare Gospel/Uvira DR Congo.

Vitabu vya kuwafundisha waamini wapya havipatikani tena, hapo zamani vilikuweko bali kwa sasa vimepotea kabisa. Sisi tunao ishi sehemu za vijijini tunakuwa na shida kubwa sana kupata vitabu ambayo tunaweza kutumia kwa kuwafundisha waamini wapya.

Kutembea Pamoja na Yesu itatusaidia sana katika makanisa zetu kuwafundisha waamini wapya na wale wale ambao wamekaa makanisani siku nyingi pasipo kuelewa maana ya ukristo. Hata na sisi pia viongozi wa makanisa kitabu hiki kitatusaidia kuelewa umuhimu wa kazi ambayo Mungu ametuuta kufanya, kita tusaidia pia kuelewa mahitaji ya wale ambao Mungu ametufanya tuwe wachungaji wao.

Balolage Muganda

Mchungaji wa 5^{ème} CELPA Mishamba Luhwinja

Kutembea Pamoja na Yesu

Yaliyomo

| | Somo | Ukurasa |
|-----|---|----------------|
| 1. | Zambi na Wokovu | 8 |
| 2. | Mambo Mapya Katika Kristo | 13 |
| 3. | Yesu Ndiye Njia Pekee | 17 |
| 4. | Ubatizo kwa Maji | 22 |
| 5. | Kuzungumza na Mungu-Maombi, Sifa & Kuabudu | 26 |
| 6. | Kusikia Sauti ya Mungu | 32 |
| 7. | Neno la Mungu | 38 |
| 8. | Mungu yuko Namna Gani? | 43 |
| 9. | Mungu Mmoja wa Kweli | 50 |
| 10. | Waelezee Wengine Kuhusu Yesu | 55 |
| 11. | Ubatizo wa Roho Mtakatifu | 60 |
| 12. | Kanisa ni Nini? | 65 |
| 13. | Mbele ya Uso wa Mungu | 71 |
| 14. | Msamaha | 75 |
| 15. | Ushindi na Uhakika Katika Kristo | 81 |
| 16. | Karama za Roho Mtakatifu | 88 |
| 17. | Uwakili, Chakumi & Sadaka | 96 |
| 18. | Umoja wa Kikristo | 106 |
| 19. | Garama ya Kumfuata Yesu. | 111 |
| | Maneno unahitaji kuelewa: Kamusi | 117 |

Somo la 1

Zambi na Wokovu

Karibu kwa mafundisho ya **Kutembea Pamoja na Yesu!** Jinsi utakavyo shiriki kila somo katika jumla ya masomo 19, utaelewa vizuri maana ya kuwa mkristo. Utakomaa pia kiroho kama vile mwanafunzi wa Yesu Kristo.

Katika somo hili la kwanza tutachunguza mambo muhimu kuhusu habari zifuatazo:

1. Zambi ni nini?
2. Namna gani zambi imeingia ulimwenguni?
3. Matokeo ya zambi katika maisha yetu leo.
4. Suluhisho la Mungu kwa kumaliza matatizo ya zambi.

Katika kitabu cha Mwanzo, kitabu cha kwanza cha Biblia, tunasoma hadisi ya jinsi Mungu alivyoumba ulimwengu na vyote vilivyomo. Humo tunasoma jinsi Mungu alivyo waumba mwanamume na mwanamuke wa kwanza, Adamu na Eva. Wote waliumbwa kwa mfano na sura Yake, na Mungu akawaweka katika bustani nzuri, iitwayo Edeni.

Mungu aliwapenda sana Adamu na Eva, akawapa kila aina ya chakula walicho kihitaji na akawapa pia uhuru kamili wa kuishi bila woga. Mwanamume na mwanamuke walioumbwa na Mungu waliishi katika amani kamili, furaha na maelewano, wakiwa na uhusiano pamoja na Mungu mwenyewe.

Mungu aliwakataza kitu kimoja kidogo pekee, wasile tunda la aina moja ya mti uliokuwa katika bustani; mti huo ujulikanao kama “mti wa ujuzi wa mema na mabaya.” Mungu akasema mkila tunda la mti huo mtakufa.

Soma kwa sauti: Mwanzo 1:26-31, Mwanzo 2:8-9 na Mwanzo 2:15-17

Kupitia maandiko hayo tunaelewa yafuatayo:

1. Watu (wanaume na wanawake) waliumbwa kwa mfano wa Mungu.
2. Adamu na Eva waliishi nafasi nzuri katika maisha makamilifu. Hapakuwepo hatari yoyote, wala jeuri, magonjwa, ama woga. Walikuwa na uhuru kamili, wakikatazwa kitu kidogo pekee, na hicho ni kutokula tunda la aina moja ya mti.
3. Mungu anataka watu waishi maisha yaliyo mazuri, pia waishi katika uhusiano uliyo mzuri pamoja na Yeye.

Zambi ya Kwanza

Soma kwa sauti: Mwanzo 3:1-6

Katika maandiko haya tunasoma kwamba Shetani (malaika mbaya) alifika katika bustani ya Edeni akijigeuza kama vile nyoka. Shetani akawadanganya Adamu na Eva ili waasi amri waliyo pewa na Mungu. Shetani akawaelezea kwamba, ikiwa mtakula tunda la mti alilo wakataza Mungu msile, hamtakufa, lakini mtakuwa kama vile Yeye.

Adamu na Eva walifanya kosa kubwa kwa kuamini maneno ya Shetani na kumuasi Mungu. Hawakujizuwia na kitu kimoja kidogo walicho katazwa na Mungu. Lakini, wakamtii Shetani na wakatenda mambo katika ubinafsii.

Adamu na Eva ndio walileta zambi ya kwanza ulimwenguni walipo amuwa kumuasi Mungu. Zambi zao zikawatenganisha, Adamu na Eva, na Mungu. Mungu ni mtakatifu, mkamilifu katika njia zake zote, na hana zambi yoyote. Mungu hataki kuwa nafasi ambapo panapokuwa zambi na Yeye havumiliyi kamwe chochote kinacho kuwa na ushirika na zambi. Mungu akawaazibu Adamu na Eva kwa sababu ya zambi zao na kuwafukuza katika bustani hiyo nzuri. Tangu hapo wakaanza kugonjwa, kifo kikaingia, woga, na mabaya yakaingizwa nao ulimwenguni.

Namna Gani Zambi Zatusumbua Maishani Leo

Zambi za mwanzo za Adamu na Eva zimeenea pote na kuambukizwa, zazidishwa kizazi hadi kizazi tangu wakati ule wa Adamu na Eva. Watu wanaendelea hadi leo kuishi maisha ya ubinafsi wakimkosea Mungu, wala hawatii amri zake. Inaleta uchungu kuona, ulimwengu leo ni tofauti sana na nafasi nzuri ambayo Mungu aliyo iumba hapo mwanzo. Zambi yaweza kuelezwa kama vile aina yoyote ile ya kutokumtii Mungu.

Hizi zifuatazo ni aina mbalimbali za zambi na matokeo yayo mabaya tuyaponayo mara kwa mara katika jamii tunamo ishi. Haya yanaendelea kuonekana kwa sababu wanadamu wanaendelea kumuasi Mungu, na kuishi maisha ya ubinafsi, na kutenda yote kwa njia ya zambi:

**Kusema uongo, ujanja, kuiba, uwasherati, ujeuri, uasi,
Kuvunja ndoa, kubomoa mimba, ubinafisi, ubakaji, ulawiki,
Ujeuri kwa watoto, uuwaji, kuabudu sanamu, uchawi, kutumia
madawa ya kulevya, ulevi, ukahaba, ulafi, rushwa na vita....**

Mambo haya mabaya yote yatajwayo hapo juu (na mengine mengi) yanafanya ulimwengu iwe nafasi ya hatari pia nafasi isiyo kuwa nzuri kuishi.

Sherti Zambi Zihukumiwe

Biblia inatueleza kwamba kila mtu aliye ishi ataazibiwa na Mungu kwa sababu ya zambi alizo zitenda.

Matendo 17:31 inasema “*kwa maana ameweeka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchaguwa; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumufufua katika wafu.*”

Soma kwa sauti: Warumi 3:23

Kila mtu atakayeonekana kuwa mwenye hatia atahukumiwa na kupewa azabu ya milele katika moto, nafasi iitwayo Jehenamu, mbali na upendo wa Mungu na uwepo wake. Jehenamu ni nafasi inayo jaa mateso na maumivu. Azabu hii inatungojea sisi sote, kwa sababu Biblia inasema kwamba kila mtu ni mwenye hatia.

Sasa tunaweza kufanya nini?

Yesu Kristo –Ndiye Suluhisho ya Mungu kwa ajili ya Zambi

Soma kwa sauti: Mwanzo 3:14-15

Kwa sababu Mungu anawapenda watu ambaa aliwaumba, Mungu akaahidi kwamba atamtuma Mkombozi ili awaokowe watu wa ulimwengu. Akaahidi kwamba mkombozi atatoka katika kizazi cha Adamu na Eva. Mkombozi huyu atasaga mjaribu mbaya, Shetani, chini ya kisingino chake. Aliye ahidiwa atawaokowa watu kutoka zambini na kuwaepusha na

mabaya. Ahadi hii imetimilika wakati Yesu, Mwana wa Mungu, alipokuja duniani, kama vile ilivyo andikwa katika Agano Jipyä iliyo ndani ya Biblia.

Mpango wa Mungu wa Wokovu

Mungu anampango mzuri wa kutuokowa. Aliona kwamba ulimwengu wote umo katika hali ya kukosa tumaini, umefungwa na zambi, na kutengwa naye ukingoja moto wa Jehenamu.

Soma kwa sauti: Yohana 3:16

Mungu anakupenda sana hata akamtuma Yesu aje afe kwa ajili yako ili usipate kuhukumiwa kwa ajili ya zambi zako. Mungu aliweka njia ili zambi zetu zipate kusamehewa na kuvutwa kabisa – Yesu alipokufa msalabani alikufa kama zabihu kamili kwa ajili ya zambi zetu. Yesu alikufa kwa ajili ya zambi za kila mtu ambaye aliyewai kuishi na aishiye sasa, na atakaye ishi baadaye.

Yesu, Mwana wa Mungu, aliishi maisha makamilifu, maisha bila zambi kwa hiyo zabihu yake ilikubaliwa mbele za Mungu, damu yake ilimwangika msalabani ili alipe garama ya zambi zetu, na kutuondoleya azabu ambayo ilikuwa ikitustahili. Zabihu ya damu ya Yesu ni njia ambayo Mungu alitumiya ili aturejeshe kwake; ili tuwe na uhusiano mzuri pamoja naye.

Mchungaji/Kiongozi: unaweza kusoma andiko hili ndefu kwa ajili ya kundi:

Soma kwa sauti: Matayo 27:31-54

Andiko hili linatuelezea jinsi Yesu alivyoteswa na kufa kwa ajili ya zambi zetu.

Soma kwa sauti: Warumi 6:23

Zambi zetu zatushitaki mbele ya Mungu; bali Mungu yuko tayari kutusamehe na kutupatia zawadi ya uzima wake.

Soma kwa sauti: 1 Petro 2:24

Yesu ametwikwa zambi zote tulizo zitenda, akateswa nafasi yetu. Yesu alikufa kwa ajili yetu, na akazikwa. Baada ya siku tatu, Mungu alimfufua kutoka kati ya wafu! Sasa yuko hai wala hatakufa tena! Ujumbe huu unaitwa injili, ama habari njema.

Kwa nini hii ni Habari Njema?

Hii ni habari njema kwa sababu, kwa sasa Yesu ameweke njia ili zambi zetu zipate kusamehewa! Kwa sasa tunaweza pokea maisha mapya mazuri, tukiishi maisha ya ushirika mzuri pamoja na Mungu!

Ikiwa tunajuta kwa ajili ya zambi zetu na kuziacha (kutubu), tunaweza kuomba Yesu atusamehe. Hiyo yatendeka kwa kuwa Yesu aliteswa nafasi yetu msalabani, amelipa tayari garama yote ya zambi zetu zote. Tuachapo zambi na kumupokeya Kristo, hatupashwi tena kuishi katika woga wa hasira ya Mungu ama hukumu yake.

Sasa kuna mambo mawili unapashwa kufanya ili upate kuokolewa na Yesu Kristo:

1. Unapashwa kutubu. Kutubu maana yake ni kugeuka na kuacha njia ya zambi. Maana ya hiyo ni kukubali mbele za Mungu kwamba umefanya zambi.

2. Unapashwa kuweka imani yako ndani ya Yesu. Ukitukwamba kwamba Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya zambi zako. Hii inaitwa imani. Ufanyapo mambo hayo unapokeya msamaha wa Mungu. Unapokea pia maisha mapya kutoka kwa Mungu, maisha ya milele.

Soma kwa sauti : 1 Yohana 5:11-12

Umuombapo Yesu akusamehe na kumualika aingie moyoni mwako, unapokea msamaha wake, na kupokea uzima wa Mungu maishani mwako.

Soma kwa sauti: Yohana 10:10

Yesu alikuja ili tupate uzima tele pia ujaao! Hatuhitaji kulipa chochote ili tupokeye huo uzima mpya. Ni zawadi kutoka kwa Mungu tupokeyayo kuitia imani katika Yesu Kristo. Hatuwezi kununua uzima huo mpya ambao atupatiyayao. Kwa sababu uzima huo ni zawadi tunayo peva kwa njia ya imani katika Yesu Kristo. Hatuwezi kujitowa sadaka ya kuteketeza ili tupokeye uzima huo. Tunacho hitaji kufanya ni kukubali mbele ya Mungu kwamba sisi ni wenge zambi na kumuomba Yesu Kristo atusamehe na kutuokowa.

Soma kwa sauti: Yohana 1:12

Tumupokeyapo Yesu katika mioyo yetu na maishani mwetu tunageuka kuwa sehemu ya jamaa la Mungu- tunageuka wana wake wa kiume na wa kike!

Soma kwa sauti: Wakolosai 1:13-15

Tumeondolewa gizani na kuleta chini ya ulinzi wa Yesu. Tunapoanza kuishi mambo kama haya, Biblia inayaita wokovu, ama kuokoka.

Jee, umeokolewa na Yesu?

Wokovu Unatendeka Namna Gani?

Ikiwa tayari umemualika Yesu kuingia katika maisha yako, hapo ndipo utakapo elewa uhuru tofauti na hatiya na matokeo mabaya yaletwayo na zambi. Tayari sasa Yesu anaishi ndani mwako akikuongoza, anakupenda, na kukusaidia, akiishi pamoja nawe kila siku.

Mchungaji/Kiongozi: jee, kuna mtu katika kundi lenu ambaye haja mpokea Yesu?

Hii ndiyo wakati sasa wa kuwauliza ikiwa tayari wamempokea Yesu. Unaweza kusema: “*Ikiwa hauja mwalika Yesu asamehe zambi zako na kuupokea uzima wa milele, unaweza kufanya hiyo sasa hivi. Inua mkono wako ikiwa unataka zambi zako zisamehewe na kumpokea Yesu kama vile Bwana na Mwokozi wako.*”

Baada ya hiyo, omba maombi haya pamoja nao, uwaalike kuyarudiliya maneno haya baada yako: “***Bwana Yesu, Naamini kwamba wewe ni Mwana wa Mungu. Naamini kwamba ulikufa msalabani kwa ajili yangu, na kwamba ulifufuka kutoka wafu. Nakuomba unisamehe zambi zangu zote. Nitakase, Niweke huru. Nafungua mlango wa moyo wangu na kukualika uingie ndani. Nisaidie kuishi kwa ajili yako siku zote. Asante, Yesu, kwa kuniokoa. Amen.***

Somo kwa ufupi:

Tumejifunza kwamba:

1. Tumuombapo Yesu asamehe zambi zetu, yeye anatusamehe, kwa sababu Yesu alilipa garama yote ili aondowe zambi zetu alipokufa msalabani.
2. Tunapokubali Yesu kama vile mwokozi wetu tunapokea uzima tele, pamoja na maisha mapya, yanayo jaa. Yesu mwenyewe anakuja kuishi ndani yetu.
3. Tuliondolewa gizani na kuishi sasa katika ufalme wa Yesu.
4. Kwa sasa sisi ni wana wa kiume na wa kike wa Mungu aliyeumba ulimwengu na vyote vilivyomo.

Maswali:

Mchungaji/Kiongozi: uliza maswali haya na kuacha kundi wayazungumuzie:

1. Ulijifunza nini kuhusu zambi leo?
2. Maana ya kutubu ni nini?
3. Umejifunza nini kuhusu wokovu?
4. Ni nani unawenza kuzungumzia kuhusu habari njema hii?



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi lijifunze na kuweka kwa ufahamu andiko hili (uwakumbushe kuweka kwa ufahamu sura na vesi):

Yohana 3:16

“Kwa maana jinsi hii Mungu alivyoupenda ulimwengu hata akamtoa Mwana wake wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa miliele.”

Somo la 2

Mambo Mapya Katika Kristo

Tunapo muomba Yesu aingie katika maisha yetu, zambi za kale za maisha yetu anazisamehe kabisa. Ndipo tunapo geuka kile ambacho Biblia inaita “*kuzaliwa mara ya pili*” na tunaanza kuishi maisha mapya, Kristo akiishi ndani yetu kupitia Roho Mtakatifu wake. Hapo ndipo tuaanzapo kuishi kama vile wakristo, ama wafuasi wa Yesu.

Soma kwa sauti: 2 Wakorinto 5:17

Maisha mapya yanaanza kwetu tujitoapo kwa Mungu kupitia njia ya imani ndani ya Yesu Kristo. Ndipo Mungu asemapo kuwa tumekuwa safi na tunaanza upya maisha yetu. Maisha yetu yanageuka tofauti sasa. Jinsi tulivyo kuwa, yale tulivo yatenda, yote yafanyika mapya katika Kristo. Tunaweza kuendelea mbele na kuishi katika mibaraka ya Mungu.

Haya maisha mapya yanatupatia nini?

Kwa Sasa Sisi ni Sehemu ya Jamaa la Mungu

Soma kwa sauti: Warumi 8:15

Tumekubaliwa katika jamaa la Mungu. Yeye ni Baba yetu wa mbinguni. Kama vile waamini wapya, tumechagua kumfuata Yesu. Tumegeuka sehemu ya jamaa la Mungu, na anatuahidia kutushugulikia. Atatutunza. Atatuongoza kwa hekima. Watu kanisani wanageuka kuwa ndugu na dada zetu, baba na mama zetu.

Soma kwa sauti Yohana 13:34-35.

Yesu alituomba tupendana sisi kwa sisi. Tunapashwa sasa kusaidiana na kushugulikiana kwa sababu sisi ni sehemu ya jamaa ya Mungu hapa ulimwenguni leo.

Tumepewa Amani na Mungu

Kama vile wamuaminio Yesu tunapokea amani moyoni mwetu. Mungu hana hasira mara tena kwa ajili ya zambi tulizozitenda, kwa sababu zimesamehewa, Yesu alilipa garama yote.

Soma kwa sauti: Warumi 5:1

Biblia inasema kwamba tumehesabiwa haki. Maana ya neno hilo ni kusema kwamba tumetangaziwa kuto kuwa tena na hatia ya zambi, kwa sasa tunao uhusiano mzuri pamoja na Mungu—hiyo yote ni kwa sababu ya yale ambayo Yesu ametenda msalabani. Kujua ukweli huu kuna tuletea amani.

Soma kwa sauti: 2 Watesalonike 3:16

Amani inatoka kwa Mungu pekee yake. Kwa sababu sasa tume mushirikisha Mungu katika maisha yetu, Mungu anaweza kutupatia amani moyoni wakati tunapokuwa na matatizo ama maumivu.

Tunaweza Kuzungumuza na Mungu

Soma kwa sauti: Yeremia 29:12

Mungu anataka tumuombe. Maombi ni mazungumuzo pamoja na Mungu. Tunaweza kuomba kimoyo moyo ama kwa ukimya, ama kuomba kwa sauti. Unaweza kuzungumza na Mungu ukiwa pekee yako, ama

ukijiunga pamoja na wengine, ama ukiwa katika kundi kubwa. Mungu anapenda kutusikiliza tukiongea pamoja Naye.

Soma kwa sauti: Matayo 7:7

Mungu anatualika kumuomba kile tunacho kihitaji maishani mwetu. Kwa sasa sisi ni wake, Yeye ni Baba yetu mzuri. Tunaweza kumuomba chochote kile tunacho kihitaji. Tunaweza kuzungumza naye kuhusu chochote kile tunacho kifikiriya. Tunaweza kumueleza jinsi tunavyo jisikiya. Ni kitu cha kufurahisha: tukiwa kimya na kusikiliza, tunaweza kusikia Mungu akizungumuza nasi! Anazungumza zaidi ndani ya miyo yetu, mahali alipomuweka Roho Mtakatifu wake.

Soma kwa sauti: Matayo 11:28-30

Yesu anatuita twende kwake na shida zetu zote. Atatupumzisha moyoni mwetu. Tunapokuwa na shida, mda huo tunaweza kuomba Mungu tukimusikiliza Roho Mtakatifu wake aliye ndani yetu na atatupatia hekima na shauri. Neno la Mungu, Biblia, inamajibu mengi kwa shida na maswali yetu.

Tunapotenda Zambi

Soma kwa sauti: 1 Yohana 1:9

Tunapashwa kutubu kila jambo mbaya tulilolitenda haraka iwezekanavyo, tukimuomba Mungu atusamehe. Ndipo Yesu atakapo weza kutuosha zambi hizo. Katika maisha hayo mapya, mara tunatereza na kuanguka zambini. Yawezekana tufanye kitu ambacho tunajua kuwa ni kibaya. Tunaanza haya maisha mapya katika Kristo na Mungu anatupatia moyo tuje mbele yake na kumuomba msamaha.

Anatusafisha mara tena, ni kama vile tuna safishwa kwa ndani. Jee, hicho si kitu kizuri ambacho Mungu ametutayarishiya?

Jamaa Zetu Zinaweza Kuokoka

Sisi tumempokea Yesu lakini bado tunaendelea pia kufikiri kuhusu jamaa zetu, marafiki na jirani ambao bado hawaja mpokea Yesu. Tunataka wao pia, wamkulali Bwana Yesu maishani mwao.

Soma kwa sauti: Matayo 7: 7-8 na Matendo 16:31

Mungu anatupatia ahadi hii: tuki mheshimu na kumuamini, jamaa zetu na wengine pia wanaweza kumuamini Yesu. Hii ni habari nzuri!

Hii inatendeka namna gani? Tunaweza kuwaombea wale tuwapendao. Mungu anasikia maombi yetu na ataanza kufanya kazi ndani ya maisha ya watu wale. Mungu anafanya kazi ili waokoke, kwa kumpokea Yesu. Ni vizuri kuelezea jamaa zetu jinsi tulivyo mpokea Yesu, na yale aliyo yatenda katika maishani yetu. Usivunjike moyo ikiwa hawakujali ama wana hasira kwa ajili yako. Nguvu za Yesu za kuokowa jamaa lako zinafanya kazi sababu kwa sasa wewe ni wa Yesu Kristo. Mungu anakupenda sana na anapenda jamaa lako, pia. Unapo omba Yesu atakuwa akifanya kazi katika jamaa lako ili liupokee wokovu.

Kufunguliwa na Pepo Wachafu

Watu wengi wanashambuliwa na pepo wachafu. Biblia inatufundisha kuhusu hawa pepo wachafu, waitwao mapepo. Tunapokuwa wa Yesu maishani, hatupashwi kuogopa mara tena mapepo ama watu ambao wanafanya kazi na nguvu za giza.

Soma kwa sauti: 1 Yohana 4:4

Mungu ni mkubwa zaidi kuliko nguvu za pepo wachafu.

Soma kwa sauti: Matayo 8:16

Yesu aliamuru pepo wachafu kuwatoka watu waliyo sumbuliwa nazo. Yesu aliponya pia aina zote za magonjwa. Injili inne katika Agano Jipyaa zaeleza jinsi Yesu alivyo fukuza pepo wachafu mara nyingi. Yesu ana mamlaka yote zidi ya pepo wachafu, na alioneshaa hiyo mara nyingi.

Soma kwa sauti : Luka 10:1-9 na 16-19

Yesu aliwapa wamuaminio (na wewe pia) mamlaka zidi ya pepo wachafu. Unaweza kuamuru pepo wachafu waondoke, katika jina la Yesu. Yesu anataka uwe na ushindi katika nyumba yako, katika jamaa yako na maishani mwako pia.

Yeye ni Mungu aliye na mamlaka zidi ya miungu, watu wanao tumia mambo ya giza, wachawi, wafumu, na pepo wachafu. Haupashwi kuishi katika woga wa mambo hayo tena.

Ana Mpango Mzuri

Jee, unajuwa kwamba Mungu ana mpango mzuri kwa ajili ya maisha yako? Ugeukapo mkristo, utaanza kuelewa mpango mzuri ambao Mungu anao kwa ajili yako.

Mpango wako ni gani? Jinsi unavyo endelea kukomaa katika kumjua Yesu, jinsi utakavyo endelea kuelewa Biblia zaidi, Neno la Mungu, utaanza kutambua shabaa ambayo Mungu aliyo nayo kwa ajili ya maisha yako. Unapo omba, utasikia Mungu akikujulisha ni nini anayo taka kwa ajili ya maisha yako. Mpango wa Mungu kwa ajili yako ni mzuri zaidi na wa kipekee katika maisha yako.

Usiogope kuanzisha kile ambacho Mungu anataka ufanye. Jinsi unavyo mheshimu Yesu zaidi, itafanya uelewe kwa uwazi shabaa aliyo nayo kwa ajili yako.

Somo kwa ufupi:

Tumejifunza kwamba:

1. Tumekubaliwa katika jamaa la Mungu kama vile watoto wa kiume na wa kike. Kwa sasa kuna amani kati yetu pamoja na Mungu. Maisha yetu ya kale, na zambi zetu za maisha ya baadaye zimesamehewa kabisa.
2. Tunaweza kuzungumza na Mungu, na kumjulisha shida tulizo nazo na kumuomba atupatiye ama atuleteye suluhisho.
3. Tunaweza kuomba Mungu aokowe jamaa zetu, marafiki hata majarani.
4. Hatupashwi tena kuishi katika woga wa pepo wachafu ama wale wanaotumia uchawi.
5. Mungu ana mpango mzuri kwa ajili ya kila mmoja wetu.

Maswali:

1. Yesu alifanya nini msalabani kwa ajili yetu?
2. Taja faida moja uliyo ipokea kupitia Yesu Kristo.
3. Uliombea hitaji gani leo?
4. Jee, kuna hitaji ulilo liombea ambalo tayari Mungu amejibu?
5. Eleza kuhusu wakati ambao Yesu alikupatia amani katika maisha.



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi wajifunze na kuweka kwa ufahamu andiko hili :

2 Wakorinto 5:17-18

"Mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipyta; ya kale yamepita; Tazama! Yote yanakuwa mapya. Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho."

Somo la 3

Yesu Ndiye Njia Pekee

Kuna madini mengi ulimwenguni na imani za aina nyingi. Zimoja kati ya dini hizi ni: Uisilamu, Dini za Kihindi, Kibuda, asili za mababu, ibada ya mizimu, na zingine nyingi tofauti. Dini hizi zote zinatuomba tufuate namna yazo ya kuabudu tukifuata imani zao wakituahidia pia kuhusu maisha yetu ya milele yajayo.

Dini hizi zina shabaa ya kutimiza malengo fulani ama kutii sheria za aina fulani. Huamini kwamba hali ya kiroho ya mtu na wokovu kamili ama zawadi hufuatana na shurti kwa utiifu kwa sheria za dini ama bidii mtu aliyo nayo kwa kuwafurahisha miungu.

Katika somo hili tutajifunza kwamba hakuna chochote tunaweza kufanya ili tustahili kupokea wokovu na baadaye tuingie mbinguni. Wokovu huja tuu kupitia imani katika Yesu Kristo, kwa neema ya Mungu. Neema ya Mungu ni msaada tusio ustahili tulio upewa na Mungu kwa njia ya Yesu. Yesu mwenyewe ndiye aliye na uwezo wa kuokowa kwa ukweli, ndiye asameheaye, na atuwekaye huru.

Kwa nini hiyo? Sisi si bora zaidi hata tuwe na uwezo wa kuondowa zambi zetu sisi wenyewe. Hatuwezi kupokea uzima wa Mungu kwa kufuaata kanuni za dini ama mila zetu. Hatuwezi kupokea uzima wa Mungu kupitia nguvu za watu ama mambo ambayo watu wanayo yafanya.

Kazi pekee aliyo ifanya Yesu msalabani yatosha ili tupate kuokolewa. Hapo msalabani Yesu alikuwa zabihu kamilifu, isiyo na zambi istahiliyo kwa ondoleo la zambi zetu. Zabihu kamili ya Yesu ilikubaliwa kwa jumla na Mungu.

Yesu Ndiye Njia Pekee Itupelekayo kwa Mungu

Soma kwa sauti: Yohana 14:6-7

Yesu anatuelezea kwamba ni yeye mwenyewe ndiye anayeweza kumjulisha Mungu kwa ukweli kwa watu. Hakuna dini yoyote ile ama imani yoyote inayoweza kutuongoza kwa Mungu. Kumuamini Yesu ndio njia pekee ya kuupata uzima utokao kwa Mungu mwenyewe.

Yesu, Mwana pekee wa Mungu, alikuwa msalabani ili aliye garama ya zambi. Yesu alichukuwa azabu yote ya zambi zangu na zako; aina yote ya zambi; zambi zote. Hatuwezi kupokeya msamaha kwa matendo mema ama kwa kutii kikamilifu sheria ama matendo ya dini. Tunacho hitaji kufanya pekee, ni kutubu zambi zetu na kukubali zawadi ya msamaha kupitia imani katika Yesu.

Yesu ni Mungu

Tunahitaji kuelewa kwamba:

1. Hakuna kiongozi yeyote wa dini aliyewai kujitaja kuwa yeye ni Mungu wa mbinguni.
2. Hakuna kiongozi yeyote wa dini aliyewai kufa na kufufuka, na kushuhudiwa na watu wengi sana ulimwenguni.
3. Hakuna mkuu yeyote wa dini ambaye amewai kuonesha nguvu zake zidi ya pepo wachafu na mashetani.

Yesu alifanya haya mambo yote. Yesu akawaomba watu wamfuate kwa kuwa yeye ni Mungu.

Soma kwa sauti: Yohana 10:7-11

Yesu ni Mchungaji Mwema. Sisi ni kondoo wake. Anatuongoza, anatalisha, na kutulinda. Yesu anasema kwamba yeye ndiye mlango pekee wa kondoo ili kondoo wapate uzima. Kondoo hawamfuati yeyote yule, hata akijidai kuwa yeye ni nani. Umupokeapo Yesu, unageuka mmoja kati ya kondoo zake. Hiyo inatufurahisha!

Soma kwa sauti: Warumi 1:1- 4

Kwa kumufufua Yesu kutoka wafu, Mungu alionesha kwamba Yesu ni Mwanawe. Yesu si dini. Kumupokea Yesu kama vile Bwana na Mwokozi hiyo ni ushirika.

Watu wengine wanaweza kuwa na imani ya nguvu katika madini ama maabudu yao. Inawezekana wawe watu wazuri, walio na mawazo mazuri, ama wazuri kwa watu na majirani zao. Lakini Yesu anatuelezea kwamba yeye ni njia **pekee** ituongozayo kwa Mungu. Pasipo Yesu hakuna mtu anaweza kumjua Mungu kwa ukweli. Pasipo Yesu hakuna mtu anayeweza kusamehewa zambi zake. Pasipo Yesu hakuna mtu awezaye kuepuka azabu ya Jehenamu. Yesu mwenyewe alieleza ukweli huu wazi wazi.

Matendo Mema na Dini Haviwezi Kutuokoa

Soma kwa Sauti: Waefeso 2:8-9

Kuokoka ni zawadi ya Mungu kwetu. Tulipokea zawadi hiyo tulipo amini Yesu kama vile mwokozi wetu na kumualika aingie katika maisha yetu. Hatukupokea zawadi ya wokovu kupitiya matendo yetu mema kama vile kusaidia wamaskini na wasiyojiweza; ama kwa kufuata sharia za dini kama vile: maombi, kutowa sadaka, kufunga ama kwa kufanya matembezi ya kidini. Hakuna yule anayeweza kujivuna kwa kusema amejiokowa yeye mwenyewe!

Soma kwa sauti: Tito 3:5

Matendo yetu mema haya kutuokowa. Kujitahidi kuwa watu wazuri haikutuletea wokovu wa Mungu. Rehema za Mungu pekee kwa kumutuma Yesu ndizo zimetuleteya wokovu. Hii imewezekana kwa sababu Yesu mwenyewe alikufa kwa ajili yetu msalabani. Hakuna chochote kizuri kile ambacho tungetenda ili tuijokowe mioyo yetu na azabu ya Jehenamu. Jee, haufurahi kwa sababu umeyatowa maisha yako kwa Yesu?

Kwenda Kanisani Haiwezi Kutuokowa

Watu wamoja wanafikiri kwamba kuwa mwanamemba wa kanisa inaweza kuwaokowa. Wengine wanafikiri kwamba wameokaka kwa sababu wamebatizwa kwa maji mengi. Biblia haifundishi hivyo. Biblia inatufundisha kwamba, kwa njia ya kuweka tumaini letu lote (imani) kwa Yesu ndicho kinachowea kutuokowa. Kwenda kanisani haiwezi kutuokowa, lakini Mungu anataka twende kanisani.

Soma kwa sauti: Yohana 3:15-18

Wale wamuaminio Yesu wameokoka. Wale wanao kataa kumuamini Yesu wamehukumiwa na zambi zao wenyewe. Katika umilele, baada ya maisha haya, watahukumiwa mbele ya Mungu milele.

Kwa Nini Kanisa ni la Maana, ama la Muhimu?

Soma kwa sauti: Waebrania 10:24-25

Tunahitaji kila mara kuchukuwa mda wa kukusanyika pamoja na waamini wengine ili tupate kupeana moyo. Katika kanisa letu tuna komaa katika ujuzi na tukipata usaidizi kwa matatizo tuliyo nayo. Majifunzo yanatupatiya nguvu na kuwa waamini wenyewe mafanikio katika Kristo. Tunacho kitu ambacho tunaweza kutowa kanisani: upendo wetu, kuwapa wengine moyo. Tunatowa msaada kwa viongozi na wazee wetu, na kusaidia kanisa kimatendo. Tunatowa pia chakumi chetu na sadaka kwa kanisa ili wengine wapate kumujua Yesu na kukomaa katika Yeye.

Kuabudu Sanamu na Uchawi ni Machukizo Mbele za Mungu

Soma kwa sauti: Kumbukumbu la Torati 18:10-13

Mungu anachukia vitendo hivyo. Hii inahu pia kuzungumza na wababu zetu waliokufa. Vitendo hivi vyote viko chini ya laana ya Mungu. Havina ushirika wowote na kumuabudu Mungu mmoja wa kweli, Yesu Kristo. Kufanya kazi pamoja na mizimu huonesha kwamba hatutumaini kikamilifu kwamba Mungu anatushugulikia. Aina yoyote ya mizimu unayo itumikia itakuharibu kwa sababu ni pepo wachafu, wafanyao kazi na Shetani. Pepo hizo zitatupeleka mbali na ushirika wa kweli pamoja na Mungu.

Soma kwa sauti: Walawi 20:6-8

Tukiendelea kwenda kwa wafumu ama wapiga ramuli kwa ajili ya shida tulizo nazo, Mungu anasema kwamba atageuza uso wake usitutizame tena na katuondowa katika jamaa ya walio wake. Maandiko hayo yanaonesha jinsi Mungu hataki uchawi na ibada ya pepo wachafu. Kushirikiana na mapepo wachafu itatuharibu sisi na jamaa zetu. Hiyo ndio sababu ifanyayo Mungu kuchukia mambo hayo. Anachukia giza iingiyayo katika maisha yetu wakati tunapo shirikiyana na pepo wachafu.

Soma kwa sauti: Kutoka 20:1-6

Mungu anatuamuru tumu abudu yeye Mwenyewe. Kuabudu sanamu ama kushirikiyana na wafumu ama roho za mababu waliokufa ni machukizo makubwa mbele za Mungu.

Mungu anataka tuishi katika mibaraka yake, bali si chini ya hasira yake. Kuabudu miungu ama kuchunguza mambo kwa kuuliza watu wa giza ni kumkoseya Mungu, kupitiya hayo ulinzi na mibaraka yetu inaondolewa.

Soma kwa sauti: Yohana 8:44

Yesu alizungumza na watu wa dini ambao hawakumuamini. Aliwaeleza kwamba Shetani ndiye baba wa waongo. Yesu alisema kwamba Shetani anafanya kazi ndani ya watu kwa kuwadanganya. Shetani anadanganya kupitiya mapepo yake. Ikiwa umetumikiya pepo wachafu, unahitaji kuwekwa huru. Pepo hao wachafu watakudanganya.

Watakuelezea kwamba waweza kumutumikia Yesu na kuwatumikia wao pia.

Soma kwa sauti: Matayo 6:24

Hakuna mtu awezaye kuwatumikia mabwana wawili. Haiwezekani uwe mkristo ukitumikiya pia mashetani. Hauwezi kutumia uchawi na kumtumikia Yesu kwa wakati mmoja. Uchawi utaleta pepo wachafu katika maisha na jamaa yako. Pepo wachafu wanaleta giza, woga, na masumbuko. Mwanzo pepo wachafu hawa wataonekana kama vile wanasadidna na kama vile ni wema, lakini baada ya mda kidogo wataanza kusumbua. Pepo hawa wachafu wanataka kukuweka chini ya kifungo chao. Ni Yesu Kristo pekee ndiye aliye na uwezo wa kumuweka mtu huru, mtu aliye katika kifungo cha pepo wachafu.

Soma kwa sauti: Matendo 19: 18-19

Waamini wapya katika mji wa Efeso waliomba msamaha kwa ajili ya kutumikiya miungu na pepo wachafu. Wakachoma vyombo vyote vya giza walivyo kuwa wakivitumia hapo mbele. Waefeso walipo geuka wakristo, waliunguza vyombo vyote, vitabu na hirizi (uchawi) walivyo abudu na kutumia. Waliepuka kuwa na ushirika mara tena na vitu vyote walivyo tumia pia kukataa ushirika wa aina yoyote na mapepo. Walimupokea Yesu na hawakuhitaji mara tena vitu hivyo. Walitambua kwamba walikuwa katika utumwa wa vitu na vitabu vile. Wakachukuwa uamzi wa kuviharibu.

Kutumikia Miungu

Viitwavyo miungu ni vitu vivyote vile vichukuwavyo nafasi ya Mungu, ama chochote kile kinacho jidai kuwa kina/ana nguvu alizo nazozu Mungu. Miungu ni kila kitu ama mtu ye yeyote tunaye muabudu ama kujitowa kwake.

Soma kwa sauti: Zakaria 10:2 Wale wazungumzao na mapepo na kuomba miungu wanadanganywa. Mungu hasemi uongo. Tunapashwa kusikiliza yale asemayo Mungu kupitiya Biblia.

Soma kwa sauti: Marko 9:2-7 Mungu alizungumza na Petro, Yakobo, na Yohana sauti ikitoka mawinguni ikisema: “*Huyu ni Mwanangu mpandwa; Msikilizeni Yeye!*”

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 10:20-21 Miungu ambayo huabudiwa kwa ukweli ni mapepo ambayo hujifanya kama vile Mungu. Haiwezekani kushiriki maisha ya kikristo tukifanya kazi pamoja na mashetani. Tunapashwa kukataa mambo hayo na kujitenga nayo.

Ombo ili Usifungwe na Miungu, Pepo Wachafu, na Madini ya Uongo

Mambo yatajwayo hapa chini ndio tunahitaji kufanya ikiwa hapo mbele kabla ya kumpokea Yesu tumetumia ama kuabudu mambo ya machukizo mbele za Mungu:

1. Tubu zambi zako kwa sababu ya kutumikiya miungu na mapepo wachafu. Uombe mchungaji wako/kiongozi aweke mikono juu yako na kukuombea. Muombe pamoja maombi haya:

“Bwana Yesu, asante kwa sababu ulikufa msalabani kwa ajili yangu, na kumwanga damu yako kwa ajili yangu. Asante kwa kuingia maishani mwangu na kusamehe zambi zangu. Ninatubu kwa sababu ya kushiriki mapepo wachafu. Ninaelewa sasa kwamba hiyo ni zambi.”

“Ninaelewa kwamba unachukia vitu hivyo. Nina kataa [taja hivyo vitendo]. Ninamukemea Shetani na chochote alicho nifunga nacho

kupitia mambo hayo. Ninakemea shetani na kila pepo chafu yoteyote ile ambayo ilipata nafasi katika maisha yangu. Sote pamoja tunaamuru mapepo, yaondoka, katika jina la Yesu. Maisha yangu imewafungia milango milele.”

“Asante, Yesu, kwa kunifungua. Asante kwa kuniweka huru na uwezo wa Shetani. Naomba unijaze na Roho Mtakatifu wako. Natoa maisha yangu kwa jumla kwako.” Amen

2. Mchungaji/Kiongozi: Amuru mapepo, yaondoke katika jina la Yesu, ndani ya jamaa la mtu huyu na nyumba yake. Uyaamuru yasirudi tena.

3. Mshukuru Yesu kwa ajili ya kukubali damu yake yote imwangike msalabani. Mshukuru kwa kuwa amekuweka huru kutoka zambini na kifungo cha uchawi.

4. Omba kwa ajili ya kujazwa na Roho Mtakatifu wa Mungu: **“Yesu, nakusihu unijaze na Roho Mtakatifu wako.”**

Maswali :

1. Miungu ni nini? Towa mfano.
2. Ni dini gani iliyo na uweza wa kutuokowa?
3. Ni nani tunapashwa kuabudu na kumfuata?
4. Ni miungu ya aina gani iliyo katika jamii yenu?
5. Matokeo gani mabaya yaliyo onekana kwako, ndani ya jamaa lako na jamii lako kwa sababu ya kwenda kwa wafumu ; na kuabudu mizimu ama miungu ?
6. Mtu hufunguliwa na pepo wachafu namna gani?
7. Jee, tunaweza kutumikia dini mbili ama imani mbili tofauti? Kwa nini?

Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi wajifunze na kuweka kwa ufahamu andiko hili :

Yohana 14:6

“Yesu akawaambia, ‘Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.’ ”

Somo la 4

Ubatizo kwa Maji

Kwa ajili ya Mchungaji/Kiongozi:

Kabla ya kuanza kufundisha somo hili, ni vizuri kujitayarisha ili uhakikishe kwamba ubatizo utafanyika. Baadaye unaweza kuwalishwa wale wanao hitaji kubatizwa ni wakati gani na nafasi gani hiyo itafanyika. Ubatizo wa waamini wapya ni mda wa furaha na shangwe kwa kanisa lote.

Kumbuka kwamba tunawabatiza watu kwa ajili ya Kristo, si kwa ajili ya kanisa lako la mahali. Kuwa mwanamemba wa kanisa ni hatua nzuri kwao ambayo watahitaji kuchukuwa, lakini hiyo haina uhusiano wowote na ubatizo kwa maji. Kugeuka mwanamemba wa kanisa ni hatua nyingine tofauti ambayo watakayo hitaji kuchukua baadaye. (Tunaweka hii wazi ili mtu aeleta kwamba kuungana na kanisa haifanyi mtu awe mkristo.)

Umeamua kumwamini Yesu Kristo katika maisha yako kama vile Bwana na Mwokozi! Umejifunza tayari mambo ambayo Yesu ametayarisha kwa ajili yako, na umejifunza kwa nini Yesu ndiye njia pekee kwa kumujuwa Mungu. Tayari umeanza maisha mapya! Hatua ifuatayo unayohitaji kuchukuwa ni kubatizwa kwa maji.

Ubatizo ni Agizo

Soma kwa sauti: Matayo 28:18-20 na Marko 16:15-16

Yesu aliamuru wanafunzi wake [wafuasi] wabatizwe. Maandiko haya ya Biblia yanatuonesha wazi kwamba Yesu anataka wale watakao mfuata wabatizwe katika maji kama vile alama ioneshayo imani yao Kwake. Yesu anafundisha pia kwamba ubatizo ufanyike kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Ubatizo kwa maji ni jambo ambalo Yesu anataka lifanyike kwa kila mtu amfuataye.

Ubatizo kwa Maji ni Nini?

Kubatizwa ni kuchomvya, ama kuwekwa mwili wote kwa jumla ndani ya maji. Ubatizo wa Biblia si kumrushia ama kumwanga maji juu ya kichwa cha mtu. Biblia inafundisha kwamba ubatizo unapewa pekee kwa wale walio tubu zambi zao na kukiri kwamba wamechukua uamzi wa kufuata Yesu.

Soma kwa sauti: Warumi 10:9-10

Mtu anakiri imani yake katika Kristo wakati amemwani moyoni mwake.

Soma kwa sauti: Matendo 8:35-38

Filipo mwijilisti alimuelizea yule towashi Mwetiopia kuhusu Yesu. Toashi huyo aliamini aliyo yasikia na akaomba abatizwe – awekwe mwili wote kwa jumla ndani ya maji na baadaye aondolewe tena. Hii ni alama ama msemwa unaoonesha kwamba toashi huyu aliamini kweli ujumbe wa injili na kutaka kumfuata Yesu kwa ukweli. Tangu wakati wa Yesu, watu ulimwenguni pote walio mwamini walibatizwa kama vile alama ya uaminifu wao kwa Yesu.

Ubatizo kwa maji ni kuwekwa mtu kwa jumla ndani ya maji-mto ama kijito, bahari, ziwa, ama kisima cha ubatizo cha kanisa. Mchungaji anamchomvya mwamini mpya katika maji na kwa haraka anamwondoa tena. Tendo hili la ubatizo kwa maji linaonesha kwa wazi kwamba mtu

anataka kumfanana Yesu. Maana ya hiyo ni kutangaza hazarani kwamba umeacha zambi na umechukuwa uamzi wa kumfuata Yesu. Ubatizo ni hatua mhimu ioneshayo utiifu kwa Yesu.

Ubatizo wenyewe hautuokowi. Tuna pokea wokovu tunapo kubali kumpokea Yesu Kristo maishani mwetu. Ubatizo ni kutangazia watu hazarani kwamba tunataka kumfuata Yesu na kuishi kwa ajili yake. Wakati wa ubatizo unawekwa ndani ya maji kwa jumla, lakini si maji hayo yaletayo mabadikiko katika maisha yako. Ni nguvu za Mungu kuitia Roho Mtakatifu katika maisha yako—ndizo ziletazo mabadiliko.

Ubatizo kwa Maji ni Alama

Ubatizo wetu ni alama wa yale Yesu aliyo yafanya kwa ajili yetu: Aliteswa na kufa msalabani hapo Kalvari, Alizikwa, na baada ya siku tatu akafufuka. Vivyo hivyo tunaingia ndani ya maji (hii ni picha ya Yesu kufa na kuzikwa), baadaye tunaondolewa majini (hii ni picha ya Yesu kufufuka na kutoka kati ya wafu).

Ubatizo wetu ni picha kwa inje ionyeshayo kwamba tuna ambatana maishani na mateso ya Yesu, tunaonesha kwamba tomekufa kwa zambi na maisha yetu ya kale. Tumefufuka sasa kwa nguvu za Mungu ili tuishi sasa maisha mapya. Tunaonesha kwamba tunajitowa kuishi maisha mapya yanayo mpendeza Mungu, na kuishi katika kuheshimu maagizo ya Biblia Takatifu.

Kwa sasa maisha yetu yanaweza kuwa mibaraka kwa wale wanaoishi pamoja nasi, jamaa zetu, na jamii zetu. Tunapo batizwa tunatangaza mbele ya watu wote kwamba Yesu alikufa na kufukuka kwa ajili yetu.

Kufa kwa Zambi na Hai kwa Mungu

Tuendapo kwa Yesu na kutubu zambi zetu. Yesu anasamehe zambi zetu, na anatupatia uzima mpya.

Soma kwa sauti: Warumi 6:3-8

Kristo alikufa kwa ajili ya zambi zetu hapo Kalvari. Kama vile waamini wapya tumekufa kwa zambi na kwa nguvu za zambi katika maisha yetu. Maana ya hiyo ni kusema hatuhitaji tena kuishi katika maisha yetu ya zamani lakini tumejitowa kuishi maisha yampendezayo Mungu. Tunaweza kufanya hiyo kwa sababu ya nguvu za Yesu zilizo ndani yetu. Yesu alifufuka kutoka wafu, wala hatakuwa tena. Kwa sasa sisi pia tumefufuka na tupo katika maisha mapya, tukiishi maisha safi na yanayo mupendeza Mungu.

Soma kwa sauti: 1 Petro 2:24-25

Yesu alikufa ili tuishi maisha matakifu na tusianguke tena katika mitego ya zambi. Hii ndiyo mapenzi ya Mungu kwa ajili yetu.

Soma kwa sauti: Waefeso 2:1-8

Tunaweza kuishi maisha safi na mazuri tukiwa katika mibaraka mingi kutoka kwa Mungu kwa sababu:

1. Kristo alikufa na kufufuka kwa ajili yetu, pia
2. Tuu hai ndani ya Kristo na Yesu aishi ndani yetu. Nguvu zake zimo ndani yetu zikiwa na uwezo wa kutubadilisha ili tufanane na Yeye.

3. Zawadi ya neema ya Mungu imetuokowa sisi, si kwa sababu ya matendo yetu mema.

Ubatizo ni picha ya uamuzi wetu na kukubali kufa kwa zambi na kuishi maisha mapya ambayo Kristo ameleta kwetu kuditia msalaba. Kwa sasa nguvu za Mungu zimo ndani yetu, tunao uwezo wa kushinda zambi na mabaya. Tunao uwezo kusema "hapana" kwa zambi wakati tujaribiwapo na mabaya.

Ubatizo Kwa Maji ni wa Maana

Tunasoma habari za wakristo wa kwanza katika kitabu cha Matendo ya Mitume ndani ya Agano Jipya. Hao ndio watu wa kwanza walio mpokea Yesu kama vile Bwana na Mwokozi.

Soma kwa sauti: Matendo 2:36-42

Watu walipo sikiya ujumbe amba Petro alihubiri, wakatubu zambi zao na kumuamini Yesu. Ndipo Petro, mchungaji wa kanisa, akasema kwamba watu hawa wanapashwa kubatizwa. Hapo tunaona kwamba watu wampokeapo kristo, wanapashwa kubatizwa haraka iwezekanavyo.

Filipo alibatiza towashi Muetiopia kwa haraka. Petro alisema kwamba waamini wapya wanapashwa kubatizwa. Hawakungojea mda mrefu ili wapate kubatizwa. Unaweza kuomba mchungaji wako akubatize. Yeye atakuelezea ni wakati gani hiyo inaweza kufanyika.

Kuna mara wakati wa ubatizo, yule atakaye batizwa anaweza kuwaelezea wengine namna Yesu alivyo badilisha maisha yake. Mtu anaweza kueleza jinsi alivyo kuwa akiishi hapo mbele kabla ya kukutana na Yesu, na kwa sasa maisha yake yanakuwa namna gani baada ya kumuamini Yesu. Hotuba hii fupi inatolewa kabla mchungaji abatize mtu, hiyo inawapa moyo wengine waliofika kutazama jinsi ubatizo utakavyo fanyika.

Jee, Tayari Umebatizwa?

Ni jukumu lako kuomba mchungaji wako akubatize. Uamzi huu unapashwa kuwa wako wewe mwenyewe, si vizuru kushurutishwa na mtu mwengine. Na si vizuri kubatizwa kwa kuiga wengine. Utaamua kubatizwa kwa sababu umeamini Bwana Yesu Kristo na kwa sababu uko tayari kumuheshimu Yesu. Siku hii ni takatifu na ya maana sana kwa ajili yako!

Makanisa mamoja yanabatiza watu siku ile walio mpokea Yesu. Makanisa mengine yanatowa mafundisho ya zaidi kwa waamini wapya kabla ya kubatizwa. Njia moja ama nyingine kuhusu mpangilio wa ubatizo ni nzuri; lakini ni jambo la maana kuchukuwa hatua hiyo ya imani haraka iwezekanavyo.

Kila mtu aliye muamini Yesu tangu karne ya kwanza hadi leo alibatizwa kwa maji. Kwa njia ya ubatizo unaungana na ma miliyoni ya watu katika historia ya kanisa walio onesha wazi imani yao ndani ya Yesu Kristo.

Usiogope—kubatizwa ni jambo nzuri na la maana sana kuishi. Lakini ikiwa una woga wakuingizwa ndani ya maji, ni vizuri uzungumze na mchungaji wako kuhusu hiyo.

Siku ya ubatizo ni siku ya shangwe kwa jamaa lote la kikristo kanisani. Ni siku ambayo hautasahau maishani mwako, tarehe hiyo ni tarehe umetangaza wazi hazarani kumfuata Bwana Yesu, umetangaza pia kutii Neno Lake, Bwana asifiwe !

Mchungaji/Kiongozi—baada ya kusoma somo hili na kueliewesha wanafunzi vizuri, uliza ikiwa kuna wale ambao wanataka kumpokea Yesu maishani mwao. Ikiwa wako, omba pamoja nao na kuwaongoza kwa Kristo. Baadaye uliza ikiwa kuna mtu ambaye anahitaji kubatizwa. Baadaye uwaelezeetarehe na nafasi ambayo watakayo weza batizwa.

Maswali:

- 1. Nani anapashwa kubatizwa kwa maji?**
- 2. Ubatizo ni picha ya tendo gani ?**
- 3. Maana ya kutubu ni nini? (Kutubu ni zaidi ya kujisikia vibaya kwa ajili ya zambi uliozo zitenda, ni zaidi ya kusikiya haya kwa sababu zambi ulizo zitenda zinazo onekana wazi. Kutubu maana yake ni kuacha njia za zambi na kumugeukia Mungu, ili tupate msamaha wa zambi utokao kwa Kristo Yesu, na kuupokea uzima wa Mungu ndani yetu.)**
- 4. Ikiwa tayari umebatizwa, elezea kundi lako maana ya huo ubatizo kwako?**
- 5. Eleza kwa nini sasa tunaweza kushinda zambi na majaribu kwa sababu sisi ni wakristo?**



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi wajifunze na kuweka kwa ufahamu andiko hili :

Warumi 10:9-10

“ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.”

Somo la 5

Kuzungumza na Mungu - Maombi, Sifa & Kuabudu

Katika somo hili tutajifunza kuhusu umuhimu wa kuzungumza pamoja na Mungu kupitia maombi na maabudu. Hizi ndizo njia ambazo kama vile wakristo tunaweza kuzitumia ili tupate kuzungumza pamoja na Mungu, Baba yetu wa Mbinguni. Maombi ni njia ambayo tuitumiayo ili tupate kuzungumza na Mungu, na kumusikiliza pia akizungumza pamoja nasi. Tunapo sifu na kuabudu Mungu, tunaonesha upendo wetu kwake, tuna muinua, tukionesha kujitowa kwetu kwa Mungu, hayo ni moja wapo kati ya mambo yaliyo sababisha Mungu kumuumba mwanadamu.

Yesu Aliomba

Soma kwa sauti: Luka 5:16 na Luka 6:12

Tunasoma katika Maandiko Matakatifu kwamba Yesu aliomba mara kwa mara. Mara nyingi alienda mwenyewe nafasi iliyo ya ukimya ili awe na Babaye. Vivyo hivyo, unapoomba, unahitaji nafasi ya ukimya ambapo unaweza kuchukuwa mda kuzungumza pamoja na Baba yako. Nende nafasi isiyo kuwa na mauzi, mfano mahali ambapo watu wakizungumza ama mahali kunapokuwa kazi za kukuletea kelele ambayo inaweza kuchukua mawazo yako. Kama vile katika kila mazungumzo kati ya watu wawili kuna mtu mmoja anaye zungumza na mwengine akiyasikiliza yale mwenzio asemayo.

Kwa sababu ya kifo cha Yesu msalabani, kizuwizi kilicho kuwa kati ya Mungu na mwanadamu kwa sababu ya zambi kimeondolewa. Hakuna kizuwizi tena kati yetu na Mungu, kwa sasa tunayo mawasiliano ya ngambo mbili pamoja na Mungu, Baba yetu wa mbinguni. Mazungumuzo hayo yanaitwa maombi.

Wakati tunapo omnia tunapashwa kumujulisha Mungu mahitaji yetu. Baadaye tuchukuwe mda wa kusikiliza kile ambacho Mungu atakachosema. Kujifunza kusikia sauti ya Mungu inachukuwa mda na mazoezi pia. Tunafanya mazoweza ya mafikiri yetu kuwa kimya, mafikiri yasiwe na angaika na kuangalia mambo mengine bali yamuelekee Mungu.

Jee, kuna mambo ambayo ungehitaji uyazungumze pamoja na Mungu leo ?

Yesu Aliwafundisha Wanafunzi Wake Kuomba

Soma kwa sauti : Matayo 6:5-13

Yesu anatueleza kwamba tunapashwa kuomba, na anatupatiya moyo ili tuombe. Mungu anatupenda sana na anajua kile ambacho tunacho kihitaji, ijapohiyo anatalika ili tuzungumze pamoja naye.

Tuombapo tunakuja mbele za Mungu na kutafuta uongozi wake kwa ajili ya maisha yetu. Ni mda ambao tunaacha miyo yetu wazi, na kumwelezea shida zetu zote, matumaini yetu, na haja za miyo yetu. Tunaweza kumulilia kwa ajili ya mahitaji yetu, ama kumuomba msamaha. Tunaweza kuomba atuongoze na kutusaidia kwa ajlili ya mahitaji ya kila siku.

Soma kwa sauti: Wafilipi 4:6-7

Mungu anataka sisi tuzungumze pamoja naye, anataka tumujulishe mahitaji yetu yote katika maombi. Kama vile wana wa Mungu tuelewe kwamba Baba yetu wa mbinguni anataka kuyasikiliza maombi yetu kila mara. Tunahitaji kumutafuta kwa sababu ni Yeye mwenyewe aliye na uwezo kutuleteya suluhisho yakudumu kwa ajili ya shida na matatizo ya maisha ambayo imufikiayo kila mmoja wetu. Tusiyatumainiye mafikiri na uwezo wetu lakini tuyapeleke yote kwanza kwa Mungu kupitia maombi.

Soma kwa Sauti: 1 Petro 5:6-7

Mungu anakupenda na anataka umushirikishe kwa matatizo na mizigo uliyo nayo. Umutwike Mungu mizigo mizito yako, kwa sababu anakushugulikia na atakusaidia kupata suluhisho na jibu iliyo nzuri zaidi kwa ajili yako.

Tuombe Namna Gani?

1. Omba Maombi Yaliyo na Shabaa.

Soma kwa Sauti: Luka 11:1-13

Biblia inatufundisha kumuomba Baba aliye mbinguni ili atupatiye chakula chetu cha kila siku. Inatufundisha kumuomba Mungu atusamehe zambi tulizo zitenda, na kumuomba nguvu zake za ulinzi na kutuepusha na majoribu ya zambi. Si vizuri kukaa kimya pasipo kuomba kwa ajili ya mahitaji uliyo nayo ama yale ambayo unahitaji kupewa na Mungu. Mungu akusikia unapo omba.

Yesu anatufundisha kumuomba kile ambacho tunacho hitaji. Hatuhitaji kufanya maombi marefu kwa kusema mengi lakini, twende mbele ya Baba yetu aliye mbinguni na kumuelezea kile ambacho tunacho kihitaji. Tutumainie kwamba, Baba yetu wa mbinguni, atajibu mahitaji tunayo kwa njia nzuri inayo stahili. Kwa nini hiyo? Kwa sababu Mungu anatupenda na ametufundisha kumuomba kile tunacho kihitaji. Tunapo omba Mungu kitu chochote katika maombi, tunatumia imani yetu.

2. Usivunjiye Moyo

Soma kwa Sauti: Luka 18:1-8

Biblia inatufundisha tuwe wavumilivu katika maombi. Tuendelee kuomba hadi wakati tunapopata jibu kwa maombi yetu. Usichoke bali uendelee kuomba ukiamini. Mnogojee Mungu. Maana yake uombe, baadaye umushukuru Mungu kwa jibu lile ambalo analo lituma. Umuelezee jinsi umupendavyo na jinsi umtumainiyavyo kwa sababu Yeye anashugulikia mahitaji yako.

Chukuwa mda ukisikiliza, ukingojea Mungu akupatiye mwongozo. Kwa kuwa Mungu ana hekima nyingi, labda hata jibu hitaji lako kwa njia ama mda ule unao utumainia. Wakati mwengine Mungu anajibu kupitia njia usiyo itarajia.

3. Usiogope

Soma kwa Sauti: Matayo 6:25-34

Biblia inatufundisha tusiwe na wasiwasi kwa ajili ya vitu tunavyo vihitaji, bali tunahitaji kumutumainiya Mungu. Kuwa na wasiwasi haituleteyi jibu lakini itatufanya tusumbuke na kujisikia vibaya. Mungu pekee ndiye aliye na uwezo wa kutupatiya yale ambayo tunayo yahitaji.

4. Omba kwa Imani

Yakobo 5:13-16

Maombi ambayo tuna omba kwa imani yanajibiwa. Imani maana yake unaamini Mungu, na unamufahamu. Imani ina maanisha kwamba wamutumainia yule aliye na uwezo wa kubadilisha mambo yote ili yawe mazuri. Imani ya kweli ni mfano wa mtu akaaye kwenye kiti. Mtu anaweza kusema kuwa ana imani kwamba kiti kitachukuwa uzito wake wote vizuri wala hakitamuangusha; imani hiyo itaonekana wazi wakati unapo kaa ukiuweka uzito wako wote juu ya kiti hicho. Vivyo hivyo kuwa na imani ndani ya Mungu ni kuchukuwa uzito wako wote ama mizigo yako yote na kumutwika Mungu.

Unaweza kusema, “*Mungu wa mbinguni, ninahitaji kumpata mtoto. Ulimpa Ana mtoto, na mimi naamini kwamba hakuna kisicho wezekana kwako.*”

Unaweza kuomba, “Mungu, Baba yangu, ulimulisha mjane ambaye hakuwa na chakula. Nina amini pia kwamba una uweza wa kunilisha mimi na jamaa langu pia. Asante kwa wema wako kwa ajili yetu. Nina kuamini.”

Kuomba namna hii inaonesha kuwa una imani. Unaweza kumuomba Mungu akupatie kazi, akuponye, alete suluhisho kwa shida za jamaa yako na kanisa lako pia. Hii ni kuomba kwa imani. Inaonesha kwamba unamfahamu Mungu vizuri kwa kuwa unazungumza naye kama vile mwanamemba wa jamaa.

Haupashwi kuzungumuza na Mungu kama vile kalombalomba. Unahitaji kuzungumza na Mungu kama vile mwana aombaye babaye mkate. Mungu anakupenda na anataka kujibu kwa mahitaji uliyo nayo. Baada ya kuomba uanze kungojea jibu kwa ajili ya mahitaji yako.

5. Maombi Yanatupatiya nguvu

Tuombapo na kupata mda pamoja na Mungu, tunapokea hekima na uhodari. Tuombapo tunajifunza kumutumainia Mungu zaidi. Tuombapo tunaona maombi yetu yakijibiwa. Tuonapo maombi yanajibiwa imani yetu yakomaa pia. Kupitiya hiyo tunawapatia wengine moyo kupitia maombi yetu.

6. Kuomba Kwa Jina la Yesu

Soma kwa Sauti: Yohana 14:13-14

Kuomba kwa jina la Yesu maana yake ni kuomba Mungu kitu fulani kwa sababu ya Yesu. Kuna tumaini kwamba Mungu atatushili, si kwa sababu ya ukubwa wetu, ama kwa sababu tunastahili kusaidiwa na Mungu, bali ni kwa sababu ya yale Yesu aliyoyafanya kwa ajili yetu. Yesu alirudisha ushirika wetu pamoja na Mungu. Akafungua njia ili tuingie mbinguni, kwa ajili ya hiyo Mungu mbinguni anatusikiliza kwa sababu ya Yesu.

Kutumia jina la Yesu tunapo omba ni kama vile unakuwa na kibarua kioneshacho kuwa kitu fulani ni chako. Ina maana kwamba Yesu ametupatia kibali cha kuturuhusu kwenda kwa Mungu na kumuomba atusaidie. Unaweza kuomba, “*Mungu, ninakuomba umponye mtoto wangu, katika jina la Yesu.*” Mungu anasikiya maomba hayo na kuyajibu.

Zambi Zinazuwia Maombi Yetu

Tukitaka Mungu asikie maombi yetu na atupatие jibu, itakuwa neno la maana sana kutubu zambi yoyote ile tulio nayo katika maisha yetu, na tusi irudilie mara tena.

Soma kwa Sauti: Mezali 15:29

Mungu anasikiya maombi ya wale walio na ushirika mzuri naye.

Soma kwa Sauti: Isaya 59:2

Zambi zetu zinatuweka mbali na Mungu. Ikiwa tunataka Mungu ajibu maombi yetu, ni vema maisha yetu yawe safi mbele yake.

Soma kwa Sauti: Yakobo 5:13-16

Zambi zinaweza kuzuwia maombi yetu yasijibiwe. Tunahitaji kuomba ikiwa tunakuwa na mahitaji, pia kuwaalika watu wengine watuombeye.

Soma kwa sauti: Matayo 5:8

Walio na miyo safi, isiyo kuwa na zambi, hao ndio watakao muona Mungu.

Jee, Katika Maisha Yako Kuna Neno Ambalo Unahitaji Kutubu?

Saa hizi umuombe ukimualika Yesu asamehe zambi zako. Uondowe neno lile maishani mwako. Wakati moyo wako ni safi, njia yako ni safi mbele za Mungu ni wazi pia katika maombi kupitiya imani ndani Yesu.

Mda Wako wa Maombi

Ikiwa unataka kabisa kuzungumza na Mungu na kusikia sauti yake, itakuwa vizuru kuweka kando mda kwa ajili ya maombi. Watu wamoja wanachukuwa saa za asubui na wengine wanachukuwa saa za jioni.

Nichukuwe saa ngapi kwa ajili ya kuomba? Unaweza kuanza na dakika 10 na baadaye utatambua kwamba kuna mengi sana ambayo unahitaji kuzungumza na Mungu kwa ajili ya hiyo utahitaji mda mrefu kabisa. Utumiye mda wako vizuru uzungumzapo na Mungu.

Unaweza kuanza mda wako wa maombi kwa nyimbo za kusifu na kuabudu Mungu. Hizo zitatayarisha moyo wako kwa maombi na kumusilkiliza Mungu kabla ya kuleta mahitaji na haja za moyo wako kwake. Unaweza pia kuchukua mda kuomba na jamaa lako ama pamoja na marafiki zako.

Somo kwa ufupi:

Tumejifunza kwamba:

1. Maombi ni njia ya kuzungumza pamoja na Mungu kuhusu yale tunayo yahitaji katika maisha yetu, bali tuelewe kwamba tunahitaji kuweka kando mda kwa ajili ya kuzungumza na Mungu.
2. Tunapashwa kuomba kwa imani na kuomba katika jina la Yesu yale mambo tunayo yahitaji.
3. Tunahitaji kuwa wavumilivu katika maombi ikiwa kweli tunatafuta suluhisho la Mungu.
4. Zambi zazuwiya maombi yetu. Tutubu zambi mbele za Mungu na kuziacha.

Maswali:

1. Jee, umefanya tayari mpango wa kuomba kila siku? Mda gani wa siku ni mzuri zaidi kwako?
2. Jee, unaomba pamoja na wengine? Watu gani uombao pamoja nao?
3. Ujaribu kifikiri kuhusu watu wawili ama watatu ambaao unahitaji kuwaombeya. Ombeya hawa watu kila juma ukingojea kuona kile ambacho Mungu atatenda kwa ajili yao. Unaweza kuomba kwa ajili hitaji lolote lile: Kanisa lako, Mchungaji wako, rafiki zako ambaao bado hawaja okoka, jamaa lako; kijiji chako; jimbo lako hata na inchi yako.
4. Jee, waweza kutafuta mtu ambaye mtaungana naye katika maombi? Huyu ni mtu aliye na jinsia moja na wewe ambaye mnaweza kuomba pamoja naye kila mara. Mungu atakuongoza kwa mtu anaye stahili ambaye utakuwa ukiomba pamoja naye. Kila mmoja anaweza kufundisha mwengine jinsi ya kuomba pia kupeyana moyo wakati wa maombi.

Sifa & Maabudu

Kumsifu na kumuabudu Mungu hutokana na moyo wa shukurani kwa ajili ya upendo na wema ambaao Mungu aliyo utenda. Tuna muabudu kwa ajili ya kutangaza wema na ukuu wake. Tuna muabudu kwa moyo ujaaو upendo yule aliye tuumba, yule aliyekufa kwa ajili yetu.

Tunaabudu kanisani pamoja; tunaweza kuabudu pia pamoja na jamaa letu na hata kwa mda wetu wa kipekee wa maombi.

Kuabudu ni kutangaza kwa sauti makuu ambayo Mungu aliyo yatenda. Tunaweza kurudilia katika nyimbo ama maneno mambo makuu Mungu aliyoafanya kwa ajili yetu.

Kuabudu ni kumupa Yesu upendo wako, moyo wako, akili zako, na nguvu zako. Una muelezea Mungu jinsi alivyo mwaminifu, mkuu na mwema kwako.

Tunaweza kuingia kwenye uwepo wa Mungu kupitia mda wa sifa na maabudu, tukitumia maneno ya vinywa vyetu, mziki, nyimbo ama mziki ulio rekodiwa ama kwa kucheza.

Mda utakao fuata utakapokuwa ukiimba na ukimsifu Mungu, fikiria kuhusu maana ya maneno ya wimbo, ili sifa yako kwa Mungu iwe kamili.

Kuabudu

Tunapo abudu Mungu tunaimba ama kutangaza kwa sauti shukurani zetu kwake. Tunaimba kuhusu jinsi Yesu alivyokufa msalabani ili tupate kusamehewa zambi zetu, jinsi Yesu alivyo tuweka huru kutoka katika vifungo vyta Yule muovu, ama namna tunavyokuwa na shukurani kwake. Tunaweza kumuabudu Mungu wa milele aliyeumba vyote vinavyo tuzunguka.

Mungu hana mipaka kama vile wanadamu, Anajua kila kitu, Yuko kila nafasi, na hana mwanzo wala mwisho. Hakuna kiumbe chochote kinachoweza kufananishwa naye. Katika maabudu yetu tunaonesha kwamba ni Mungu mwenyewe astahiliye kupokea upendo wetu, kujitowa kwetu, na maabudu yetu, tukitangaza kuwa hakuna mwengine tumupendaye sana na tumtumikiaye isipokuwa Yeye.

Kwa Nini Tuna Abudu?

Tumeumbwa na Mungu ndani mwetu mkiwa kiu cha kuabudu. Kila mmoja wetu moyoni mwake ana kiu cha kuabudu muumba, aliye Mungu mwenye nguvu zote.

Watu wasio mjua Mungu mmoja wa kweli mara nyingi wana tafuta kitu kingine watakacho kiabudu. Kitu hiki kinaweza kuwa kitu chochote, mfano picha ya jiwe lililo chongwa, mti, mlima, sanamu, ama vitu ambavyo ulivyo navyo. Wamoja wanawaabudu wapiga mziki mashuhuri, wengine huabudu mtu anaye julikana sana, ama aina fulani ya imani. Wengine wana abudu mamlaka ama pesa. Chochote kile ambacho unacho toleya upendo wako, mda wako, ama kujitowa kwacho — ndicho unacho abudu. Wakristo wanapashwa kumuabudu Mungu wa mbinguni pekee yake.

Maswali:

- 1. Soma kwa Sauti: Yohana 4:23-24.** Ni aina gani ya waabuduo Mungu awatafuta?
- 2. Soma kwa sauti: Zaburi 100. Maandiko haya yanatuelezea nini** kuhusu namna tunapashwa kumuabudu Mungu?
- 3. Ni nini uliyo iabudu siku zilizo pita?**
- 4. Ni nani aliye kuumba ili umuabudu?** Ikiwa bado unaabudu kitu chochote kile ama mtu yeote yule tofauti na Bwana Yesu, hii ni wakati wa kutubu na kumfanya Yesu awe Bwana na Mwokozi wa maisha yako.

Mchungaji/Kiongozi: uwe tayari kumuongoza mtu huyu kwa Kristo.



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi lako kujifunza na kuweka kwa ufahamu andiko hili:

Wafilipi 4:6-7

“Msijusumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru, haja zenu na zifulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.”

Soma la 6

Kusikia Sauti ya Mungu

Umegeuka mkristo mpya aliye amini, na sasa wewe ni mwana wa Mungu. Kila mtoto anajua sauti ya mzazi wake. Somo hili litatusaidia kuelewa jinsi ambavyo tunaweza kuisikia sauti ya Mungu. Ukijifunza kuisikia sauti ya Mungu, hautahitaji tena kuyatumainia mafikiri yako mwenyewe ama uwezo wako wa kipekee kwa kuishi maisha yako. Lakini utahitaji kupata mwongozo na usaidizi wa wa Baba yako wa mbinguni.

Mungu anataka kukusaidia katika mipango yako na matatizo unayo yaishi. Anafanya hivyo kwa kukushirikisha kimawazo kupitia Neno Lake (Biblia Takatifu). Anakusaidia pia kwa kuzungumza na wewe kama vile mwana wake wa kiume ama binti wake. Kujifunza kuisikia sauti ya Mungu itakupatia uwezo wa kuchukua uamzi mzuri katika maisha yako ya kila siku.

Mungu anataka maisha yako yawe mazuri kwa ujumla. Anataka maisha yako yawe mazuri jinsi yanavyo stahili kuwa. Kumusikiliza Mungu na baadaye kuheshimu uongozi wake itakuletea baraka kwako wewe, kwa jamaa lako, na jamii yako, na kwa inchi yako kwa jumla.

Soma kwa Sauti: Mezali 3:5-6 na ujibu maulizo yafuatayo:

1. Mungu anataka wewe ufanye nini?
2. Mungu ana ahidi kufanya nini kwa ajili yako?

Mawazo ya Mungu

Soma kwa sauti: Isaya 55:8-9

Mawazo ya Mungu yako juu zaidi, makubwa, na mazuri sana kuliko mawazo yetu. Mungu anajua namna ya kutusaidia na atatuelezea namna tunavyo hitaji kutembeya. Atatupatiya majibu ambayo tunayo yahitaji.

Soma kwa sauti: Yeremia 33:3

Unapomuita Mungu atakujibu na kukuonesha mambo makubwa usiyo yajua.

Soma kwa sauti: Yeremia 29:11-12

Mungu ana mpango mzuri kwa ajili yako. Anataka umuombe [uzungumze pamoja naye]; atakusikiliza wakati wowote unapoomba. Mungu, Baba yako wa mbinguni, anataka ashirikishwe katika kila ngazi ya maisha yako, katika mipango yote mikubwa ni hiyo midogo ichukuwayo.

Mungu Anazungumza na Watu Wake kwa Njia Tofauti

Biblia inatufundisha kwamba Mungu anazungumza na watu wake kwa njia mbalimbali. Anazungumza zaidi kupitia Neno Lake lililo katika Biblia Takatifu. Mara ingine anazungumza nasi kupitia ndoto na maono, mara nyingine anazungumza nasi kupitia Roho Mtakatifu akiongea moja kwa moja nasi, ama kupitia waamini wengine. Biblia inaonesha kwamba Mungu anaweza kuchaguwa kuzugumza nasi kupitia malaika, lakini mara kwa mara anazungumza mwenyewe nasi kupitia miyo yetu. Hizi zifuatazo ni mojawapo wa njia ambazo Mungu anatumia kwa kuzungumza nasi:

1. Mungu Anazungumuza Nasi Kupitia Maneno Yaliyo Katika Biblia

Mungu anazungumza na watu leo kuitia maneno yaliyo katika Biblia Takatifu.

Soma kwa Sauti: Zaburi 119:105

Neno la Mungu linaongoza hatua za maisha yetu.

Soma kwa Sauti: Zaburi 119:9-11, na 18

Mwandishi wa maneno haya anatuonesha jinsi Neno la Mungu ni la maana sana kwake. Tunapo sikia na kutii Neno la Mungu, Neno hilo latuzuulia tusitende zambi na kutusaidia kuishi maisha matakatifu yampendezayo Mungu.

Biblia ni ujumbe wa upendo wa Mungu kwa ajili ya watu wote walio ulimwenguni, kwa watu wa luga zote, rangi zote, na vizazi vyote. Tukizara maneno ya Biblia Takatifu tutakuwa tumekosa moja wapo kati njia ya muhimu sana ya kusikiliza sauti ya Mungu.

Ni vizuri sana kuwa na zowezi ya kusoma Biblia yako siku baada ya siku. Kwa kufanya hayo utaanza kujifunza ni nini Mungu asemayo kuitia maneno yake matakatifu. Ikiwa hauna Biblia, ni vizuri uombe Mungu ili uipate! Mungu anataka uwe na Biblia. Unaweza pia kwenda nafasi ambayo watu wanasoma Biblia katika kundi ama kurudilia kwa ufahamu Neno la Mungu.

Ni jambo la maana sana kujua maneno ya Biblia kwa ufahamu. Mwisho wa kila somo utaona maandiko kwa ufahamu ambayo utakayo andika na kujifunza. Yatakusaidia kukomaa kiroho katika Bwana. Katika maandiko hayo wakristo wapewa ujuzi, ahadi, na kupewa moyo wanaposoma na kuyarudiliya kwa ufahamu maandiko ya Biblia.

Soma kwa sauti: 2 Timoteo 3:15-17

Maandiko ya Biblia yanatufundisha, yatuongoza, yatuonya makosa, na katuongoza katika wokovu. Biblia inatufundisha kuishi maisha safi yanayo mpendeza Mungu.

2. Mungu Anazungumza Nasi Kupitia Watu Wake.

Mungu anaweza kuruhusu mkristo mmoja kufundisha mafundisho ya Biblia. Ama Mungu anaweza kumtuma mtu fulani aje kukupatia moyo unapoishi katika mda mgumu. Mungu anaweza kuzungumza nawe na kukupatia ujumbe wa kumpelekea mtu fulani kanisani ama katika kundi lako (hii inaitwa neno la unabii).

3. Mungu Anazungumuza Nasi Kupitia Ndoto na Maono

Katika Biblia tunasoma jinsi Mungu anavyotumia ndoto (usiku) na maono (mchana) kama vile namna ya kutowa habari ama kusema watu wafanye hange (tahazari).

Soma kwa sauti: Matayo 1:18-21

Yusufu, mume wa Maria, alipata ndoto kutoka kwa Mungu.

Mifano:

Ndoto – Mwanzo 37:5-9 (Mtu mwengine aitwaye Yusufu aliona ndoto.)

Maono – Matendo 10:1-11 (Petro aliona maono.) Tazama pia **Isaya 6:1-4**.

4. Wakati Mwengine Mungu Anamtuma Malaika

Soma kwa Sauti: Ufunuo 1:1

Yohana alipokea ujumbe mrefu uliyo tumiwa na Mungu kupitiya malaika. Yohana aliona mambo mengi katika maono na akayaandika ili sisi tupate kuyasoma. Alichu andika Yohana kinaitwa kitabu cha ufunuo, kitabu cha mwisho ndani ya Biblia.

Soma kwa sauti: Matendo 12:5-11

Petro aokolewa na malaika aliye tumiwa na Mungu. Malaika alizungumza naye na kumupatia mwongozo.

5. Mungu Anaweza Kuzungumza Nasi Kupitia Sauti Inayosikika.

Moja kati ya njia nzuri ambayo tunaweza kumsikia Mungu ni wakati asemapo nasi kwa sauti. Ijapokuwa hii haionekani zaidi, Mungu atumia pia njia hiyo kuzungumza nasi.

Soma kwa sauti: 1 Samueli 3:4-10

Mtoto Samueli alisikia Mungu akizunguza naye kwa sauti inayo sikika.

Soma kwa sauti: Kutoka 3:4-20

Musa anazungumza na Mungu na Mungu anamjibu kwa sauti inayo sikika. Utajifunza namna gani Mungu anazungumza nawe unapo muomba, umtii, ili ukomae katika ushirika wako pamoja na Mungu. Mungu ana ujumbe wa kukupatia kuhusu maisha yako, na anataka kukutumikisha wewe ili uwasadie watu wengine.

6. Mungu Anazungumza Nasi kupitia Roho Mtakatifu

Sauti ya Mungu yatufikia kupitia Roho Mtakatifu aishiye ndani yetu.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 2:9-12

Roho Mtakatifu aliye ndani yetu anatuelezea mawazo ya Mungu na mambo mazuri ambayo Mungu anayo yapanga kwa ajili yetu. Tunapo mkubali Yesu kama vile Bwana na Mwokozi, Roho Mtakatifu wake anakuja na kuishi ndani yetu. Anatuongoza na kutupatia moyo kila mara ili tufanye chaguo lilolo nzuri. Anatuongoza ili tupate kuchagua kufuata njia iliyo nzuri.

Roho Mtakatifu ni Mungu aliye ndani yetu, anazungumza pamoja nasi. Jinsi tunavyo chukuwa mda pamoja na Mungu, tukimtafuta na kumsikiza, tunaweza kusikia Mungu akizungumza kwa sauti ndogo ya ndani, kupitia hiyo tunapokea kile tunacho hitaji kukijua.

Ngojea kwa Ukimya ili Umsikilize Mungu

Soma kwa sauti: Zaburi 4:4

Ngojea kwa ukimya ili umsikilize Mungu. Mara nyingi watu wanafanya makosa kwa kuwa haraka kuchukua uamuzi na kufanya mambo kufuatana na mawazo wanayo yataka. Wanatafuta uongozi wa Mungu baada ya kufanya mipango yao, wakifikiri kwamba Mungu atawabariki katika mipango walio panga wao wenyewe. Ikiwa tuna muweka Mungu pemberi katika mipango yetu ya kila siku, katika mawazo na maisha yetu, kuna uwezekano mwangi kuona mipango hiyo isifanikiwe ama isiendelea vizuri. Matokeo ya mwisho, ni kujisikia kuvunjika moyo na kuchanganyikiwa.

Soma kwa sauti: Zaburi 46:10

Kaa kimia ukielewa kwamba Mungu yuko karibu nawe. Mungu anataka ashirikishwe katika kila kitu maishani mwako. Mupatie nafasi kwa kujifunza namna ya kuisikia sauti yake maishani mwako. Hii itachukua mda na uvumilivu, lakini baadaye utaanza kusikia Mungu akizungumza nawe.

Mungu Anazungumza Nami

Biblia inasema kwamba Mungu anazungumza nasi. Kwa nini sasa tunashindwa kumsikiya?

Tunashindwa kwa sababu hatujaribu.

Tunashindwa kwa sababu tuna woga.

Hatuwezi kwa sababu shuguli ni nyingi na kushindwa kuziacha kwa mda.

Ama kwa sababu hatuweki mda pembedi kwa ajili ya maombi tuki kaa kimia ili tumsikilize Mungu.

Soma kwa Sauti: Yohana 10:2-5

Yesu alisema kwamba kondoo wake waijua sauti yake. Tunaweza kufanya mazowezi ya kusikia sauti ya Mungu na kujifunza kuijua sauti yake. Wakristo wataijua sauti ya Mchungaji Mwema na watakuwa tayari kufuata mwongozo wake.

Soma kwa sauti: Marko 1:35

Yesu alikuwa akiamka asubui na mapema ili aende nafasi ya ukimia akutane na Babaye ili wapate mda wa kuzungumza pamoja naye. Yesu alipata mda mara kwa mara wa kuzungumuza na Babaye katika maombi wakiwa nafasi ya ukimya, hiyo ilikuwa ikifanyika saa za asubui na mapema na hata kwa saa zingine za siku. Wakati huo Mungu alikuwa akizungumza naye wazi wazi na alimuelezea yote ambayo alihitaji kufanya.

Soma kwa sauti: Matendo ya Mitume 10:9

Petro alipanda kwenye chumba cha juu gorofani (nafasi ya ukimya) ili aombe.

Soma kwa sauti: Wakolosai 1:9

Paulo aliwaombea wamuaminio Kristo ili wapate kujua mapenzi ya Mungu kwa ajili yao. Mungu anataka uelewe mapenzi yake kwa ajili ya maisha yako.

Soma kwa sauti: Yohana 12:49-50

Yesu anasema kwamba anafundisha yale aliyo yapokea kutoka kwa Baba, hiyo imefanyika kuititia mda wa kuwa pamoja naye. Tunapashwa kufanya yale ambayo Yesu aliyo yafanya. Tunapashwa kutafuta nafasi ya ukimia ambapo tutazungumza na Baba tukiwa pekee yetu. Ni vizuri kila mara baada ya kuomba Mungu tuchukuwe mda wa kumusikiliza.

Jinsi unavyo kaa hapa leo na kusikiliza somo hili, unapashwa kusikiliza kwa makini yale yanayo fundishwa pasipo kutawanya mafikiri yako kwa mambo mengine tofauti. Ikiwa hausikilizi kwa makini, ama ukiwa hapa ukiyafikiria mambo mengine yanayo tendeka pahali pengine, utakosa kitu cha maana sana. Wala hauta elewa vizuri somo lote kwa jumla. Itakuwa vivyo hivyo kwetu pia ikiwa tunataka kusikia sauti ya Mungu. Tunahitaji kusikiliza kwa makini, kama si hivyo tunaweza kukosa kusikiya yale ambayo Mungu anayo tuelezea sisi.

Soma kwa sauti: Matendo 13:2-3

Roho Mtakatifu alizungumza na watu walio kuwa wakiomba na kutafuta kujua mpango wa Mungu. Unapo omba, tafuta nafasi ya ukimia, chumba ama nafasi ambapo hakuna mauzi ya watu wengine. Hili ni jambo Yesu alilofanya. Hata Petro alifanya hiyo pia alipopanda kuomba katika chumba cha juu gorofani. Mda huu tuna soma Neno la Mungu ama kurudilia maandiko tulio yaweka kwa ufahamu. Uimbe wimbo wa kikristo wa maabudu.

Msifu Mungu na kumushukuru kwa yale yote aliyo yatenda katika maisha yako, umuelezee pia matarajio yako, ndoto, na mipango uliyo nayo. Uombe akuongoze katika kazi zako zote. Baada ya hiyo kaa kimia na kuomba Mungu azungumze nawe. Omba Roho Mtakatifu akusaidie kuelewa wakati unapo sikiliza.

Somo kwa ufupi:

Ikiwa unataka kusikiya Mungu akizungumuza nawe, ni vizuri uanze mazowezi kila mara kwa njia ya maombi na kumusikiliza.

1. Weka pemberi mda wa kuomba kila siku. (Tumia dakika za kutosha).
2. Soma Biblia. (Ama nende mahali ambapo wanasoma Biblia ama sehemu ambayo maandiko ya Biblia yanarudiliwa kwa ufahamu.)
3. Mshukuru Mungu na kumsifu kwa ajili ya namna alivyo kubariki na jinsi alivyo kusaidia wakati wa shida.
4. Wakati unakaa katika ukimya, ufikiri kuhusu Mungu, na atazungumza nawe.

Mungu anazungumza na kila mtu; Anatumia njia mbalimbali kwa kuzungumza na kila mmoja wetu. Hatuwezi kumushurutisha Mungu kuzungumza nasi kwa njia ile tunayo itaka sisi! Lakini tuwe na uhakika kwamba Mungu atazungumza nasi. Mungu anazungumza na kila mtu amtafutaye kwa bidii. Hatazami miaka, umbo, cheo, rangi ya ngozi, ama unatoka katika jamaa ya aina gani ili azungumze nawe. Atazungumza nawe. Baada ya mda fulani utajifunza kujua sauti ya Mungu na kuelewa ni wakati gani anapozungumza nawe.

Maswali:

Mchungaji/Kiongozi, uliza maulizo haya ukiomba kundi lako liyazungumzie:

1. Unahitaji kufanya nini ili uanze kuisikia sauti ya Mungu?
2. Utatambua namna gani kwamba ni Mungu ndiye azungumza nawe? (Maneno uyasikiayo na mawazo upokeyayo yahitaji kukubaliana na mafundisho ya Biblia.)
3. Kwa nini unahitaji kusikiliza yale Mungu anazungumza nawe?

Namna ya Kutambua Sauti ya Mungu

Ukifikiri kwamba Mungu azungumza nawe lakini hauna uhakika kwamba ni Yeye, tumia mwongozo huu kwa ajili ya usaidizi:

1. Hakikisha kwamba moyoni mwako mna Amani kuhusu yale ambayo unafikiri kwamba Mungu anazungumza nawe. Mungu anampa mtu amani; bali Shetani analeta kuchanganyikiwa na woga.
2. Unaweza hitaji uhakikisho wa watu wa Mungu wengine kuhusu kile ambacho unafikiri kwamba Mungu anazungumza nawe.
3. Mara nyingine Mungu analeta uhakikisho kupitia maneno ya unabii. Tuelewe kwamba sherti maneno ya unabii yakubaliane na yale ambayo Biblia inafundisha.
4. Ukitisikiyacho kutoka kwa Mungu sherti kilette furaha moyoni mwako, na hakipashwi kuleta matengano kati ya watu wa Mungu.
5. Mungu anenapo nasi, maneno yale yamutiya heshima na kumuinua. Yale Mungu ayanenayo hayaleti kiburi ndani yetu.
6. Mungu hawesi kusema chochote kipinganacho na Biblia Takatifu. Maneno ya Mungu yanakubaliana kila mara na mafundisho ya Biblia.



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Mwalimu: Saidia kundi kujifunza na kuweka vesi na andiko hili kwa ufahamu.

Mezali 3:5-6

“Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atakuonesha mapito yako.”

Lesson 7

Neno la Mungu

Katika somo la 6 lililo tangulia, tulijifunza njia mbali mbali ambazo zatuwezesha kuisikia sauti ya Mungu. Moja wapo kati ya njia muhimu ya kuisikia sauti yake ni kusoma maandiko yaliyo andikwa katika Biblia. Tunaweza pia kutafakari Neno la Mungu, kutafakari inatusaidia kumukaribiya Yesu.

Soma kwa Sauti: 2 Timoteo 3:16-17 Maneno ya Biblia yana “*pumzi ya Mungu.*” Mungu ametupatia Neno Lake mnamo kuwa uhai wake na Roho wake. Tunaweza kuliamini Neno la Mungu, Biblia, kwa kuwa ni Mungu mwenyewe aliye litowa kwetu.

Neno la Mungu Litabadilisha Maisha Yetu

Kutafakari Neno la Mungu maana yake ni kujaza akili zako na maneno unayo yasoma ama unayo yajua; kuyafikiria, kutafuta kuelewa yanasema nini. Kutafakari maana yake ni kumufungulia Mungu moyo wako unaposoma ama unapo sikiliza maneno yale Biblia isemayo.

Biblia ni Neno la Mungu kwetu. Tunahitaji kujaza akili zetu na Neno la Mungu jinsi tunavyo jaza tumbo zetu na chakula wakati wa sherehe ama siku kuu. Neno la Mungu linapenya kabisa ndani ya akili zetu hata zaidi- Neno lapenya hata katika utu wa ndani, moyoni mwetu, na linaleta mabadiliko kwa mtu kuanzia ndani hadi inje. Tunapokula neno la Mungu tunajazwa na uzima, nguvu, na hekima, kwa kuwa pumzi ya uhai wa Mungu imewekwa katika Neno Lake.

Mungu anataka kuzungumza nawe kuhusu kazi zako za kila siku, mipango yako, matarajio uliyo nayo, uamzi, na hata kuhusu matatizo unayo yaishi ili upate kuelewa mapenzi yake katika kila jambo.

Neno la Mungu Lina Nguvu

Soma kwa Sauti: Waebriana 4:12

Neno la Mungu li hai na linafanya kazi katika maisha yetu. Linaweza kufanya mambo makubwa ndani yetu na kwa ajili yetu. Tusomapo Biblia tuelewe kwamba Neno la Mungu li “***hai tena lina nguvu***” linaweza pia kuhukumu mawazo na tabia zetu. Neno la Mungu latuongoza kutofautisha mema na mabaya, na kutofautisha njia za Mungu na za wanadamu hata na mawazo.

Soma kwa sauti: Isaya 55:10-11

Kusudi la Mungu linatimilika wakati Mungu asemapo maneno yake. Mungu asemapo kwamba atafanya kitu fulani, hakika kitafanyika. Hawezi kushindwa na kitu chochote; ni kuititia Neno Lake ndilo Mungu atumia ili shabaa yake itimilike kwa kila mmoja katika maisha yetu.

Soma kwa sauti: 1 Watesalonike 2:13

Tunapo lipokea Neno la Mungu na kuliweka katika vitendo, Neno hilo latimiza mipango ya Mungu na kusudi lake ndani yetu. Neno la Mungu linafanya kazi kwetu ili sisi pamoja na wengine sote tuwe katika hali nzuru ifaayo.

Yesu alisema, “maneno yangu ni roho na ni uzima pia” (Yohana 6:63).

Neno la Mungu linauwezo wa kumfungua mtu na pepo wachafu.
Neno la Mungu linauwezo kuwafufua wafu na kuponya wagonjwa.
Neno la Mungu linauwezo kufanya wale wanao teswa kucheza kwa furaha.
Neno la Mungu laweza kukupatia hekima na nguvu za kumfuata Yesu.

Neno la Mungu linauwezo wa kubadilisha watu, pia Neno Lake linauwezo wa kubadilisha jamaa, kijiji, mji hata kubadilisha taifa nzima.

Maswali:

(**Mchungaji/Kiongozi:** Kundi lizungumze kuhusu maswali yafuatayo.)

1. Ni kitu gani kinacho hitajika kubadilika katika maisha yako?
2. Hekima gani unahitaji kupata kutoka kwa Yesu?

Biblia ni kitabu kilicho tofauti na vitabu vingine vyote. Tunaposoma na kutafakari Neno la Mungu, Roho Mtakatifu anatumia maandiko hayo kuzungumza na mioyo yetu kwa njia ya ajabu na ya kipekee. Neno linakuwa hai na latufaa sisi na lafaa kwa hali zote za maisha yetu. Mungu alikusudia hiyo iwe hivyo. Wakati wowote Mungu asemapo, mambo yaanza kutendeka.

Soma kwa sauti: Matayo 4:4

Ni vizuru kila siku kula Neno la Mungu kama vile miili yetu inavyo hitaji kula chakula kila siku.

Neno la Mungu Latufunulia Kristo

Ikiwa tunahitaji kumjua Yesu vizuri, tunapashwa kusoma Neno la Mungu.

Soma kwa sauti: Yohana 1:1-14

Maandiko haya yanaeleza jinsi, Yesu, aliyeumba ulimwengu na vyote vilivyomo, alikuja ulimwenguni. Yesu akakataliwa na watu ambao aliowaumba yeye mwenyewe. Yesu anaitwa Neno la Mungu. Yesu ni nuru ya ulimwengu.

Kwa kujifunza Neno la Mungu tuna muelewa Yesu vizuri, Mwana wa Mungu. Kitabu cha Mwanzo kinatuelezea kwamba Mungu aliumba ulimwengu wote kupitiya Neno Lake, ulimwengu ukawa kwa uwezo wa Bwana Yesu Kristo.

Soma kwa sauti: Waembrania 1:2-3

Ijapokuwa Mungu alisema na watu kwa njia tofauti kwa karne nyingi, alitowa ujumbe wa mwisho kwa watu kupitia Mwanawe, Yesu Kristo. Kwa kujua hiyo, tunapashwa kuelewa vizuri yale ambayo Yesu anatuelezea katika Neno Lake, Biblia. Pia tunahitaji kutazama vizuri yale ambayo Biblia inatuelezea kuhusu Yesu.

Neno la Mungu Limetuokowa

Soma kwa sauti: 1 Petro 1:23

Neno la Mungu limetuwezesha kuzaliwa mara ya pili, kuwa hai mbele za Mungu. Kama vile Mungu alivyo umba vitu vyote kupitia Neno Lake, vivyo hivyo pia aliletu wokovu kwa wale wamuaminio kupitia Neno Lake. Ni

nguvu za Neno la Mungu ndizo ziumbazo imani katika miyo yetu ili tumuamini Yesu. Pasipo Neno hilo hatuwezi kumugeukia Mungu.

Soma kwa sauti: Warumi 10:17

Imani iongozayo mtu kwa wokovu na imani itakayo tusaidia kuishi vizuri inatokana na kusikia na kutii Neno la Mungu. Ni katika Yesu na kupitia Yeye ndiyo njia Baba aliyo itumia ili atimize kazi kubwa ya wokovu.

Kitabu cha Ufunuo kinasema kwamba jina la Yesu ni “*Neno la Mungu*” (Ufunuo 19:13).

Neno la Mungu Latupatia Nguvu

Soma kwa sauti: Zaburi 119:28

Tunapokuwa katika mafanikio Neno la Mungu linatupatia hekima na kutuweka nguvu. Ligeukie Neno la Mungu wakati mambo hayaendeki vizuri kwako; pia uligeukie Neno la Mungu wakati mambo yanapo enda vizuri.

Soma kwa sauti: 1 Yohana 2:14

Neno la Mungu linaloishi ndani yetu linatuweka nguvu; lina fukuza uwezo wa yule muovu.

Neno la Mungu Latuongoza katika Mafanikio na Mibaraka

Soma kwa sauti: Yoshua 1:8-9

Kutii Neno la Mungu na kuyafuata maagizo yake inatuletea mafanikio maishani. Kutafakari Neno la Mungu inaleta kuinuliwa na mibaraka kwetu. Hizo ni ahadi za Mungu kwetu tuzisomazo katika Biblia.

Unataka kufanikiwa maishani? Unataka kuendelea mbele? Ukitaka hayo weka maandiko kwa ufahamu na kuyatafakari, soma, sikiliza, na utii yote yaliyoandikwa kwa ajili yako katika Biblia. Kila siku unayo nafasi ya kujifunza mengi kuhusu Yesu na utii yale ambayo anayo kuelezea. Njia za Mungu si ngumu, lakini unapashwa kufanya yale ambayo Mungu anayo zungumza nawe.

Utii Neno la Mungu

Soma kwa sauti: Yohana 3:36

Kumtii Yesu inatupatia uzima; kumkataa Yesu na Neno Lake inaleta hasira ya Mungu.

Soma kwa sauti: Luka 11:28

Tunabarikiwa na Mungu tusikiapo Neno la Mungu na kulitii.

Soma kwa sauti: Matendo 5:29

Petro alielewa kwamba ni kitu cha maana sana kumheshimu Mungu. Mungu anatuelezea kuhusu yeye mwenyewe na kuhusu mwanawе katika maneno ya Biblia. Mungu anatuelezea kuhusu mapashwa yetu kwake, anatuelezea pia kuhusu mibaraka itokayo kwake katika maandiko ya Biblia. Hii ndio sababu Petro alimuelezea Yesu, “*wewe una maneno ya uzima*” (Yohana 6:63).

Tunapo tazama na kumsikiliza Yesu, tunaona na kusikia ni nini Baba anataka tujue kuhusu yale ambayo yanayo muhusu.

Watu wamoja wanaskia na wasoma yale Biblia iwaelezeayo lakini hawafanyi yale Biblia inasemayo. Maisha yao hayabadilike, wanabaki vivyo hivyo. Tunaposhindwa kuyatii maneno ya Mungu, tunapoteza hiyo nafasi

ya kumjua Mungu vizuri na kuwa na maisha yaliyo mazuri. Utii kwa mafundisho ya Biblia huleta kila mara mibaraka ya Mungu kwetu.

Neno la Mungu lina nguvu. linafungua vifungo maishani na kutupatia tumaini. Hii ndiyo sababu Zaburi 1:1-2 yasema "*Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri ya wasio haki; wala hakuketi barazani pa wenyewe mizaha. Bali sheria ya Mungu ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku.*"

Jee, unahitaji kubarikiwa? Ikiwa ndio, sasa utafakari, usome, na kulitii Neno la Mungu, Biblia.

Kutafakari Neno la Mungu

Kutafakari ni zoezi ya kwenda nafasi ya ukimya ili ukae katika hali ya maombi ukisoma Biblia yako. Wakati ufanyapo hivyo ujitahidi kuheshimu mambo yale uyasomayo. Uombe Mungu azungumze nawe wakati usomapo Neno Lake. Kutafakari ni kama vile kucheuwa kitu kwa uangalifu mara nyingi ili ukielewa vizuri, pia kukiweka katika vitendo maishani mwako.

Soma kwa sauti: 1 Petro 2:2

Tunapashwa kulipenda Neno la Mungu kama vile mtoto mdogo apendavyo maziwa. Hii itatusaidia kukomaa katika maisha yetu ya kiroho.

Soma kwa sauti: Wakolosai 3:16

Kutafakari ni kuliacha Neno la Mungu liishi katika maisha yetu: likitufundisha, likitushauria, na kulisha mioyo yetu kama vile chakula kizuri kwa ajili ya miili yetu. Tule Neno la Mungu!

Kutafakari ni kama kuitizama picha na kuangalia kila sehemu jinsi kila kipande kinaungana na kingine. Ukitazama maneno ya Biblia kuwa ni ya maana, utaanza kuona ukweli ambao utakao badilisha maisha yako. Mungu anazungumza nawe kwa njia hii. Elewa kwamba Yesu anataka kuzungumza nawe sana kuliko jinsi wewe unataka kuzungumza naye.

Ikiwa utahitaji kuwa rafiki aliye karibu sana na Mungu na kupata mafanikio katika maisha (yako mwenyewe, ya jamaa yako, kazini mwako, katika huduma yako, na afya yako), unahitaji kupata mda wa kusoma Biblia na kutafakari Neno la Mungu. Ujitowapo namna hii utaanza kuona mabadiliko mazuri yakianza kuingia maishani mwako.

Soma kwa sauti: Zaburi 19:7-8

Neno la Mungu linaleta nguvu mpya, hekima, na furaha kwako ikiwa unalitazama kwa uangalifu.

Soma kwa sauti: Warumi 12:1-2

Tumebadilishwa kwa kuwa mafikiri yetu yamegeuzwa kuwa mapya kupitiya Neno la Mungu. Hatuwezi kujibadilisha sisi wenyewe ili tuwe watu wazuri, vivyo hivyo hatuwezi kujiokowa. Ni neno la Mungu pekee ndilo linalokuwa na uwezo wa kutubadilisha na kubadilisha jamii zetu.

Namna ya kutafakari Neno la Mungu—Hatua za Usaidizi

- 1. Zowezi.** Ujiwekee mda kando mwenyewe kwa ajili ya kutafakari Neno la Mungu, ni vizuri zaidi kutumia ma saa za asubui (jaribu kuanza na dakika 30). Usianze kisha usiendelee. Usiache siku zipite pasipo kupata mda wa kuwa pamoja na Mungu na Neno Lake. Uwe na mpango wa kusoma –

utafute Biblia utakayo soma, sura baada ya sura, ama umuulize Mungu ni wapi utakapoanza kusoma? Kwa waamini wapya, ni vizuri kuanza na injili katika Agano Jipy. Injili ya Yohana ni kitabu kizuri cha kuanza nacho.

2. Uwe na nafasi ya ukimya. Nenda nafasi ya ukimya ili upate kulitafakari Neno la Mungu. Uondoke ili uwe nafasi ya kipekee pamoja na Mungu. Zima chochote kinacho weza kuchukuwa mafikiri yako mda unapokuwa pamoja na Mungu (radio, simu yako, ama muziki, ...).

3. Ujitayarische. Uwe na Biblia, kalamu, na karatasi. Usomapo, tumia ama weka mistari mahali andiko lolote lakuvutia. Uandike kile ambacho una sikia kuwa Mungu anasema nawe.

4. Jiulize mwenyewe maswali haya usomapo:

- a. Maandiko haya yanasema nini kuhusu Mungu?
- b. Maandiko haya yanasema nini kuhusu wewe? Ama jamaa yako, kanisa lako, jirani zako, inchi yako?

5. Aliko Mungu azungumze nawe. Andika vesi yoyote ile inayo kuvutia pia uiweke kwa ufahamu.

6. Ombo. Jinsi Mungu anakuwa akikufundisha, uombe kuhusu yale aliyo kuonesha. Utii yale aliyo kuonesha. Pia uviweke katika vitendo.

Maswali:

Mchungaji/Kiongozi, uliza maswali haya na kuomba kundi lizungumze kuhusu hizo swali:

1. Ni kitu gani cha maana sana ulichojifunza kuhusu Biblia katika somo hili?
2. Kwa nini unafikiri kwamba ni jambo la maana kutafakari Neno la Mungu?
3. Ni nini inayo tuweka nguvu tunapokutana na shida maishani? (Kula Neno la Mungu ni kama vile kula chakula)
4. Namna gani tunaweza kukomaa katika imani? (Kwa njia ya kusoma, kusikia, kutafakari, na kutii Neno la Mungu.)
5. Ni kitu gani tunapashwa kufanya ili tufanikiwe na kupata sifa ? (Yoshua 1:8-9)

Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi lako kujifunza na kuweka kwa ufahamu andiko hili:

1 Petro 1:23

“Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo; bali kwa ile isiyo haribika; kwa neno la Mungu lenye Uzima; lidumulo hata milele.”

Somo la 8

Mungu Yuko Namna Gani? (Kuelewa Jinsi Mungu Alivyo)

Kwa sababu hatuwezi kumuona Mungu kwa macho yetu ya mwili, hiyo inafanya mara nyingi tushindwe kuelewa jinsi Mungu alivyo.

Mungu yuko namna gani? Biblia inatuelezea kwamba asili ya Mungu ni Roho; hana mwili wa nyama kama huu mwili tulio nao, na hana nyama wala damu kama vile sisi. Mungu ni wa kipekee yuko tofauti na sisi katika maumbile, asili na tabia. Sasa ni namna gani tunaweza kujua jinsi alivyo?

Hata kama haujawai kumuona Mungu kwa macho yako, unaweza kuelewa jinsi Mungu alivyo kupitia usomi wa yale yanayo andikwa katika Biblia Takatifu. Utaelewa mengi zaidi tena kumuhusu Mungu anayekupenda kwa kuendelea kumuomba na kusikiliza yale azungumzayo na wewe kwa upekee.

Asili ya Mungu

Tunapozungumza kuhusu “asili ya Mungu” tunaona namna Mungu alivyo tukitizama alama za tabia ambazo ni za Mungu pekee yake. Mambo haya yanatufunulia jinsi Mungu alivyo.

1. Mungu ni wa milele

Soma kwa sauti: Zaburi 102:24-27

Mungu hana mwanzo wala mwisho; alikuweko na yuko, na ataendelea kuwa hata milele. Kila mwanadamu anakuwa na mwanzo na mwisho wake bali Mungu ni wa milele na ataishi milele.

Soma kwa sauti: 1 Petro 1:24

Watu waishi baadaye wanakufa. Maisha ya mwanadamu yanafananishwa na maisha mafupi ya mauwa, hiyo ni kuyalinganisha na uwepo wa milele wa Mungu. Maneno ayasemayo Mungu hayanyauki wala kubadilika; bali yanadumu milele.

Mungu ni wa milele; habadiriki kufuatana na jinsi miaka inavyo pita. Miaka yake haiongezekaki wala hazeheki kama vile sisi wanadamu; jinsi miaka inavyopita haimuongezei wala kupunguza maarifa yake, hekima wala uwezo wake. Hakuna wakati uliokuweko ambapo Mungu hakukuweko. Hana mipaka. Yeye ni wa milele.

2. Mungu ni muumba wa kila kitu

Soma kwa sauti: Mwanzo 1:1 na Matendo 17:24

Mungu ni muumba wa vitu vyote, vyote vionekanayo (mfano mimeya na wanyama) pia vyote visivyo onekana (mfano chembechembe, nguvu zifanyazo ulimwengu kuzunguka, hewa ambayo tunayo pumua na roho). Aliumba vitu ambavyo tunavyo vijua na vingine tusivyo vijua.

Vitu vyote vinavyo kuwa sasa na vyote vitakavyokuweko baadaye vimeumbwa na Mungu. Watu wanaweza kuunda vitu vipyta wakitumia vitu ambavyo vilivyoumbwa na Mungu. Kwa mfano kuundwa kwa vitu kupitia uvumbuzi wa kisayansi na teknologia hayo yote yafanyika, watu wakitumia vitu ambavyo Mungu alivyo viumba. Tunapashwa kumtii na kumuabudu Mungu pekee yake, bali tusiabudu vitu ambavyo vilivyo umbwa na Mungu.

Soma kwa sauti: Yohana 1:1-3 na Wakolosai 1:15-17

3. Mungu –Anaweza yote

Mungu ana mamlaka zidi ya vitu vyote alivyo viumba ulimwenguni pote.

Soma kwa sauti: Yeremia 32:17

Hakuna chochote kisicho wezekana kwa Mungu. Hakuna chochote kinacho weza kumzuwia Mungu wakati atumiapo uwezo wake. Anao uwezo wa kufanya chochote kile anacho kitaka. Bali, Mungu hutenda kufuatana na tabia yake, na yeze hutenda yote katika haki na wema wake.

Pepo wachafu wote na mamlaka yote humtii Mungu. Yesu alionesa jinsi upopo na bahari vilitii amri yake (Matayo 8:23-27). Kwa sababu Yesu ni Mungu, anao uwezo wa kutenda miujiza, hata kuwafufua wafu.

Soma kwa sauti: Marko 10:27

Ni Mungu pekee yake ndiye aliye na uwezo wa kuleta suluhisho ya kudumu kwa shida na masumbuko maishani mwetu. Yeye mwenyewe ndiye aliye na uwezo wa kutenda mambo yasiyo wezekana kwa mwanadamu kwa ajili yetu. Pahali pa kutegemea akili na nguvu zako, wala kuwatafuta wanadamu ili wakusaidie kupata suluhisho, ni vizuri tumtegemeye Mungu. Usiwaendee ama kuweka tumaini lako kwa wachawi, wafumu, ama watu wa giza-Mungu hataki tuingie katika vitu hivyo.

Soma kwa sauti: Kumbukumbu la Torati 18:9-11

Mungu anafukuza adui za watu wake. Ni maadui gani wakusumbua maishani leo? Zambi, magonjwa, umaskini, mabaya, ujinga, na kifo. Mungu ni mwenye nguvu zote, ana mamlaka zidi ya hivyo vyote.

Soma kwa sauti: Matayo 8:14-17

Yesu ana nguvu zidi ya magonjwa.

Soma kwa sauti: Matayo 8:28-33 na Luka 10:17-20

Yesu alionesa mamlaka yake zidi ya pepo wachafu.

Soma kwa sauti: Luka 7:11-15

Yesu alionesa mamlaka yake zidi ya kifo.

Ikiwa unaishi maishani mambo yanayo kuletea woga: ndoa yako, jamaa, jamii, ama inchi, unaweza kuchukua mahitaji haya na kuyapeleka kwa Yesu. Mtumainie Mungu kwa sababu atatenda akileta suluhisho kwa matatizo hayo. Uendelee kumshukuru na kumsifu kwa ajili ya jibu ailetayo.

4. Mungu anajua yote

Mungu anajua yote. Ujuzi wake hauna mipaka kwa njia yoyote. Mungu hahitaji kwenda shulenii ama kuwa na mwalimu kama vile sisi. Anaona katika moyo wa kila mmoja. Mungu anajua mateso ya moyo wako na matatizo unayo yaishi na anakujali, akikushugulikia pia.

Soma kwa sauti: Zaburi 39:1-4

Mungu anakujua kabisa; alikujuu kabla wewe hauja zailiwa.

5. Mungu yuko kila mahali

Soma kwa sauti: Zaburi 139:7-13

Mungu yuko kila nafasi. Haiwezekani tujifiche asituone. Mungu anatuona na anajua mawazo yetu hata yale tunafanya kwa siri anaona. Hakuna mahali ambapo tunaweza kujificha ili asituone.

6. Mungu ni Roho

Soma kwa sauti: Yohana 4:23-24 na 1Timoteo 1:17

Mungu ni Roho, hana mwili wa damu na nyama kama mwili huu wewe na mimi tunao. Haiwezekani umuone Mungu kwa macho uliyo nayo, ijapohiyo yeeye anakuona kwa mda wote na nafasi zote unapokuwa.

Yesu, Mwana wa Mungu, alichukuwa mwili wa nyama na maumbile ya mwanadamu alipozaliwa na Maria, aliyekuwa binti bikira. Mimba ya Maria ilikuwa tendo la kimiujiza ya Mungu. Yesu akageuka mwanadamu aliye na mwili na damu, ili ajue na kuelewa maisha yanakuwa namna gani kwa kuishi duniani. Bali Yesu aliishi maisha makamilifu pasipo kufanya zambi, alikuwa akiongozwa na Roho wa Mungu na Neno Lake.

7. Yesu ni Mungu

Yesu ni nani? Mungu ni nani? Maulizo kama haya yanaweza kuwachanganya wale ambaeo ni waamini wapya katika imani. Jibu fupi ambalo tunaweza kutowa ni kwamba Yesu **NI** Mungu. Yesu na Mungu ni umoja na sawasawa, tutajifunza mengi kuhusu hiyo katika somo lifuatato.

Yesu Mwana pekee wa Mungu, aliyetumwa kutoka mbinguni. Alikubali kutoka huko na kuja hapa duniani, akazaliwa kama vile mtoto wa wanadamu. Yesu alitumiwa na Mungu ili atuokowe kutoka zambini na kuturudisha kwa Mungu. Mungu Baba alimpatia Yesu jina liliilo juu ya majina yote na alimpatia haki ya kuongoza ulimwengu wote na vyote vilivymomo.

Soma kwa sauti: Waebrania 1: 1-3 na Wafilipi 2:4-11

8. Mungu ana ushirika na watu

Mungu alimuumba kila mwanadamu akitaka kila mtu awe na ushirika wa kipekee pamoja naye. Alimutuma Mwanawe wa pekee, Yesu Kristo, ili mimi na wewe tupate kumjua. Mungu alituma pia Roho Mtakatifu wake ili aishi ndani yetu, wakati tunapompokea Yesu maishani kama vile mwokozi Roho aingia ndani yetu. Hii ni tofauti na kwenda tu kanisani, ama kuheshimu sheria za dini kwa sababu tunamuogopa Mungu!

Soma kwa sauti: Yohana 20:11-18 na Matendo 17:28-29

Tabia za Mungu

Tusemapo tabia tunaangalia jinsi mtu alivyo ndani ya moyo, tunaangalia pia tabia zake. Tunaweza kusema, "Huyu ni mtu mzuri.", ama, "Huyu mwanamke ni mbaya." Tusemapo hivyo tunatazama tabia za mtu huyu, tabia ambazo zinatambulisha huyu mtu kama vile binadamu.

Katika tabia za Mungu yeye ni mtakatifu, ana upendo, ni mwaminifu, mwenye haki, na mwenye rehema. Maana ya hiyo ni kusema kwamba Mungu anaonesha hiyo katika yote aliyo yafanya na yale ayafanyayo hata sasa.

Mungu ni mtakatifu; hakuna mabaya ya aina yoyote ndani yake. Mungu ni mwenye haki; yote ayatendayo kwa watu ni katika haki na pasipo upendeleo; katika hukumu zake hadanganyiki kamwe. Mungu ni mwenye rehema kwa wale wamuitao ili wasaidiwe na kusamehewa. Tabia hizi ndizo Mungu anataka tuwe nazo katika maisha yetu ya kila siku sisi ambao tunao mwamini.

Mungu ni Mtakatifu

Soma kwa sauti: Isaya 59:1-2

Mungu ni Mtakatifu; hawesi kutenda zambi wala mabaya. Mungu ni mwema kabisa, mwenye haki, na mkamilifu. Kwa sababu yeye ni mtakatifu havumiliye kamwe zambi, anajitenga na uovu, zambi, na chochote kilicho na ushirika na zambi. Kwa sababu Mungu ni mtakatifu, ana azibu mabaya na zambi.

Watu wanaweza kuja mbele ya uwepo wa Mungu kupitia damu ya haki ya Yesu ambayo iliyo mwangika. Hivi ndivyo sisi kama vile wakristo tunaweza kumjua Mungu kama vile Baba yetu, kwa sababu tumemkaribia Mungu sababu Yesu alijitowa na kufa msalabani ili tuokolewe. Jee, unafurahi kwa sababu Yesu aliturudisha ili tuwe hai mbele ya uwepo wa Mungu ?

Kwa sababu Mungu ni mtakatifu, anataka sisi pia tuwe watakatifu (maana ya hii ni kujitenga na zambi, mabaya, rushwa na kuepuka uharibifu wa ulimwengu wetu kwa sababu tunapashwa kumfanana Mungu).

Soma kwa sauti: Waebrania 12:14 na 1 Petro 1:15-16

Mungu ni Mwaminifu

Uaminifu ni kujitowa kutenda yale ambayo umeahidia pasipo kubadilisha mawazo yako ama kuacha kutenda yale uliyo ahidia kufanya. Mungu ni mwaminifu katika mambo yote ayafanyayo. Hawezi kusema neno leo baadaye kesho alibadilishwe. Uaminifu ni wa maana sana katika jamaa zetu, ndoa, biashara na kwa watu wote walio katika jamii wanaweza kufanikiwa na kuishi kwa amani na maelewano.

Soma kwa sauti: 2 Timoteo 2:11-13

Mungu ni Kweli

Mungu ni mkweli katika yote ayatendayo. Mungu hasemi uongo kamwe ama kuwapeleka watu katika njia zisizo za kweli. Yeye mwenyewe ni kweli- ukweli wote unatoka kwake.

Jaribu kufikiria shida ambazo zinatokeya wakati watu hawaelezeyani ukweli wao kwa wao. Ujanja, ama kutokusema ukweli, unafanya watu

wasiaminiane, waogopane, na kuto kuwa na uhakika. Kukosa ukweli inaleta hata hasira, mafarakano, hata na vita. Kuwa mkweli ni tabia ya Mungu. Kuto kusema ukweli (kusema uongo) ni tabia za shetani, aliye adui wa Mungu. Kuwa mkweli katika yale uyasemayo na katika maisha uyaishiyo na yote uyatendayo ni kitu kinacho mfurahisha Mungu, na ni hivyo ndivyo anataka uishi na kutenda kwa ajili ya watu wengine.

Soma kwa sauti: Yohana 14:16-17

Mungu ni Mwenye Haki

Mungu ni mwenye haki. Maana ya neno hili ni kusema yeye si mkorofi, ni mwenye haki, hana upendeleo, ni mkamilifu kwa kila kitu. Mungu hawezi kutenda kitu kwa ujanja ama upendeleo. Mungu anataka pia tuishi na kutenda mambo yote kwa njia ya haki.

Mungu hasemi uongo; hawezi kusema kamwe kwamba kitu kibaya ni kizuri; hawezi akamtendeya mwenye haki kama vile mtenda mabaya.

Kwa sababu hizo ndizo tabia za Mungu hatupashwi kuwa watu wa upendeleo, ama wanao chukua rushwa. Mungu anawatazama watu wote ulimwenguni kuwa ni sawasawa na hana upendeleo kwa mtu yeyote. Kama vile wakristo tutende mambo kwa haki kwa kila mtu, na tuwe watenda haki katika matendo yetu yote.

Soma kwa sauti: Zaburi 89:14

Mungu ni Mwema

Mungu ni mwema, na anatenda yote kwa wema. Hawezi kutenda mabaya kamwe, na hawezi kutenda tofauti na asili ya wema wake.

Soma kwa sauti: Warumi 8:28

Ndani ya Mungu hamna ubaya wa aina yoyote; ubaya uliingia ulimwenguni kupitia uasi wa shetani kwa Mungu. Wanadamu pia wakaongeza mabaya mengi ulimwenguni kama vile matokeo ya zambi. Hii ndiyo sababu kuna vita, wizi, chuki, ujanja, vita na mabaya mengine mengi ulimwenguni. Mungu hakuumba ubaya, bali alimtuma Mkombozi ili watu, jamaa, jamii wapate kutoka katika mabaya wapokeye mambo mazuri kutoka kwa Mungu.

Mungu ni mwenye haki; anapashwa kuazibu zambi. Ijapo hiyo yeye ni mwema; anatowa msamaha wa zambi kupitia damu ya Yesu; na Mungu anatowa msamaha wa zambi kupitia damu ya Yesu. Mungu anataka kutusaidia maishani ikiwa tutamgeukia na kumuomba msaada.

Soma kwa sauti: Waebirania 4:16

Uje leo kwa ujasiri mbele ya Mungu katika maombi, tena bila woga umuombe leo akusaidie na utapokea msaada. Kwenda mbele ya kitu chake cha neema maana yake; yeye ni Mfalme aliye juu zaidi, na ana mamlaka yote ya kutenda vitu kwa ajili ya faida yetu.

Soma kwa sauti: 1Timoteo 4:8 na Waebirania 12:5

Kama vile baba wa hapa duniani anawaadibisha watoto wake ili wawe watoto wazuri. Ndivyo Mungu anavyotenda kwa ajili yetu. Anawaadibisha wale walio wake ili maisha yao yawe mazuri. Mungu anataka tuwe na matunda ya wema katika maisha yetu, ili watu wapate kumjua yule Mungu mwema tunaye mtumikiya.

Mungu ni Mwenye Rehema

Rehema hutokana na upendo. Rehema ni kuwaonesha wema wale ambao wako katika mateso na giza. Rehema ni kuonesha wema na kumpatia mtu samani wakati mtu huyu anastahili hukumu ama azabu. Rehema hupewa na wale waliyo na uwezo zaidi ama mamlaka kwa wale wasiyo stahili usaidizi bali wako katika hitaji la kusaidiwa. Rehema ni tabia ya kuwatazama watu na kusikia kwamba wanahitaji kuwasaidia kwa sababu ya shida na matatizo walio nayo, hata ikiwa hawastahili kusaidiwa. Wakati Mungu anapo tutazama sisi wanadamu, anaturehemu, zaidi wakati tunapokuwa na matatizo katika maisha yetu.

Upendo mkubwa ambao Mungu alio nao kwa ajili yetu ulimfanya awe mwenye rehema. Vivyo hivyo Mungu anapenda wewe na mimi tuwe wenye rehema kwa ajili ya watu wengine.

Soma kwa sauti: Waefeso 2:4-6 na Matayo 18:21-22.

Mungu ni Pendo

Biblia inatufundisha kwamba Mungu ni pendo. Si kusema tu kwamba Mungu ana upendo bali huo ndio moyo wake ambao ni upendo. Mungu anatupenda na anataka tupendane sisi kwa sisi pia. Yesu alipoulizwa amri kubwa ni gani, alijibu akisema ni: "kumpenda Mungu na kupendana sisi kwa sisi" (Matayo 22:36-39).

Wakati watu wanapendana wao kwa wao mambo mengi mazuri yana anza kuonekana katika jamii. Mungu ni pendo na matendo yake kwetu yaonesha upendo. Tendo kubwa la upendo wa Mungu ni kumutuma Yesu achukuwe zambi zetu msalabani na akafufuka kuwa Bwana wetu.

Soma kwa sauti: Yohana 13:34-35 na Yohana 14:23-24

Yesu anatuamuru tuwapende wengine. Kwa njia hii watu wataelewa kwamba sisi tu wafuasi wake. Upendo tunao uonesha unatoka kwa Mungu, ikiwa wewe una tatizo la kuwapenda wengine, uombe Bwana Yesu akusaidie ili uwapende watu wengine.

Somo kwa ufupi:

Kwa sasa tuna elewa kwamba Mungu ni wa milele, Mwenye Nguvu zote, na Anajua vitu vyote. Mungu ni mwenye upendo, mwaminifu, ni mwenye kweli, mwenye haki, na mwema. Kwa sababu ya tabia nzuri za Mungu zisizo badilika, unaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu atatenda wema kwa ajili ya maisha yako. Anataka kuleta matunda mazuri mengi maishani mwako ili akubariki na kuwabariki wengine. Umtumainie ye ye kwa sababu ana uwezo wa kukutunza na kushugulika kwa matatizo na shida zako zote.

Soma kwa sauti: Wafilipi 2:13 na Warumi 8:28

Maswali:

Mchungaji/Kiongozi, uliza maswali haya na kuacha kundi liyazungumzie:

1. Sehemu gani ya somo hii ilikusaidia kuelewa Mungu vizuri?
2. Ikiwa kila mtu katika jamii yako (ama jamaa) anaanza kuonesha mema, wema, rehema, na uaminifu, unafikiri matokeo ya hiyo itakuwa nini ama itasaidia namna gani?
3. Ni tabia gani ya Mungu ambayo uliyo ifurahia zaidi? Kwa nini?
4. Unaweza kubadilisha maisha yako yawe mazuri namna gani? (Kwa kusoma Neno la Mungu na kumjua Mungu vizuri; kwa njia ya maombi na kumuomba Mungu abadilishe maisha yako.)



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi lako kujifunza na kuweka kwa ufahamu andiko hili:

Warumi 8:28

“Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao, katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.”

Somo la 9

Mungu Mmoja wa Kweli

Mungu mmoja aliyeumba vyote na anaye mamlaka zidi ya ulimwengu wote ni Mungu wa Biblia. Alijifunua mwenyewe kwa watu kupidia Yesu Kristo. Yesu alisema: “*Yeye aniaminiye mimi, haniamini mimi bali yeye aliyenituma. Naye anitazamaye mimi, amtazama yeye aliyenituma.*” (Yohana 12:44-45). Mungu wa Biblia ndiye Mungu pekee wa kweli.

Wote waitwao miungu si Mungu kabisa. Walitengenezwa na mikono ya wanadamu (mfano miungu ya wahindi, Budha, Allah, mapepo, hirizi na vitu vingine vinavyo abudiwa). Kama vile tulivyo jifunza katika somo la tatu, watu pia wanaweza kuwa miungu, mafikiri ya aina fulani ama mambo yanayo chukuwa nafasi ya Mungu maishani mwetu.

Biblia inatuelezeya wazi kwamba Bwana, Mungu wa Biblia, ndiye muumba wa mbingu na inchi na vyote vilivymo. Ni yeye mwenyewe ndiye anaye stahili kuabudiwa na watu ambao waliumbiwa naye mwenyewe. Hakuna mtu, wala kiumbe, roho, ama sanamu ya kuchongwa istahiliyo kuabudiwa. Mungu hawezi kugawa kamwe utukufu wake na mtu yeyote ama kitu chochote, kugawa utukufu wa Mungu pamoja na watu ama vitu ni chukuizo kubwa sana machoni pake.

Soma kwa sauti: Kutoka 20:1-6 na Zaburi 78:58

(Mchungaji: angalia pia Yeremia 10:3-15)

Jina la Mungu ni Nani?

Soma kwa sauti: Kutoka 3:1-15

Katika andiko hili tunasoma jinsi Mungu alivyo lifunua jina lake kwa Musa kuwa yeye ni “Mimi Niko Ambaye Niko”, maana yake, Mungu ambaye kila mara alikuweko, na ambaye kila mara atakuweko. Jina hili latafsiriwa kwa sasa katika Biblia zetu kama vile “Bwana” ama “Bwana Mungu”. Wakati wakristo wanapo omnia mara nyingi wanamuomba Bwana, tunaweza kuzungumza na “Bwana”. Hili ndilo jina la Mungu Mwenyewe. Ni wa milele, ni muumba ambaye aliye kuweko na aokowaye.

Soma kwa sauti: Kutoka 6:2-3

Mungu Mmoja

Mungu anatuamuru tumutazame na kumuabudu yeye mwenyewe. Kumbukumbu la Torati 6:4-5 inasema: ‘‘*Sikiliza, Ee Israeli; Mungu wetu ni mmoja. Nawe mpende, Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote.*

Ni kitu cha maana sana kumuabudu Bwana Mungu, na kumuabudu yeye mwenyewe, kujitowa kumuabudu Mungu wa kweli ni ufunguo wa kubadilisha maisha yetu. Kumuabudu Mungu kunaleta mabadiliko katika jamii yetu na tumaini kwa inchi zetu.

Soma kwa sauti: Isaya 42:8 na 43:11-13

Mungu anatuelezea kwamba yeye ni Mungu mwenye vivu. Maana ya hiyo ni kusema hatavumilia kamwe yeyote anaye abudu sanamu ama miungu mingine. Atawaazibu wale wanao mkosea kwa njia hiyo, bali kwa wale wanao tii amri zake, Mungu huwatolea upendo wake pasipo kulipa chochote, anawatolea ukingo, na kuwapa ahadi nyingi nzuri za mafanikio.

Biblia inatufundisha kumuabudu Mungu mmoja wa kweli; hakuna Mungu mwengine tofauti isipokuwa yeye mwenyewe.

(**Mchungaji**: tazama pia: 1Timoteo 2:5; 1 Wakorinto 8:6 na Isaya 44:6-8.)

Utatu Utakatifu

Biblia inatuonesha wazi kwamba Mungu ni mmoja, inatuonesha pia kwamba yuko katika nafsi tatu: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Baba ndiye Mungu mmoja wa kweli, ambaye jina lake baba latumiwa kuwaita mababa wazazi wetu ulimwenguni. Baba alimpatia Mwana mamlaka zidi ya ulimwengu ili autawale. Mwana, Yesu, akaja kufa ili awaokowe wanadamu walio anguka zambini. Tunamuamini Yesu, na kupitia maisha yake, mateso, kifo, na ufufuko, tumeokolewa naye.

Roho Mtakatifu anatenda kazi kama vile mtumishi wa Mungu ulimwenguni na yuko ndani ya miyo yetu. Roho Mtakatifu alishiriki katika kazi ya uumbaji wa ulimwengu; Mwana alisema neno ili kuwepo uumbaji na ukawa. Wakati wa mwisho utakapotimia Yesu atauweka ufalme wake wa milele hapa duniani ndipo hapo atakapo chukuwa vyote alivyo navyo na kuvirudisha kwa kuviweka katika mikono ya Baba yake.

Inawezekana je Mungu Mmoja awe Katika Nafsi Tatu?

Watu wamoja wanadanganyika kufikiri kwamba wakristo wana abudu wa Mungu watatu. Hii siyo kweli. Biblia inafundisha wazi kwamba Bwana Mungu ni mmoja, ambaye anatenda mambo ulimwenguni kupitia Utatu Utakatifu wake:

Baba – Ni Mungu asiyeonekana na watu na ni yeye aliyeumba ulimwengu na vyote vilivyomo. Ni yeye aliye juu ya yote na aliyeumba vyote.

Mwana, Yesu Kristo – Ni Mwana wa Mungu, aliyetumwa ulimwenguni, alionekana na kujulikana na watu, na ni yeye aliye chaguliwa na Baba ili alete wokovu ulimwenguni.

Roho Mtakatifu – ni Roho wa Mungu, yeye afanya kazi ulimwenguni pasipo kuonekana, anaishi katika miyo ya watu waliozaliwa “mara ya pili”. Utatambua kwamba kila nafsi katika utatu ina kazi fulani, ama huduma, katika utatu huo.

Soma kwa sauti: Matayo 28: 19-20

Katika maandiko haya Yesu ana waamuru wamuaminio kuhusu yale ambayo wanapashwa kufanya ulimwenguni. Maandiko haya huonesha kwamba watatu hawa walikuweko na hawawezi kutenganishwa ndicho kijengacho utatu utakatifu

Soma kwa sauti: Kumbukumbu la Torati 6:4

Nafasi hii katika Biblia inatangaza wazi kwamba Mungu ni mmoja. Ikiwa Mungu ni mmoja, kwa nini izungumziwe tena kuhusu utatu wa Mungu? tutaelewa zaidi kupitia kuyachunguza maandiko ya Biblia.

Tuangalie mfano mmoja tunao usoma katika Mwanzo 2:24 : “Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.” Andiko hili linatuelezea kwamba mme na mke ni mmoja. Inatuonesha kwamba kuna muungano wakudumu kati ya watu hawa wawili tofauti. Watu wawili wanao zungumziwa hapa, Adamu na Eva, wakageuka kuwa mwili mmoja. Hapa tunaona mfano mzuri

ya namna watu wawili wanatazamiwa kama mtu mmoja. Kanuni hii inaonesha hata jinsi nafsi tatu za Utatu ni Mungu Mmoja.

Kitabu cha Mwanzo kinatuelezea hadisi ya uumbaji. Mwanzo 1:26 inasema "Mungu akasema, "Na tuumbe mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na inchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya inchi." Hapa tunasoma kwamba Utatu Utakatifu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu walikuweko wakati wa uumbaji wa ulimwengu. Walizungumza pamoja na kuchukua uamzi wa kuumba mwanadamu. Mungu akasema "Na tumuumble **mtu**" tena akasema "na watawale ... inchi." Neno **mtu** maana yake mwanaume na mwanamuke. Hii ni mfano ya watu wawili tunao watazama kama vile mtu mmoja.

Tuuangalie mfano unaoweza kutusaidia kuelewa vizuri mafundisho kuhusu Utatu Utakatifu wa Mungu. Jaribu kutazama avoka (parachichi, embe mafuta). Ina sehemu tatu tofauti (ngozzi, mnofu na mbegu) ijapo hiyo yote kwa jumla ni tunda moja. Kila sehemu ni tofauti ijapohiyo kila sehemu ni ya tunda hilo. Kila sehemu ina kazi yake na inafanana tofauti na sehemu zingine, bali kila sehemu ni ya tunda moja.

Yesu anazungumziwa kuwa ni "Mwana wa Mungu." Yeye ni umoja wa Utatu Utakatifu kwa sababu ya hiyo yeye ni Mungu aeneaye.

Yesu anatabiriwa katika maandiko ya Agano la Kale karibuni mara 300, na alichaguliwa na Utatu Utakatifu ili alete wokovu na urejesho wa waliopotea na kuhukumiwa ulimwenguni. Kuja kwa Yesu na kazi yake imeandikwa na kufunuliwa katika vitabu vya agano jipya.

Tumuombapo Mungu, tunaweza kuomba Mungu Baba, Yesu, ama Roho Mtakatifu. Wako umoja na Mungu mmoja. Usomapo Biblia utaona mara nyingi Mungu wakimuita Baba, Mwana (Yesu) ama Roho Mtakatifu.

Mafundisho ya Utatu Utakatifu si mepesi kuelewa, katika somo hili tulijaribu kutowa maelezo mafupi. Umuombe Yesu akusaidie kujua ukweli na kukupatia kuelewa zaidi.

Mungu Mmoja Pekee Katika Maisha Yako

Kama waamini katika Kristo tunahitaji sana kuwa waangalifu tusiwe na ushirika na vitu vyovyote ambavyo adui anaweza kutumia kwa kuharibu imani zetu. Tuepuke vitu ambavyo vinaweza kugeuka kuwa miungu katika maisha yetu na kutuharibu tusiwe na ushirika mzuri na Mungu.

Soma kwa sauti: Kutoka 20:3-5.

Neno **miungu** si neno ambalo linatumwiwa sana katika maisha yetu ya siku hizi. Ni neno linalo maanisha kitu chochote kinachoweza kutuvutia maishani ili tukiabudu, kukiamini, ama kumuweka mtu ao kitu kwenye mstari wa mbele kuliko kumuweka Mungu wa mbinguni mwenyewe.

Agano la Kale linaeleza kuhusu habari ya wana wa Israeli, waliowekwa huru na Mungu kutoka katika utumwa wa Farao, mfalme wa Misri. Baada ya kuwekwa huru na kutoka utumwani Misri, kwa ujinga wao waisraeli wakatengeneza sanamu ya ndama ya zahabu na wakaanza kuiabudu pahali pa kumuabudu Mungu wa kweli mwenyewe. Walitazama sanamu ya ndama hiyo kama vile ina uweza wa kuwabaraki katika maisha yao.

Soma kwa sauti: Mambo ya walawi 26:1

Hata leo watu wanaendelea kufanya na kuabudu sanamu za miungu walizo zitengeneza na mikono yao wenyewe, sanamu hizi zina ushirika na uchawi, vitendo vya giza, na madini ya uongo. Watu wanajidanganya wakifikiri kwamba vitu hivyo na matendo hayo ni vya miungu ama madawa yana uwezo wa kuwasaidiya, kuwaponya, ama kuwabariki. Vitu hivi vinaweza kuonekana kama vile havina mazara yoyote, kwa mfano: dawa ya bahati, sanamu, hirizi, ama vitu vilivyo na ushirika na asili zetu ama mapepo. Vitu kama hivi mara nyingi vinatazamiwa kama vile vina nguvu maalumu. Inawezekana kuwa na vitu vya aina hiyi ndani ya nyumba zetu labda, viliingia ndani ya nyumba kabla tumuamini Yesu kristo. Kama vile tulivyosoma katika somo la 3, vitu hivyo tunapashwa kuvikataa, kuviacha na kuviharibu. Zungumza na mchunjaji wako na umuelezee ikiwa una vitu vya aina hiyo nyumbani ama maishani mwako.

Soma kwa sauti: Isaya 46:9 na Wakolosai 3:5-6

Kuabudu sanamu inaweza kuchukuwa sura mbalimbali katika maisha yetu. Katika kuabudu sanamu mnaweza kuwa mambo tofauti: vitu vilivyo tengenezwa na mikono ya wanadamu, kuchukua mda wetu wote ama upendo wetu kwa vitu vya ulimwengu, mfano kama vile kupenda pesa, watu walio na mamlaka ama wajulikanao sana, pombe, uasherati, TV, madawa ya kulevyo, utajiri, internet, ama kazi zetu. Kumuabudu na kumtumikia Mungu wa kweli inaturuhusu kuishi katika mibaraka na ulinzi wa Mungu, kwetu sisi, katika jamaa, na jamii lote.

Soma kwa sauti: Matayo 6:24

Yesu alijuwa kwamba ni vigumu kupenda pesa na kumtumikia yeye. Mungu anataka tumtumikie na kumuabudu yeye mwenyewe. Tunapo tumia mda wetu na nguvu zetu kufanya mapenzi ya Mungu, anatupatia yale yote ambayo tunayo yahitaji. (Matayo 6:31-33).

Ni vizuri kulirudilia somo la 3 mara tena ikiwa una ulizo ama tatizo ya namna hii. Zungumza na mchungaji ama mwalimu wako kuhusu tatizo lako. Ikiwa una miungu, ama hirizi, ama una ushirika na wachawi/wafumu ama mapepo, utahitaji kuwekwa huru na vifungo hivyo. Rudilia mara tena somo la 3 na ukalisome pamoja na mchungaji wako ama kiongozi wako, na upate pia mda wa kuombewa.

Soma kwa sauti: 2 Wakorinto 6:16-18

Kama vile wakristo, tunahitaji kumuweka Mungu kwenye mstari wa mbele. Ushirika wako na Mungu ndicho kitu chenye kustahili kuwekwa kwenye mstari wa mbele, tofauti na kitu chochote cha ulimwengu. Kwa njia hii mutaishi pamoja na kufurahia mibaraka ya Mungu maishani mwenu.

Soma kwa sauti : 1 Yohana 5:20-21

Kama vile waamini, tumeunganishwa na Yesu, Mungu mmoja wa kweli. Hakuna Mungu mwengine ambaye tunahitaji kumuabudu ama kumtumikia isipokuwa Yeye. Tunahitaji kuwa waangalifu ili tujikinge na kuabudu miungu ama kuwapa nafasi katika maisha yetu na jamaa zetu.

Maswali:

Mchungaji/Kiongozi, uliza maswali yafuatayo kwa kundi lako na kuwapa nafasi ya kuyazungumzia:

1. Miungu ni nini ? (Kitu chochote, sanamu, ama mtu upatiaye mda mwingi, upendo, ama kumuamini — pahali pa kujitowa kwa Mungu wa kweli.)
2. Ni miungu ya aina gani ipatikanayo kati ya watu mnao ishi pamoja nao?
3. Kuiabudu miungu imeharibu maisha yako namna gani, jamaa lako, hata watu mnao ishi nao?
4. Ni sehemu gani ya somo hili ilikusaidia kumuelewa Mungu upya? (Soma kwa sauti: Wakolosai 3:5 na Matayo 6:24)



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi lako kujifunza na kuweka kwa ufahamu andiko hili:

1 Yohana` 5:20-21

“nasi tumo ndani yake yeye aliye wa kweli, yaani, ndani ya Mwana wake Yesu Kristo. Huyu ndiye Mungu wa Kweli, na uzima wa milele. Watoto wadogo, jilindeni nafsi zenu na sanamu.”

Somo la 10

Waelezea Wengine Kuhusu Yesu

Kuwaelezea wengine kuhusu Yesu inaitwa kushuhudia. Somo hili litakusaidia kuelewa namna gani unaweza kuwaelezeya wengine vizuri habari za Yesu, pia uwe mshuhuda asiye kuwa na woga unapo watangazia wengine imani yako kuhusu Yesu.

Katika Agano Jipya, Kitabu cha Matendo ya Mitume, tunasoma hadisi ya kanisa la kwanza hapo Yerusalem. Petro na mitume wengine walikuwa viongozi wa kanisa hapo.

Soma kwa sauti: Matendo 13:46-49

Moja kati ya vitu vya maana zaidi watu wa kanisa walifanya, ilikuwa kutangaza habari njema kwa kila mtu waliyo kutana naye.

Agizo la Yesu

Soma kwa sauti: Marko 16:15-16

Haya ni moja wapo ya maneno kati ya maneno ya mwisho ambayo Yesu alisema. Aliamuru wanafunzi wake kutangaza habari zake kwa kila mtu. Yesu alisema, "Mtakuwa mashahidi wangu" (Matendo 1:8). Shahidi ni mtu asemaye yale aliyo yaona, aliyo yasikia, na aliyo yaishi. Yesu anataka uwaeleze wengine kuhusu maisha yako mapya ndani yake.

Biblia inasema kwamba Yesu ni Shahidi Mwaminifu na wa Kweli (Ufunuo 1:5 na 3:10). Imeandikwa hivyo kwa sababu Yesu alikuja na kuwaelezea watu ukweli kuhusu Baba yake wa mbinguni. Yesu alifundisha kuhusu mambo yote aliyo yaona, aliyo yasikiya na yale aliyo yaishi pamoja na Baba wa mbinguni. Sisi pia ni mashahidi wa yale Yesu alitenda maishani mwetu, sisi pia tunahitaji kueleza hiyo kwa wengine.

Mchungaji/Kiongozi, uliza maswali haya: "*Jee, umewai kumuelezea mtu yeyote hadisi yako kuhusu jinsi ulivyo mpokea Yesu maishani mwako? Kama bado huja fanya hivyo, ni vizuri uanze kuwaelezea wengine habari hiyo.*"

Yesu hakusema kwamba ni wachungaji, wazee, ama wainjilisti, na mashemasi pekee ndio wanapashwa kuhubiri Habari Njema. Alisema kwamba yeyote amuaminiye anapashwa kutangaza imani yake. Mpango wa Mungu wa kuwafikia walio potea katika jamii yako ina maana kwamba Mungu anataka kukutumikisha wewe, pasipo kuangalia elimu yako, wala hajali ulicho kiishi katika maisha yako, wala hadisi ya jamaa yako. Mungu hajali umbu lako ukiwa mwanamume ama mwanamuke, tajiri wala maskini. Sote tuliomukubali Yesu maishani mwetu tunapashwa kutangaza imani yetu.

Soma kwa sauti: Matendo 11:19-20

Watu wa kanisa walitawanyika kutoka manyumbani kwao huko Yerusalem. Popote walipo enda walitangaza habari za Yesu. Walitangaza popote na kwa kila mtu habari hizo, kwa sababu upendo wao kwa Yesu ulikuwa mkubwa sana.

Soma kwa sauti: Matayo 28:19-20 Kazi yetu kama vile wakristo ni kuufikishiya ulimwengu wote ujumbe unaomuhusu Yesu, tukiwafundisha na kuwaongoza watu katika imani yetu ya kikristo.

Injili, ama Habari Njeme ni Nini?

Ni kitu cha maana sana kwako wewe uaminiye kuelewa vizuri ujumbe wa wokovu, ili upate kuwatangazia watu wengine habari hii njema kwa uhakika na ushujaa. Ujumbe kuhusu Yesu unaitwa Injili, ama Habari njema. Ni habari njema kujua kwamba zambi zako zinaweza kusamehewa na hauta pelekwa tena katika hukumu ya Jehenamu. Ni habari njema kujuwa kwamba unaweza kuwekwa huru na kufunguliwa na vifungo vyote vinavyo kufunga, ni habari njema kujua tena kama unaweza kuwa rafiki ya Mungu! Hii ndio sababu jambo hili ni maana sana kwa Yesu. Yesu anataka tutangaziye wengine habari hii njema. Kila mtu anahitaji kujua habari za Yesu!

Soma kwa sauti: 1 Timoteo 2:3-5

Mungu anapenda kila mtu, anataka kila mtu aelewé kuwa ye ye ni mwenye upendo, pia yuko tayari kusamehe. Watu wanaweza kumupokea Yesu ikiwa tuna watangazia habari zake. Mungu hakuwapa malaika kazi hii ama kutumia nguvu zake za kimiujiza kuwafanya watu wamuamini—amewapa kazi hii walio okolewa waitwao wakristo. Kila mmoja wetu amepewa kazi hii—vijana, wazee, wanawake, wachungaji, na watu wote waliyo kanisani. Kati ya watu hawa kuna wewe pia! Kuitangaza imani yako ni kitu ambacho waaminio wote wamealikwa kufanya.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 15:1-5

Maandiko haya yanatowa maelezo kwa ufupi kuhusu maana ya neno injili:

Yesu aliteswa na kufa kwa ajili ya zambi zetu;
Yesu alizikwa na baada ya siku tatu alifufuka kutoka kati ya wafu;
Leo hii Yesu ni yu hai, ni mzima ameshinda kifo na mauti.

Kila mkristo anapashwa kujawa maneno yaliyo katika andiko hili; hii ndio tunaita Injili na huu ndio ujumbe tunaopashwa kuwatangazia watu wengine.

Mchungaji/Kiongozi: Soma andiko hili mwenyewe kwa sababu ni ndefu sana kwa watu wako:

Matendo ya Mitume 10:34-48

Haya ni mahubiri ya Petro katika jamaa ya Kornelio. Tunasoma hapa sehemu ya mafundisho ya msingi kuhusu wokovu. Wakati Petro alipo waelezea watu kuhusu Yesu, aliwaelezea ujumbe wa injili. Tunapotaka wengine waokoke tunahitaji kuwahubiri Injili, hii ni shurti kwetu kuitangaza injili.

Sehemu Mbili ya Ushuhuda wako

Sehemu mbili ya kushuhudia; ama kuwaelezea watu wengine kuhusu Yesu, ni hizi:

1. Kutangaza injili. Soma mara tena 1 Wakorinto 15:1-4.

Mchungaji/Kiongozi: Uwaalike watu warudilie maneno yaliyomo katika andiko hilo:

Yesu aliteswa na kufa kwa ajili ya zambi zetu;
Yesu alizikwa na kufufuka toka wafu baada ya siku tatu;
Leo hii ni mzima.

Hayo maneno yaliyotendeka kuhusu Yesu ni Habari Njema ambayo tunahitaji kuwatangazia wengine.

2. Shirikisha hadisi ya maisha yako. Una hadisi ambayo unaweza kuelezea wengine kuhusu namna ulivyo kutana na Yesu na ni nini aliyotenda maishani mwako. Hadisi ya maisha yako ni ya kipekee na tofauti na watu wote. Labda utafikiri kwamba si ya maana hadisi hiyo, hadisi ya maisha yako ni ya maana sana kwa wengine, Mungu ataitumia kuwaleta watu kwake. Kuna watu ambao watahitaji kujua jinsi umempokea Yesu. Tafazali usijizuwie kuitangaza hadisi yako!

Hizi ndizo sehemu mbili kuhusu jinsi unaweza kutangaza injili. Unaweza kushirikisha hizi sehemu mbili kwa yule anaye hitaji kuokoka.

Usivunjike moyo wakati uzungumuzapo na watu ambao hawakujali wala hawataki kukusikiliza. Tangaza maneno ya injili, kwa sababu yenewe yana nguvu na Mungu atayatumia hayo kufanya kazi maishani mwa watu wasikilizao. Tangaza hadisi ya maisha yako kwa imani na Mungu mwenyewe atajishugulisha na mengine yanayo baki kuhusu hao watu.

Soma kwa sauti: Wakolosai 1:5-6

Injili inafanya kazi na kuleta matokeo maishani mwa wale wasikilizao.

Soma kwa sauti: 1 Petro 1:23

Neno la Mungu haliwezi kushindwa kufanya kazi maishani mwa wale tunao watangazia hilo Neno. Tangaza kwa sauti ili wasikie, baada ya hayo uwaombeye wale ambao ulio washuhudia habari za Yesu.

Ni Nini inayo Kuzuulia Kushuhudia?

Woga ndilo tatizo kubwa ambalo lawazuilia watu wengi kumshuhudia Yesu. Tunaweza kuogopa kwa sababu watu watatuchekilea, kutukataa, ama tunaweza kuhukumiwa kwa sababu tunatangaza habari za Yesu. Ijapo kuna shida hizo, tujue kwamba hayatuondolee mapashwa yetu ya kumtii Yesu na kuwatangazia wengine imani yetu. Ikiwa wewe una woga ufanye mambo mawili yafuatayo:

1. Uombe. Chukua woga wako uupeleke kwa Yesu na kumuomba akubadilishe na kukupatia ushujaa. Yesu ana uwezo wakukuponya nafasi ambapo kuna woga.

2. Uombe Mungu ili akuongoze kujua ni nani ambaye utakaye zungumza naye. Baadaye uombe Munguakupe hekima ili ujue wakati mzuri ni upi ili uzungumze na huyu mtu. Umuombe Yesu naye atakusaidia.

Umejifunza tayari kwamba jinsi unavyo komaa katika Neno la Mungu na katika maombi, utakomaa katika imani pia. Na jinsi unavyo endelea kutangaza habari za Yesu, utajifunza mengi na kujua vizuri namna ya kuwatangazia wengine habari za Yesu. Roho Mtakatifu yuko ndani yako na yuko tayari kukusaidia.

Hatari ya Kuto Kuamini Yesu

Soma kwa sauti: Yohana 3:16-18

Katika andiko hili Yesu anasema kwamba yejote asiyehu kuwa na Mwana wa Mungu ndani yake huyu hana uzima.

Watu ambao hawaja mpokea Yesu wanakuwa katika hatari ya kwenda Jehenamu ikiwa wametupilia mbali ama wamekataa Yesu. Ni jambo la muhimu sana kuwashuhudia wengine injili. Ikiwa mtu anakufa gafla pasipo kumpokea Yesu, huyo anaenda moja kwa moja hadi Jehenamu. Yesu hataki hiyo ifanyike, ndio sababu anakualika kutangaza Habari Njema yake kwa wengine.

Yesu anakupenda sana na alikufa kwa ajili yako. Kwa sasa yuko mbinguni, na huko anatuombea. Upendo wa Yesu kwa ajili ya kila mmoja wetu ni upendo mkubwa sana upitao akili zetu. (**Soma kwa sauti: Waefeso 3:14-19**).

Uombe Mungu ajaze upendo ndani moyo wako ili uwe tayari kuwafikia watu walio potea, na Mungu atafanya hiyo. Upendo wa Mungu ulio ndani yako utakuwezesha kutangaza habari njema kwa kila mtu.

Kanisa Lako Litakomaa

Wakati watu wa kanisa lako wanaanza kuwatangazia watu walio katika jamii yako Habari Njema za Yesu, watu wataokoka na kanisa lako pia lita komaa.

Uwafundishe waamini wapya ukitumia kitabu hiki cha *Kutembea Pamoja na Yesu*, uwafundishe namna ya kuanza hapo hapo kutangaza Habari Njema. Usikawie. Ikiwa utakuwa tayari kutii amri hii nyepesi ya Yesu, kanisa lako litaongezeka, litakuwa lenye na nguvu, na jamaa lako pia; na jamii litabadilika na kuwa nzuri.

Mara nyingi watu ambao tunashindwa kuwashubiria habari za Yesu ni watu wa jamaa zetu. Ni wale watu ambao tunaowajua vizuri. Unahitaji kuwa mvumilivu kwa jamaa lako. Kwa kuwa wanazowea kuwaza na kufikiria kuhusu yale uliyo yatenda kabla umuamini Yesu.

Yesu anasema: “*vivyo hivyo nuru yenu iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*” (Matayo 5:16).

Maisha yako yanazungumza kwa sauti kubwa sana kuliko maneno yako. Ni vizuri jamaa lako likutazame na kuona mabadiliko ndani yako, hapo ndipo maneno yako yatakuwa na maana unapo zungumza nao kuhusu habari za Yesu.

Waamini wa kanisa la kwanza walikuwa na imani kubwa sana wakafikia katika hali ya kupigwa, kufungwa hata kuuwawa kwa sababu ya kumfuata Yesu.

Soma kwa sauti: Matendo 4:1-4 na Matendo 8:4-8.

Ni wapi hawa waamini wa kanisa la kwanza walipata ushujaa huo wa namna hii, wa kushuhudiya imani yao? Yesu alijua kwamba walihitaji usaidizi wa Mungu kwa kushuhudia ujumbe wa injili. Hii ndiyo sababu Yesu alitupatia ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambao tutasoma katika somo la 11. Ubatizo wa Roho Mtakatifu unatupatia nguvu, ushujaa, na uhakika wa kushuhudia.

Maswali:

1. Mungu anataka umuelezee nani habari za Yesu?
2. Jee, umewai kushuhudia injili kwa mtu yeyote ambaye baadaye alimpatia Yesu maisha yake?
3. Kabla Yesu anyakuliwe na kurudi mbinguni, ni nini alituamuru kufanya?
4. Sehemu mbili za kutangaza injili ni gani? (Kushudia ujumbe wa injili ; na kuwashuhudia watu kuhusi hadisi ya jinsi tulivyo mpokea Yesu maishani mwetu.)
5. Jee, unaweza kurudilia maneno yaliyomo katika habari njema, injili?



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Uwasaidie kundi lako kujua andiko hili na kuliweka kwa ufahamu:

Marko 16: 15-16

“Akawaambia, ‘Enendeni ulimwenguni mwote, mkahubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.’”

Somo la 11

Ubatizo wa Roho Mtakatifu

Je, mmewai kumupokeya Roho Mtakatifu wa Yesu?

Unapompokea Yesu, hapo hapo anakupatia Roho Mtakatifu wake ili aishi ndani yako. Baada ya kuokoka Mungu anataka ubatizwe na Roho Mtakatifu. Ubatizo wa Roho Mtakatifu unaletwa maishani mwetu kwa nguvu za Mungu. Unahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu ili uwe na nguvu na uhakika wa kushuhudia Yesu kwa uhodari.

Ahadi Kutoka Kwa Mungu

Kwa wakati wa Agano la Kale Mungu aliahidi kutuma Roho Mtakatifu wake na kuwajaza watu wake.

Soma kwa sauti: Yoeli 2:28-30

Mungu aliahidi kumwanga Roho Mtakatifu wake kwa uwingi (si uchache tu) juu ya watu wake. Kati ya hawa watu kuna wanaume, wanawake, watoto na wakubwa, walio na elimu na wasio na elimu.

Ahidi Itokayo Kwa Yesu

Ujio huu maalumu wa Roho Mtakatifu uliahidiwa na Yesu pia.

Soma kwa sauti: Yohana 7: 37-39

Yesu alizungumza kuhusu Roho Mtakatifu akitiririka ndani ya watu kama vile mto wa maji ya uzima. Biblia inasema kwamba Roho Mtakatifu atatolewa kwa watu baada ya Yesu kutukuzwa. Hii ina maanisha kwamba Roho hanelikuja kabla Yesu hajainuliwa na kurundi mbinguni.

Soma kwa sauti: Matayo 3:1-11

Yohana Mbatizaji aliwaalika watu kutubu zambi zao. Yohana alihubiri kuhusu Yesu, na kusema kwamba atawabatiza watu kwa Roho Mtakatifu na moto. Hii ni ubatizo tofauti na ule ubatizo wa maji mtu aupokeyao baada ya kumuamini Yesu. Mchungaji anawabatiza waamini wapya kwa maji; bali Yohana anasema kuwa Yesu atapokuja na atawabatiza watu. Yesu atatubatiza (kutuweka kwa jumla) katika Roho Mtakatifu na moto. Ahadi hii ilirudiliwa na Yesu kabla ya kurudi kwake mbinguni.

Soma kwa sauti: Luka 24:45-49

Baada ya kufufuka kutoka kati ya wafu, Yesu aliwaelezea wanafunzi wake kwamba, watakuwa mashahidi wake kwa mataifa yote. Watatangaza mateso yake, kifo, na ufufuko wake na kuwaleta watu kwa toba na kumuamini Yeye. Wanafunzi walialikwa na Yesu kungojea katika mji hadi wakati Yesu atatumua **"ahadi ya Baba,"** ambayo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Soma kwa sauti: Matendo 1:4-8

Yesu aliwaomba wanafunzi wake wangojee Yerusalem hadi watakapo batizwa na Roho Mtakatifu. Yesu alisema kwamba baada ya kuja kwa Roho Mtakatifu watakuwa mashahidi wake kila nafasi ulimwenguni. Baada ya siku 40, ahadi ya Baba, ya kumtuma Roho Mtakatifu ikatimia kwa waamini. Siku hii maalumu inajulikana kama vile siku ya Pentekoste.

Ni kitu cha maana kuelewa kwamba yejote aliyetubu kwa kweli, na kukubali Yesu maishani mwake tayari anaye Roho Mtaakatifu aishiye ndani

yake. Ahadi ambayo Yesu anazungumzia katika kitabu cha Matendo ya Mitume ni jambo la pili ambalo tunahitaji kuishi ama kuliona baada ya kupokea wokovu; hii ni kuacha huru nguvu za Roho Mtakatifu—ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Usome katika andiko lifuatalo ni nini iliyo tendeka kwa waliyo muamini Yesu mara ya kwanza:

Soma kwa sauti: Matendo 2:1-4

Wanafunzi ni watu waliomuamini Yesu; walikuwa na Roho Mtakatifu ndani yao. Walikuwa wakiomba na kungojea ahadi ya Roho Mtakatifu, ambayo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Roho alikuja katika nyumba walimo kuwa kama vile ndimi za moto ambazo zilikuja na kutuwa juu ya vichwa vyao, na kukawa mngurumo na upepo mkubwa. Kwa njia hiyo waamini walikuwa wakibatizwa na Roho Mtakatifu.

Mungu akatuma upepo na moto kuwajulisha kwamba Roho Mtakatifu yuko hapo. Waamini wakaanza kusema kwa luga mpya ambazo hazikuwa zao. Wakasema lugha ambazo hawajawai kujifunza. Hii ni karama ya lugha ambayo kila aaminiye anapokea aombapo kubatizwa na Roho Mtakatifu. Leo hii hatuoni mara kwa mara ndimi za moto juu ya vichwa vyetu ama kusikia upepo, bali tunaelewa kwamba tayari Roho Mtakatifu ametujia kwa sababu tayari tumeanza kusema kwa luga mpya.

Baada ya kujazwa kwa wanafunzi, ama kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, kulionekana nguvu nyingi za kimiujiza zifananishwazo na “mito ya maji ya uzima” ambayo Yesu aliyoizungumzia. Wakawa na ushujaa wa kushuhudia Yesu. Roho Mtakatifu alitenda kazi ndani yao kwa nguvu na kwa njia ya kimiujiza, nguvu walizo pewa na Mungu.

(Mchungaji/Kiongozi: Soma usomi huu mrefu mwenyewe ikiwa itakuwa vigumu kwa watu wako kuusoma: Soma kwa sauti: Matendo 2:5-39)

Petro na waamini wengine walikuwa wenyе furaha na kujaa na Roho wa Mungu, hiyo ikawafanya waseme luga mpya kwa sauti kubwa. Watu waliyo kuwa hekaluni waliotoka katika inchi zingine wakasikia wakisema kwa luga zao, wakashangaa! Hakuna mtu aliye elewa jinsi mambo kama hayo yangetendeka, kwa sababu wanafunzi hawakujua luga zile! Petro akasimama na kuwashubiri habari njema kwa watu walio kusanyika hapo. Watu elfu tatu wakatubu zambi zao na kumpokea Kristo kama vile Bwana na Mwokozi wao.

Hatuwa za Maana Kwako

Unahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu ili uwe na nguvu na uhakika wa kushuhudia habari za Yesu. Roho Mtakatifu alimpa Petro nguvu ya kuwashubiri maelfu ya watu. Kanisa la kwanza lilielewa kwamba kupokeya ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kitu cha maana sana, na ni hatua ya maana sana katika maisha ya wale ambao tayari wamempokeya Yesu.

Soma kwa sauti: Matendo 8:4-8 na Matendo 8:12-17

Filipo alihubiri habari za Yesu kwa watu wa samaria. Watu hawa walipomuamini Kristo, aliwabatiza kwa maji. Kisha Filipo akawaita mitume kutoka Yerusalem ili waje wawawekeye mikono hawa waamini wapya ili wapate kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Matendo 10: 33-48

Petro alihubiri habari za Yesu kwa umati wa watu walio kusanyika katika nyumba ya Kornelio. Watu wakaanza kumpokea Yesu wakati Petro alipo kuwa akihubiri. Watu walijazwa Roho Mtakatifu mda huo huo, na wakasema pia kwa luga mpya tofauti.

Soma kwa sauti: Matendo 19:1-7

Paulo alikutana na watu wenye bidii na kuwafundisha kuhusu Yesu. Baada ya kumuamini Yesu, Paulo akawabatiza kwa maji. Kisha Paulo akaweka mikono juu yao na wakapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, na wakasema pia kwa luga. Paulo alielewa kwamba ni jambo la muhimu kwa waamini wapya kupokea pia ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Wakati waamini wana batizwa kwa Roho Mtakatifu, ishara nyingi zinifuata, kama vile tulivyo soma katika maandiko ya Biblia yaliyo tangulia. Waamini wasema kwa luga mpya, wagonjwa wanapon, na wenye kufungwa na mapepo wakafunguliwa. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni nguvu za kimiujiza za Mungu zinazo tiririka kutoka ndani ya watu wake, kwa kufanya kazi ya injili.

Kipawa Kutoka Kwa Yesu

Roho Mtakatifu ni zawadi kutoka kwa Mungu, ilio ahidiwa kwetu sisi waaminio miaka mingi iliyo pita. Ni wale pekee walio amini, hao walio zaliwa mara ya pili ndio wanaweza kupokea kipaji hicho. Yesu ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu. Mara tunaita ubatizo huu "kujazwa Roho Mtakatifu."

Unapojazwa na Roho Mtakatifu, ni kama vile chupa lina mimiwa ndani maji na linajazwa hadi wakati chupa halipokei tena maji---maji hayo yataanza kumwangika, na kuenea kila sehemu. Sisi ni kama chupa hiyo. Tunasafishwa na Roho Mtakatifu naye aishi ndani yetu. Yesu anapotubatiza (ama kutuweka ndani yake kwa jumla) kwa Roho Mtakatifu, tunajazwa zaidi na Roho wa Mungu hadi anapo anza kutiririka-pamoja na neema yake, nguvu, uhodari, na utajiri wake.

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni zawadi itolewayo na Mungu na anataka upokeye zawadi hiyo.

Kupokea kwa Imani

Tunapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa imani, si kwa kufanya kazi kwa nguvu. Hakuna chochote ambacho tunaweza kufanya ili tustahili kupokea kipaji hiki. Tunamuomba Yesu kwa imani ili tumpokee, kama hivyo tulivyomuomba atusamehe zambi zetu na kuingia miyoni mwetu. Mara nyingine watu wanaweza mikono yao juu ya wengine ili wapokee kipaji hiki kutoka kwa Yesu. Lakini wakati mwengine mtu anaweza kupokea ubatizo huu akiwa katika maombi akiumuomba Mungu. Usifikiri kwamba hauwezi kupokea kipaji hiki kutoka kwa Yesu. Unacho hitaji kufanya ni kuomba tuu na kuamini, na utapokea.

Utajua kwa uhakika kwamba umepokea huu ubatizo wakati utaanza kusema kwa luga ambayo siyo yako, ama luga nyingine ambayo hauja wai kujifunza. Luga ambayo Roho akupatiyayo ni luga mpya. Hii ni muujiza wa Mungu kwa kuonesha upendo na nguvu zake kwako. Luga yako mpya ni luga ya maombi. Utahitaji kuomba kwa luga hii kila siku, pia mara kwa mara. Usikubali Shetani akuelezeye kwamba luga hii ama mambo unayo

yaishi hayatoki kwa Mungu ama sio ukweli. Imani yako itakomaa ukiendelea kuomba kwa roho (omba kwa luga).

(Mchungaji/Kiongozi, ikiwa unahitaji kujazwa na Roho Mtakatifu, omba maombi haya mwenyewe, kabla ya kufundisha somo hili. Wewe pia unaweza kupokea kipaji hiki ambacho Yesu aliahidia.)

Mchungaji/Kiongozi, uliza: “Jee, umewai kumuomba Yesu akujaze, akubatize na Roho Mtakatifu? Unaweza kuomba Yesu na kupokea kipaji hiki leo.”

Mchungaji/Kiongozi: omba maombi haya, msemwa baada ya msemwa: *“Bwana Yesu, asante kwa kuniosha zambi zangu na kuniokowa. Nina kuamini, nina kukubali kama vile Mwokozi na Bwana wangu. Ninakuomba, Yesu, unibatize kwa Roho Mtakatifu. Nipatie kipaji chako hiki kizuri. Nijaze mda huu Roho Mtakatifu. Asante kwa kipaji chako!”*

(Mchungaji/Kiongozi: Kwa sasa uwekee mikono juu ya mtu huyu ambaye anahitaji kujazwa kwa Roho Mtakatifu. Omba kwa luga ukimpa moyo mtu huyu kuomba pia. Roho Mtakatifu atamupatia maneno mapya ikiwa atatumia ulimi wake na sauti.

Umuombe huyu mtu asiombe kwa luga yake ya kizalikio, bali aseme maneno mapya ambayo anapewa na Roho Mtakatifu. Ikiwa kuna wengine hapo ambao tayari wamejazwa na Roho Mtakatifu, uwaombe wawaombee watu wako. Uwe na uhakika kuwa watajazwa Roho Mtakatifu kama vile Yesu alivyo ahidi.

Usiwasukume watu ikiwa kwa wakati huu watu hawasemi kwa luga, uwe mfurahivu na kuwapa moyo pekee, kwa kusema, “Mmeomba kipaji cha Mungu na tayari amewapatia; kwa sasa mnahitaji kupata mda wa kuwa pekee yenu pamoja na Yesu.” Uwaeleze jinsi watakavyo endelea kumsifu Bwana na kufungua miyo yao kwa Yesu, watajazwa na watasema kwa luga mpya.)

Kutumia Luga Yako Katika Maombi

Soma kwa sauti: Yuda 20

Unapoomba kwa luga, unajenga imani yako kwa Mungu maishani mwako. Kuomba kwa luga inakupatia nguvu kiroho, na inakuweka nguvu kiimani. Unahitaji kuomba kila siku kwa luga ili nguvu za Mungu zitiririke kupitia wewe.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 14:18

Mtume Paulo aliomba kila mara kwa Roho. Ndivyo sisi pia tunahitaji kuomba.

Nguvu za Kumshuhudia Yesu

Ubatizo wa Roho Mtakatifu umepewa kwetu ili tuwe na nguvu za kumshuhudia Yesu. Yesu anatuelezea: ‘’mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yeresalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa inchi’’ (Matendo 1:8). Utakuwa na ushujaa mkubwa kuhubiri habari za Yesu utakapo pokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, ndipo utakapo tambua kuwa ni vyepesi kutangaza habari za Yesu. Jee, unataka kuwa tayari kuwahubiri wengine habari za Yesu kwa wepesi? Jee, unataka watu wamkubali Yesu

jinsi wewe ulivyo mkubali? Roho Mtakatifu ni kipaji cha Mungu ambacho alikiandaa kwa ajili yako, ili uwe na uhakika pia ushujaa wa kuwatangazia wengine imani yako.

Somo kwa ufupi:

Ulipokea Roho wa Yesu Kristo ulipotubu zambi zako na kuweka imani yako ndani ya Yesu kama vile Bwana na Mwokozi. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni hatua ya zaidi unayo hihitaji baada ya kuokoka. Upokeapo ubatizo wa Roho Mtakatifu unatii agizo la Yesu la kujazwa na Roho (Matayo 3:11, Matendo 1:5).

Umepewa ubatizo wa Roho ili uwe na nguvu na uhakika wa kumshuhudia Yesu. Kumbuka kwamba Yesu alisema: "*Mtapokea nguvu atakapowajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu.*"

Mtu anayejazwa Roho Mtakatifu ataonesha ushujaa na upendo mwingi kwa ajili ya Yesu. Hii ndio sababu Yohana Mbatizaji alisema kwamba Yesu atabatiza watu kwa Roho Mtakatifu na moto, Watu wajitoao, wampendao, na wamatumikiao Yesu mara nyingi watu wanasesma kuwa "*wana moto kwa ajili ya Yesu.*"

Roho Mtakatifu anatowa vipaji kwa wanamemba wa kanisa, mwili wa Kristo. Unaweza kusoma kuhusu karama hizi katika 1 Wakorinto sura 12 na sura 14, na pia tutasoma kuhusu karama za Roho Mtakatifu katika somo la 16 la kitabu hiki.

Neno la mwisho: Utambua kwamba kuelewa kwako kwa mambo ya kiroho, na kumjua Yesu Kristo kutakomaa unapobatizwa katika Roho Mtakatifu. Unapoishi jambo lolote katika haya, shukuru Mungu na kumsifu. Kumbuka kwamba tumepewa Roho Mtakatifu ili tupate kujua mengi kuhusu Yesu na kutusaidia kukumbuka maneno aliyo tufundisha Bwana Yesu (Yohana 16:13-14).

Maswali:

1. Ni nani Yesu aliahidi kututuma kabla anyakuliwe na kurudi mbinguni? (Roho Mtakatifu, ahadi ya Baba.)
2. Ni nani ana weza kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu? (Yeyote aliyetubu na kumuamini Yesu kama vile Bwana na Mwokozi.)
3. Kwa nini tumepewa ubatizo wa Roho Mtakatifu? (ili tupate kuwa na nguvu na ushujaa wa kuwatangazia wengine habari kuhusu Yesu.)
4. Jee, umewai kumuomba Yesu akubatize na ubatizo huu wa Roho Mtakatifu? Kwa nini ama kwa nini bado?

Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: saidia kundi lako kujifunza na kuweka kwa ufahamu andiko hili (uwasaidie kuweka kwa ufahamu):

Matendo ya Mitume 1:8 "*Lakini mtapokea nguvu; atakapowajilia Roho Mtakatifu juu yenu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa inchi.*

Somo la 12 Kanisa ni Nini?

“Ninyi mnasema mimi ni nani?” ndivyo Yesu alivyo uliza Petro. Petro, aliye kuwa mmoja kati ya wanafunzi wake wa karibu alijibu, akisema: “*Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye Hai.*” Yesu akamjibu Petro: “*Heri wewe Simoni Bar-yona, kwa sababu mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.*” (Matayo 16:16-18).

Yesu alisema kwamba atalijenga kanisa lake juu ya mwamba. Mwamba ambao Yesu asemao siyo mtu, bali ni juu ya neno lile, lililo nenwa na Petro. Petro alijua kwamba Yesu ni yule aliye tumiwa na Mungu ili aondoe zambi za ulimwengu, na Petro alisema hiyo waziwazi.

Ulipo muomba Yesu akusamehe zambi zako na kuingia katika maisha yako, wewe pia ulifanya tamko la imani katika Yeye. Ukakubali kwamba Yesu alikufa msalabani ili aondoe zambi zako, na alifufuka kutoka wafu ili akuokowe. Yesu akageuka Mwokozi wako. Wewe pia ulifanya tamko hilo la imani kama alilo lifanya Petro. Tamko letu la imani ni mwamba ambao kanisa limejengwa juu yake.

Yesu aliahidi pia kulijenga kanisa lake (sisi) kwa nguvu zaidi ili kusiwe shambulizi lolote la shetani ambalo litaishinda.

Kanisa ni la Yesu

Kanisa limejengwa na kila aaminiye anaye ishi ulimwenguni sasa, na kila mkristo ambaye aliye ishi hata kama hayuko hai tena. Wakristo toka mataifa, jamaa, rangi, kabila na luga wote ni sehemu ya kanisa la Kristo ulimwenguni.

Soma kwa sauti: Wakolosai 1:12-14

Agano jipya linasema kwamba kanisa ni kundi la watu ambao wameitwa kutoka gizani ili wawe na ushirika pamoja na Yesu. Wakristo ndio walio na ushirika wa kipekee pamoja na Kristo kwa sababu wame amini kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu aliye tuokowa.

Soma : 1 Wakorinto 6:17-20 na 1 Petro 1:18-19

Yesu alitununua kwa kumwanga damu yake msalabani. Yesu alinunua kanisa (watu wake) ili wawe wake milele. Neno kuokoka maana yake ni kukombolewa na Mungu kuitia Yesu.

Soma kwa sauti: 1 Petro 2:9-10

Sisi ni uzao teule wa Mungu na tumeitwa ili tutangaze sifa zake ulimwenguni. Katika andiko hili kumeandikwa kwamba tumechaguliwa na Mungu na kwamba tunapokea rehema kutoka kwa Mungu.

Kazi yetu ni kumushuhudia Yesu ulimwenguni, kwa sababu sisi sote ni makuhani wa Mungu. Tume elezwa kuwa sote tumeondolewa kutoka katika giza na kwamba tunahitaji kuwa watakatifu (tunapashwa kuishi maisha safi na ya haki). Kujua kwamba Yesu alitununua kwa damu yake ingetufanya tuwe wenye shukurani na kutupatia furaha katika maisha haya mapya ambayo tumepewa naye. Sisi ni watu maalumu mbele ya Mungu,

na tunapashwa kuwaelezea wengine kuhusu yale aliyo yatenda Yesu kwa ajili yetu.

Kila Mkristo ni Sehemu ya Kanisa la Kristo

Kwa kuwa sasa unamjua Yesu, wewe ni sehemu ya kanisa lake. Unaweza kufikiria kwamba kanisa ni jengo ambamo watu wanakusanyikia kwa ajili ya kuimba na kumsikiliza mchungaji akihubiri. Hii ni kweli, bali Biblia inatuelezea kwamba **watu** waliomkubali Kristo kama vile Mwokozi **hao ndio kanisa**. Kwa sasa, ikiwa wewe umetubo zambi zako na kualika Yesu katika maisha yako, hiyo ina maanisha kwamba wewe ni mmoja wa kanisa lake la milele (hata ikiwa wewe ni wa shirika la kikristo tofauti katika jamii yako).

Katika agano la kale watu wa Mungu walijenga hekalu ambalo lilitumiwa kama vile nafasi ya kuabudiya Mungu. Baada ya kufufuka kwa Yesu, Alituma Roho wake ili aishi ndani ya watu walio muamini; kwa sababu ya yale Yesu alitenda, sisi wenyewe tumegeuka sasa kuwa hekalu la Mungu, mahali ambapo Mungu anaishi.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 3:16

Walio amini wana Roho Mtakatifu aishiye ndani yao. Pahali jengo iwe nafasi tuitazamayo zaidi kama nafasi ya kumuabudia Mungu, tuwaone walio zaliwa mara ya pili kuwa ndio wanaogeuka kuwa nyumba ya Mungu, kanisa.

Kanisa ni Mwili wa Kristo

Soma kwa sauti: Wakolosai 1:18

Kanisa linatazamiwa kama vile mwili wa Kristo; Yesu ndiye kichwa, na sisi ni viungo vya mwili wake. Tunaunganishwa na Kristo kama vile viungo vya mwili vinaungana na kichwa. Kama vile mwili wa mtu, kichwa ndicho kitowacho mwongozo kwa viungo vingine vyote vya mwili.

Kama vile mwana memba wa kanisa, sisi ni mwili wa Kristo, kwa hiyo tunahitaji kutii mwongozo wa Kristo, kwa sababu yeye ndiye kichwa. Mara nyingine kanisa la mahali linatizamiwa kama vile mwili wa Kristo, maana ya hiyo ni kikundi cha waamini wanao kaa sehemu fulani.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 12:12-30

Kuna mwili mmoja wa Kristo, bali kuna viungo vingi. Kila mmoja wetu ni kiungo cha mwili huu. Kila mtu ana kazi na kusudi pia katika mwili huu. Mfano, kazi ya jicho ni kuona, kazi ya sikio ni kusikia. Kila mmoja wetu ana kazi tofauti katika mwili huu. Kila mmoja wetu ni kiungo cha mwili wa Kristo, na kila mmoja wetu ana kazi, kwa kila mmoja wetu kuna kitu ambacho kilicho sababisha aumbiwe na Mungu. Tunahitaji kumuuliza Mungu ni nini kila mmoja wetu anapashwa kufanya katika mwili wa Kristo, kanisa.

Soma kwa sauti: Wakolosai 3:8-15

Tunapo pendana na kushugulikiana sisi kwa sisi tunaleta umoja katika kanisa. Hapo tutakuwa na moyo ya kumpenda kila mtu kwa kuwa Kristo yuko miyoni mwetu. Kama vile viungo vya mwili mmoja tunahitaji kufanya kazi kwa umoja pamoja na wengine walio viungo vya mwili huo, ili tutimize lile ambalo Mungu anataka tulifanye.

Ijapokuwa tuna karama tofauti, na kazi tofauti (kusudi) kati ya mmoja na mwengine, sisi sote tuu umoja pamoja na viungo vingine vya mwili wa Kristo. Mkono hauwezi kutupilia jicho, ama mguu uamuwe kusema kuwa ni

wa maana sana kuliko sikio. Kila mmoja wetu anahitaji kujitahidi kuishi katika maelewano na wengine ili utukufu umurudilie Mungu kwa njia hii.

Soma kwa sauti: Waefeso 4:28-32

Maandiko haya yanatowa kwa kanisa mwongozo kamili kuhusu namna tunapashwa kutembea na jinsi kila mmoja ana hitaji kutenda kwa mwengine.

Soma kwa sauti: Tito 2:14

Yesu alikufa ili atuokowe tutoke katika uovu, kwa hiyo tunahitaji kuwa tayari kutenda mema na kuonesha kuwa sisi ni watu wa Mungu.

Kanisa ni Jamaa la Mungu

Tunageuka sehemu ya jamaa la Mungu tunapomkubali Yesu kama vile Bwana na Mwokozi. Mungu anatuita wana wake na sisi tunamuita Baba yetu aliye mbinguni. Anatujali kama vile Baba anavyowajali wana wake. Anatufundisha na kutuadibisha wakati inapo hitajika. Mungu anazungumza nasi na yeze anataka tuzungumze naye kupitia maombi.

Soma kwa sauti: Yohana 1:12 na Wagalatia 4:6

Kila mtu aliyemukubali Kristo ni mwana wa Mungu. Tunapo kusanyika pamoja kama vile jamaa la Mungu. Tuwatendeye wengine kwa upendo na heshima, tuwatazame kupitia macho ya Mungu.

Soma kwa sauti: Wagalatia 6:10

Kama vile jamaa linavyo saidiyana. Kila mmoja anamtazama mwengine kuwa ni wa maana, ni wa samani. Mfano huu utusaidie sisi tulio viungo vya kanisa la Kristo. Kuwa na upendo wa ajabu kati ya wanamemba wa Mwili wa Kristo.

Kanisa ni Kundu la Kristo

Soma kwa sauti: Zaburi 23 na Yohana 10:11

Yesu ni mchungaji wetu. Sisi ni kondoo wake. Kama vile mchungaji anavyo chunga kundoo ama mbuzi wake, Yesu anatuongoza kwa usalama na anajibu kwa mahitaji yetu. Anatuongoza katika njia ziliyo nzuri. Tunaweza kutumaini kuwa yeze anajishugulisha kwa ajili yetu.

Soma kwa sauti: Waefeso 4:10-13

Mungu amekupatia mtu ambaye ni mwanamume ama mwanamke, aitwaye mchungaji. Mchungaji ni kiongozi wa kanisa na anashugulukia maisha ya kiroho ya kundi la Kristo. Mchungaji anatalisha Neno la Mungu, anatusaidia na kutuongoza, na kutufundisha pia. Mchungaji anatuombea, na kutuongoza ili tumfuate Mchungaji Mkubwa, Yesu. Ni vizuri umsikilize Mchungaji wako na pia umuombeye. Umuheshimu na kumusaidia kufanya kazi kanisani. Uwatangazie wengine habari za Yesu na kuwaleta kanisani.

Sisi ni sehemu ya kundi la Yesu na tunapashwa kuelewana na kila mmoja aliye kanisani. Kusudi la Mungu ni kwamba tuishi katika amani na umoja.

Kanisa ni Nyumba ya Mungu

Mara tunafikiri kuwa kanisa ni jengo la miti ama matofali ambamo watu wanakusanyikia ili wamuabudu Mungu. Bali Mungu yeze anatutazama sisi tulio mwaamini kuwa ni sisi ndio nyumba yake. Ana nafasi

ya Roho Mtakatifu wake ndani ya kila mmoja wetu, sisi ambao tulio kombolewa tunaitwa nyumba ya Mungu.

Soma kwa sauti: Waefeso 2:19-22 Mungu anakutazama wewe kama vile sehemu ya nyumba yake, iliyo jengwa juu ya Yesu.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 3:9-11

Kila mmoja wetu ni sehemu ya nyumba ya Mungu. Umuruhusu Mungu afanye kazi maishani mwako ili akujenge vizuri, uoneshe matendo ya Mungu. Tunasoma 1 Petro 2:5, “*Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazo kubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo.*”

Zabihu yetu ya kiroho ni nini?

Ya kwanza, kumuheshimu Yesu kwa yale anayo tuamuru tutende. Tunaweza kumpatia zabihu ya sifa na maabudu (Warumi 12:1-2). Tunaweza kutowa zabihu ya upendo kwa kuwatendea wengine mema, kwa kuomba, ama kwa kupeyana moyo sisi kwa sisi. Tunaweza kuchukua mda kujifunza njia za Mungu na kuwafundisha wengine.

Tunaweza kutowa zabihu za sadaka za shukurani, kwa kumshukuru Mungu kwa yale yote aliyo yafanya kwa ajili yetu. Mungu anafurahia aina hizi za zabihu ambazo zinazotoka katika mioyo ya upendo na moyo wa kumtumikia Yesu.

Soma kwa sauti: Waembrania 3:1-8

Yesu ndiye Bwana wa nyumba. Sisi ni nyumba ya Mungu na tuko chini ya uongozi wake na anatushugulikia pia. Tukumbuke kwamba watu wanatazama maisha yetu na kuchunguza ikiwa tabia zetu zinaonesha kwamba sisi ni wakristo wa kweli.

Kanisa ni Bibi Arusi wa Kristo

Soma kwa sauti: Waefeso 5:25-30

Yesu anaita kanisa kuwa ni bibi arusi wake. Yesu anapenda kanisa lake (wale waaminio) kama vile Bwana arusi anampendavyo bibi arusi. Hii ni picha ioneshayo upendo mkubwa wa kujitowa alio nao Yesu kwa ajili yetu. Yesu, Bwana arusi, alipenda bibi arusi (kanisa) na aliteswa na kufa msalabani kwa ajili yalo. Hii ingetufanya tuwe wenye shukurani kubwa na uaminifu kwa Bwana Arusi wetu aliye mbinguni.

Inawezekana uwe na matatizo katika ushirika na wengine hapa chini ya jua bali uelewe kwamba ushirika wako pamoja na Yesu, Mwokozi wako, unaweza kuwa mkubwa na ujaao upendo sana kama vile ule wa bibi arusi mpya anampenda mumewe.

Maandiko haya ya waefeso yanatuelezea kwamba Yesu anaosha bibi arusi (kanisa lake) na kumtayarisha kwa ajili ya arusi, ama muungano, ambao utakao kuja siku zijazo

Soma kwa sauti: Ufunuo 19:5-9

Kwa mda unao stahili Yesu atakuja na kuchukua bibi arusi wake, kanisa lake, hadi mbinguni ili kanisa lipate kuishi pamoja naye milele.

Kuungana na Kanisa la Mahali

Unapo mpokea Kristo, wewe tayari unageuka kuwa mwana memba ulimwenguni pote wa kanisa la Kristo. Ni vizuri sasa uchukuwe hatua ifuatayo ili uungane na kanisa la mahali unapo ishi.

Soma kwa sauti: Matendo 11:20-26

Makanisa katika Biblia yalipewa majina ya miji na vijiji ambamo wakristo waliishi ndani. Kila kikundi kilicho kusanyika ni sehemu ya kanisa kubwa ndani ya mji. Makanisa mawili yanatajwa katika andiko hili: kanisa la Yerusalem na kanisa la Antiokia.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 16:19

Hii ni salamu ilio andikwa kutoka kanisa la Azia lililo kuwa likikusanyikiya ndani ya nyumba.

Soma kwa sauti: Waebrania 10:24-25

Ni jambo la maana kushiriki kwa uaminifu katika kanisa lako la mahali. Unahitajika hapo kanisani, na wewe pia unahitaji yale ambayo wengine wanaweza kukusaidiya nayo hapo kanisani. Kuwa mwanamemba wa kanisa inatofautiyana sehemu moja na nyingine, bali kila mkristo ni mwanamemba wa kanisa la milele la Yesu. Mchungaji wako ama kiongozi wako atakupatia ushauri kuhusu namna unaweza kuungana na kanisa mahali unapo ishi.

Kazi ya Kanisa

1. Kazi ya kanisa ni kutangaza habari njema kuhusu Yesu kwa watu wanao wazunguka. Kila mwanamemba anapashwa kufanya kazi hiyo, si kazi pekee ya mchunjaji, mzee, muinjilisti ama shemasi.
2. Kazi ya kanisa ni kuwasaidia pia wengine wapate "kukomaa katika neema, na katika kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo"(2 Petro 3:18). Maana ya hii ni kujifunza pamoja na kupeana moyo mmoja na mwengine.
3. Kazi ya kanisa ni kuwasaidia wa maskini na wasiyo jiweza na hiyo inatendeka katika jina la Yesu.
4. Kazi ya kanisa ni kumsifu na kumuinua Yesu Kristo.

Soma kwa sauti: Wafilipi 1:9-11. Tunahitaji pia kumsifu Mungu kuititia jinsi tunavyo ishi, ili wengine waone hiyo na kumheshimu Mungu.


Somo kwa ufupi:

1. Kanisa linajengwa na watu walio okolewa na damu ya Yesu Kristo ilio mwangika.
2. Kanisa la Yesu Kristo si jengo lililo jengwa na mikono ya watu. Watu amba ni wa Yesu hao ndio nyumba ya Mungu.
3. Kila mkristo ni sehemu ya mwili wa Kristo na jamaa la Yesu Kristo kwa sababu tumenunuliwa na damu yake ya samani.
4. Kama vile watakatifu wa Mungu, sisi ni mawe yaliyo hai ya kanisa lake. Tunatowa zabihu za kiroho kwa Mungu kwa kuonesha upendo kwa

wengine, kwa kushuhudia imani yetu, na kwa kumsifu na kumuabudu Mungu.

Maswali:

1. Uligeuka kuwa sehemu ya kanisa la Kristo namna gani?
 2. Kwa nini ni jambo la maana kuelewa kwamba kanisa ni jamaa?
 3. Yesu alitununua (kutukombowa) na nini?
 4. Ikiwa sisi ni nyumba ya Mungu, na jamaa la Mungu, ni tabia gani ambazo tuna hitaji kuwa nazo katika jamaa zetu? Jamii yetu? Na ndani ya kanisa?
 5. Ni namna gani unavyoweza kutangaza injili (habari njema) inayo husu Yesu?
- (Mchungaji/Kiongozi,** Saidia kundi lako kujifunza njia tofauti ya kufanya hiyo.)



Vesi kwa uahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi lako kujifunza na kuweka kwa uahamu andiko hili na maneno yake:

Waebrania 10:24-25

“tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile inakaribia.”

Somo la 13

Mbele ya Uso wa Mungu

Katika somo hili tuta tazama namna Mungu ana tazama kila mtu na kumpatiya samani na tutatazama pia maana ya hiyo kwetu sisi wanawe wa kiume na wa kike.

Kila Mtu Aliumbwa kwa Mfano wa Mungu

Soma kwa sauti: Mwanzo 1: 26-28

Katika maandiko tunasoma kwamba watu waliumbwa na Mungu kwa sura na mfano Wake. Tuliumbwa ili tuwe na uhusiano mzuri pamoja na Mungu. Tumejifunza kwamba zambi ndizo zilivunja uhusiano wetu pamoja na Mungu na zikaharibu pia sura ya Mungu maishani mwetu. Bali tunapo geuka waamini, na kumukubali Yesu kama vile Bwana na Mwokozi wetu, kunaanzishwa mara tena urejesho ili tuwe na sura ya Mungu na mfano wake kama vile Mungu alivyo kuwa ana kusudia.

Kila Mmoja Wetu Ulimwenguni Ameumbwa kwa Njia ya Kimaajabu

Soma kwa sauti: Mwanzo 1:31 na Zaburi 139:13-15

Mungu alipotuumba, alisema, "*ni vizuri sana.*" Kila mtu aliumbwa na Mungu akiwa wa kipekee na akapewa zawadi ya uzima. Mungu alikujuwa wewe kabla hauja zaliwa, alikujua ulipokuwa katika tumbo la mama yako. Alikupenda na kuweka mpango mzuri kwa ajili ya maisha yako. Anataka akuone unabarikiwa, kwa jumlaa, na kuishi mpango alio andaa kwa ajili yako. Hii ndio sababu iliyotuma akuumbe ili umtendee yale aliyo kusudia utende hapa duniani.

Maandiko ya Mwanzo sura 1 na Zaburi 139 inaeleza kwamba watu wote, wewe na mimi, tunayo samani kubwa sana mbele za Mungu. Mungu anatutazama sote kuwa tunayo samani sawasawa na watu wengine wote waliyomo ulimwenguni. (hii inahusu pia hata mtu anaye kaa pamoja nawe leo hii.)

Mungu anakupenda wewe hata ukiwa mwanamume, mwanamuke, ama mtoto. Mungu hajali ikiwa wewe ni mweusi wala muzungu, ama rangi nyingine, tajiri ama maskini, mrefu ama mfupi, ikiwa una elimu ama hauna, hajali luga unayo isema. Mungu anakupenda wewe kama vile mtu aliye muumba, na ana kusamini sawasawa na watu wengine wote. Watu wamejibagua na wengine, bali Mungu anataka sisi tuishi kwa amani pamoja na wengine, na kuishi pia katika ushirika ulio mzuri na maelewano sisi kwa sisi.

Soma kwa sauti: Warumi 12:10 na Warumi 13:8

Alika kundi lako kuzungumza kuhusu maswali haya:

1. Ni namna gani tunaweza kuonesha upendo wa Kristo kwa mtu aishiye pamoja nasi katika jamii, mtu ambaye anatihitaji kumpokeya Kristo?
2. Utaonesha namna gani upendo wa Kristo kwa mtu aingiyaye kanisani pamoja na wewe?

Kwa sababu Kristo anaishi ndani yetu tunao uwezo wa kushinda zambi katika maisha yetu. Tunao pia uwezo wa kuwapenda watu ambao wanao tupililiwa na kuchukiliwa. Hii inaweza kufanyika kuitia nguvu za Roho wa Mungu pekee aliye ndani yetu.

Mungu aliumba mwanadamu (wanaume na wanawake) ki maajabu na kumpatia kila mmoja vipawa. Tuna vipawa kiakili, kiutashi, pia kihisia. Tunavyo vipaji vya kuanzisha vitu vipyta, vipaji vya kufikiri, na nguvu za kihisia. Ni kwa njia ya kutumia vipawa hivi ndiyo Mungu anataka tuvitumie ili tubadilishe ulimwengu wetu iwe nafasi nzuri kwa kuishi.

Kutazama Kupitia Macho ya Mungu!

Tukijifunza kuangaliana sisi kwa sisi na samani kama vile Mungu anavyo tutazama, tutaanza kuona mabadiliko ya kweli katika maisha yetu, katika maisha ya jamaa zetu, jamii yetu na hata maisha ya inchi nzima.

Mtu mmoja aliuliza: ‘Amri kubwa katika sheria za Mungu ni gani?’ Yesu akajibu akisema: “*Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa Raho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika hizi amri mbili hutegemea torati na manabii*” (Matayo 22:37-40).

Yesu alikuwa akisema kwamba kuonesha upendo (katika yale tuyasemayo, tunayo yafikiri na kutenda) kwa ajili ya Mungu na wale watuzungukao ni jambo la muhimu sana katika maisha yetu.

Watu wote waishio duniani na wale waishio katika jamii zetu waliumbwa na Mungu. Pasipo kujali kabilia ya mtu yeote hata akiwa anatoka Burundi, Rwanda, Tanzania, Uganda, Kenya, Sudan, Zambia ama Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo,... hata mtu awe ametoka mbali zaidi; hata akiwa mweusi ama mzungu, ama muarabu; watu waishio vijijini wakifanya kazi mashambani ama za ufugo, wale wanaoishi ndani ya miji na vijiji; hata madaktari, watumishi wa serekali, wale wafanyao kazi jeshini na polisi, wafanyao biashara ama wale wafanyao huduma manyumbani; watu wanaoishi ndani ya manyumba na wale wasiokuwa na nyumba walalao inje na mabarabarani, watoto wa barabarani, wanafunzi, walio na afya na wagonjwa; watu hawa wote waliumbwa na Mungu, na wanapendwa naye pia. Mungu anawatazama wote kuwa na samani moja ama wote sawa sawa mbele zake. Hakuna mtu kati ya hawa wote aliye na samani zaidi kuliko mwengine mbele ya uso wa Mungu, kwa kuwa wote waliumbwa kwa mfano na sura ya Mungu.

Kwa ajili ya hiyo tuwatazame wengine jinsi Mungu anavyo watazama, tuwatendee mambo kufuatana na yale ambayo Biblia inavyo tuamuru: kuwapenda, kuwaheshimu, na kuwasikilia huruma, pia kuwasaidia wanapokuwa katika shida.

Soma kwa sauti: Marko 5:38-48

Yesu alikuja kuwatafuta na kuokowa watu wa dunia hii ambao wameshikwa na mitego ya zambi na kutengwa na Mungu. Yesu hakuja ili ashangiliwe ama kutafuta faida za kipekee. Jaribu kufikiria jinsi sisi wakristo tanahitaji kuwatazama wengine na kuwatendea.

Soma kwa sauti: Marko 10:42-45

Yesu alituokowa kwa kuja ulimwenguni na kuleta uponyaji na ukweli, msaada na upendo. Baada ya hiyo Yesu alituokowa kupitia kufa kwake msalabani, na kulipa garama ya zambi zetu. Hapo kalvari Yesu alilipa garama ya mwisho na alionesha upendo mkubwa kwa ajili yako wewe na mimi.

Kwa njia ile ile, wewe na mimi tutafute kuishi maisha yaoneshayo upendo wa Mungu na kusamini kila mtu atuzungukaye, watu wote kwa jumla wazuri na wale ambao wamechukiliwa na kutupiliwa. Si vizuri kuwa watakatifu siku ya Mungu asubui pekee ama wakati tunakusanyika na wakristo wengine, na siku zingine tusiwe watakatifu. Tunahitaji kuonyesha upendo wa Mungu kwa kila mmoja siku baada ya siku, kwa kila mtu, na katika hali zote.

Soma kwa sauti: Wafilipi 2:3-4

Kupeana samani mmoja kwa mwengine maana yake ni kutanguliza mahitaji ya mtu mwengine mbele ya mahitaji ulio nayo, kama jinsi Kristo alivyofanya. Ikiwa tunawapenda na kuwasamini watu wengine, ujeuri na mapigano na vita kati ya watu yatapunguka kwa ngazi ya juu. Amani itatiririka na watu wataishi vizuri na kwa furaha.

Mungu ana Samini Watu Wote, Sote ni Sawa Sawa

Tusome Biblia na kuangalia jinsi Mungu anavyo watazama watu tofauti:

Wanaume na Wanawake:

Soma kwa sauti: Yohana 4:7-29

Wayahudi waliwachukia Wasamaria na kwao mwanamke hakuwa na samani yoyote. Yesu alitembea kinyuma ya desturi hiyo na kinyuma ya imani za kiyahudi akafundisha upendo kwa Wasamaria.

Soma kwa sauti: Marko 15:42-47

Yesu aliwaweka pia wanawake kati ya wanafunzi wake. Yesu anawapa wanaume na wanawake samani moja.

Watoto:

Soma kwa sauti: Matayo 19:13-15

Yesu aliwasamini watoto kama vile alivyo samini watu wakubwa.

Rangi zote za watu, kabilia, watu wote:

Soma kwa sauti: Warumi 1:16-17

Mungu anaonesha kwamba watu wote ni sawa wayahudi, mataifa, wote ni sawa sawa mbele ya Mungu. Yesu anawapenda watu wote na alikufa kwa ajili ya kila mmoja wetu. Kile Mungu anacho patia samani zaidi ni imani yetu tulio nayo katika Kristo.

Ngazi mbalimbali:

Soma kwa sauti: Wagalatia 3:28

Kusiwe mtu ambaye atakaye jitazama kuwa yeye yuko juu zaidi ama chini zaidi ya mtu mwengine, ama kumzarau jirani yake. Wanaume na wanawake wote wamekubaliwa kama vile watumishi wa Mungu.

Somo kwa ufupi

Mungu alimuumba mwanadamu, mwanaume na mwanamke, kwa mfano na sura yake; kila mmoja ana samani kubwa pasipo kujali ngazi anayo ama mahali anapotokea. Kama vile watu wa Mungu tunahitaji kuwatazama wengine namna ambayo Mungu anawatazama.

Yesu alikuja ili arejeshe uhusiano kati ya mtu pamoja na Mungu. Yesu alilipa garama yote, akatowa maisha yake kwa sababu ya upendo wa Mungu kwa ajili ya watu wote. Kwa ajili ya hiyo sote tunamurishwa na Biblia kuwapenda wengine kama vile Yesu alivyo tupenda. Tunahitaji kuweka pembedi utofauti na ubaguzi ulio kati yetu, tukiweka matengano kati yetu pembedi, na kupendane sisi kwa sisi ili tuishi kwa upendo, uvumilivu, na maelewano kila mmoja pamoja na mwengine.

Maswali:

1. Kwa nini unafikiri kuwa Mungu ana patiya watu samani kubwa? (Tumeumbwa kwa mfano na sura yake. Mungu anatupenda kwa upendo usiokuwa na mwisho na anatupatia samani.

Soma kwa sauti: Yeremia 31:3).

2. Soma kwa sauti: Matayo 6:14

Tunaweza kufanya nini kwa ajili ya wale amba wanatutesa?

3. Soma kwa sauti: Wagalatia 5:14

Fikiri na ushirikishe wengine namna gani andiko hili linaweza kuwekwa katika vitendo.

4. Soma kwa sauti: Matayo 20:28

Mungu Mwenyewe (Yesu Kristo) alioneshaa aina ya upendo huu kwa ajili yako na kwa ajili yangu. Sisi kama vile wakristo ni namna gani tunaweza kuonyesha upendo wa namna hii kwa wengine?

5. Uombe kila mmoja afunge macho na kufikiri kuhusu andiko hili ukiwa unalisoma: 1Timoteo 2:1- 6.

Mchungaji/Kiongozi sema maneno yafuatayo: “Jaribu kufikiri kuhusu mtu ambaye uliwaza vibaya kwa ajili yake, ama umemtendea mabaya katika jamii yako; uombe Mungu akusamehe; umuombeye huyo mtu sasa hivi.”

Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi kuweka kwa ufahamu andiko hili:

Wagalatia 3:28

“*Hapana Myahudi ama Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mme wala mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu.*”

Somo la 14

Msamaha

Katika somo hili tutazame yale Biblia ifundishayo kuhusu msamaha. Kusamehe maana yake kumuacha mtu huru asilipe deni, ahadi aliyo ahidi, ama mapashwa anayo stahili kufanya kwa ajili yetu. Inahusu pia kuondoa uchungu ama hukumu inayo kuwa kwa ajili ya mtu huyo.

Tunapo fikiri kuhusu tendo la kuacha mtu huru tunaweza kufikiria, mfano, ndege ilio shikwa kwenye mtego; unaiondoa mtegoni na kuiacha huru ili iruke mara tena. Ndege hiyo inaondoka na kuruka pasipo kikwazo chochote, ikiwa huru, ikiwa na shukurani kwa kuondolewa mtegoni. Ama tunaweza kufikiria kuhusu mfugwa gerezani ambaye amewekwa huru, anaondolewa gerezani na kuondolewa mashitaka yote aliyokuwa nayo; ama kuondoa vikaratasi vyote nya mashitaka kwa ajili yake.

Kwa uchungu, miyo yetu inaweza kufananishwa kama vile magereza ambamo mmejaa chuki, hasira, kinyongo na uchungu kwa sababu ya watu wengine kuhusu mabaya ambayo walisema ama waliyo tenda kwa ajili yetu. Tunasikia kuumizwa na kusikia hasira nyingi sana na kwa mwisho tunafikia kuwa na uchungu siku baada ya siku, wiki baada ya wiki, mwaka baada ya mwaka, tukijisikia kuwa hatuwezi kuwasamehe walio tukosea ama kuwaacha huru wengine na kuondoa hasira tulio nayo kwa ajili yao. Tunapo endelea kuhesabu makosa waliyo tutendea, tunajenga ndani mwetu uchungu, kinyongo na chuki kwa ajili ya watu wengine. Tunapoishi namna hii tunageuza miyo yetu kama vile magereza zinazo jaa na hasira inayoweza kuripuka kwa sababu ya kutokusamehe.

Kuendelea kuweka uchungu na hasira namna hii inaweza kuleta msukumo wa kuwatendea mabaya wale walitukoseya. Mawazo yetu yanaweza kuripuka kwa sababu ya chuki na kutuelekeza kwa vitendo nya machukizo, jeuri, kulipiza kissasi; na kwa njia hiyo tunaweza kuwaharibu watu wengine. Ndio sababu tunahitaji kuondoa moyo wa kuto kusamehe ndani yetu.

Kusikia uchungu, hasira, na chuki kwa ajili ya wale walio tukosea vyaweza kujaa siku baada ya siku na vyaweza kazaa na kuzidisha matatizo kiafya ndani ya miili yetu. Watu wamoja kati yetu wanawea kupata maumivu ya kichwa, matatizo ya moyo, damu kutembea haraka, kukosa usingisi, mchoko, woga, na matatizo mengine. Pahali pa kulala kwa amani usiku ili wawe na nguvu za kufanya kazi siku ifuatayo, wanapoteza ma saa mengi ya kulala na kufikiria makosa ambayo wengine wametutendea.

Hali ya kusikia uchungu moyoni inaleta pia kuvunjika kwa ushirika kati ya watu wa jamaa na jamii yote pia

Yesu anatufundisha nini kuhusu kusamehe?

Kama vile wakristo, ni jambo la maana sana kuelewa maana ya msamaha wa kweli, kama vile Yesu alivyo fundisha katika Biblia.

Soma kwa sauti: Luka 23: 32-39

Wakati aliposhikwa na maaskari, Yesu alitukaniwa, alichekelewa, alipigwa na kukogotewa na kuvikwa taji ya miiba kichwani. Baadaye, maaskari wakamubamba msalabani kwa kutumia misumari. Yesu akachagua kuwasamehe wale walio msulubisha na wale walio mchekelea.

Hata wakati alipokuwa msalabani alimuomba Baba yake kuwasamehe wale walio mtendea mabaya. Aliwaombea msamaha wale amba walio kataa kumuamini na wale walio chagua kumtendea mabaya makubwa ya namna hii.

Soma kwa sauti: Matayo 18:21-22; na Marko 11:25-26

Mchungaji/Kiongozi, uliza: “*Yesu anatufundisha nini katika maandiko hayo?*”

Mungu anatowa msamaha wake ulio kamili kwa kila mmoja tunapotubu na kumuomba atusamahe. Hatustahili kupokea msamaha wa Mungu ijapo hiyo yeye anatusamehe tukiweka imani yetu ndani ya Kristo. Ikiwa tutahitaji kuishi kwa furaha na kutosheka maishani, tutahitaji kuwasamehe wale walio tukosea. Ikiwa tutahitaji kuwa na amani maishani na katika jamii zetu tutahitaji kuchagua kusamehe walio tukosea. Mungu pekee ndiye anaweza kutusaidia kusamehe.

Msamaha wa Kibiblia

Ni jambo la maana sana tuelewe maana ya kusamehe. Msamaha una sehemu mbili tofauti ziunganazo pamoja; ya kwanza ni kupokea msamaha na ya pili ni kutoa msamaha.

Sehemu ya kwanza ya msamaha: Sehemu ya kupokea

Soma: Luka 7:48 na Matendo 10:43

Tunapokea msamaha wa Mungu tunapoenda kwake na kutubu, na kuacha njia zetu za zambi. Tunapokea msamaha wa Mungu pasipo kulipa chochote, bali tuelewe kwamba Yesu alilipa garama kubwa sana kwa ajili ya zambi zetu. Biblia inasema kwamba zambi zetu zimeondolewa na kutupiwa mbali sana kama vile mashariki inatengana na magaribi (Zaburi 103:12). Tuna pokea msamaha wa Mungu kuitia imani kwa njia ya kusulubishwa kwa Yesu, Mungu hata kumbuka zambi zetu mara tena.

Ni huzuni sana, kuona kuna wakristo wengi amba wanaendelea kujisikia vibaya na kuwa na hatia hata baada ya kusamehewa na Mungu maishani mwao. Tunahitaji kuelewa kwamba neema ya Mungu tumepewa kwa jumla; Yesu alilipa garama yote ya zambi zetu hapo Kalvari. Tujisikie huru kwa jumla kwa sababu tumesamehawa na Mungu.

Soma kwa sauti: Waefeso 1:7 na Wakolosai 2:13

Yesu alipokusamehe, makosa yako yakavutiwa kabisa. Maana ya msemwa huo ni kusema hauhesabiwi kuwa na zambi tena; ni kama vile zambi zako zimetupwa mbali kama vile mashariki inatengana na magaribi. Baada ya Yesu kukusamehe, Mungu hawesi kumbuka zambi zako tena. Uliposamehewa, Yesu alikuweka huru na kukuondolea azabu yote ya zambi, ambayo ulistahili kuipata.

Soma kwa sauti: Yohana 8:36

Mchungaji/Kiongozi, uliza: Jee, umekubali msamaha amba Yesu amekutolea?

Yesu alikuja kuweka huru ulimwengu ambaa umetekwa na hatia ya zambi. Msalabani Yesu alilipa garama yote ya zambi. Kuitia imani katika Kristo na kujitoa kwake tumetolewa msamaha unaotolewa kwetu na Baba wa mbinguni.

Kuendelea kujisikia hatia inatokana na yule mwovu. Baada ya Mungu kutusamehe makosa yote tuliyo yafanya, tunasamehewa kwa jumla, mbele ya Mungu tunakuwa huru pasipo shutuma yoyote. Tunaweza kukaa kwa amani tukiwa na uhakika kwamba tumesamehewa na Mungu.

Vivyo hivyo, kama tumesamehewa na mtu mwengine kwa ajili ya kitu tulicho kifanya, hatupashwi kuendelea kuishi katika kujilaumu ama kuendelea kwa kusikia hatia miyoni mwetu tena. Tunahitaji kupokea msamaha ambao tumepewa na mtu mwengine, na kumshukuru Mungu kwa ajili ya msamaha huo.

Soma kwa sauti maandiko yafuatayo. Omba kundi lako kurudiliya maneno yaliyomo. Uwaalike wapokeye ukweli huo katika maisha yao:

1 Yohana 1:9 “*Tukiziungama zambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.*”

Warumi 8:1 “*Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhazu juu yao walio katika Kristo Yesu*”.

Sehemu ya Pili ya Msamaha: Sehemu Itowayo Msamaha

(Mchungaji/Kiongozi: Soma andiko hili ni ndefu zaidi kwa watu wako)
Luke 15:11-24 (Hadisi hii ni ya mwana mpotevu)

Jaribu kufikiri kwamba katika hadisi hii wewe ndiwe Baba. Jee, ungelimusamehe mtoto huyu kwa matendo ya ujingga aliyoyatenda kama vile alivyo msamehe Baba huyu katika hadisi hii? Jaribu kufikiria mda na nguvu wewe baba uliyo tumia ili upate utajiri huu, baadaye mtoto wako kwa njia ya upumbafu anamaliza utajiri huo wote kwa mda mfupi. Kwa ukzeli; wengi wetu wanaweza kushindwa kutoa msamaha wa kweli.

Katika hadisi hii, Yesu aelezayo tutatambua kwamba Baba huyu si baba wa ulimwenguni kabisa, bali ni Baba Mungu mwenyewe. Baba aliye katika hadisi hii yuko tofauti kabisa na wa baba wa ulimwengu na katika hadisi hii tunaona kwamba Mungu ni mwenye kujaa huruma. Mungu anataka sisi tumurudiliye; anatungojea na yuko tayari kutusamehe. Mungu asamahe mtu kwa jumla hajali wingi wa zambi zake. Anawasamehe watu pasipo kuhesabu wingi ama uzito wa zambi walizo zitenda.

Yesu anatufundisha kwamba sisi kama vile wakristo tuige mfano wa kuonesha rehema na msamaha kwa wengine kama mfano huo, pasipo kuhesabu wingi wa uzito ya makosa walio tutendea.

Kwa Nini Napashwa Kusamehe?

Soma kwa sauti: Waefeso 4:32

Mungu anatuamuru kusameheyana sisi kwa sisi. Mahali pote kunapokuwa watu wanao kaa pamoja, kutafika mda ambapo mtu anaweza kumkosea mwengine. Hata katika kanisa, na sehemu zingine pia. Kitakacho tusaidia kuishi katika umoja na kuelewana ni kutii maagizo ya Mungu. Inawezekana na tunapashwa kusameheyana sisi kwa sisi.

Soma kwa sauti: Matayo 18:21-35

Yesu alitoa hadisi hii, ili atusaidie kuelewa kwamba tunapashwa kuwasamehe wengine kama vile alivyo tusamehe sisi. Yesu alilipa garama ya kila toni ya damu yake ili tupate kusamehewa. Tulikuwa na deni kubwa sana ambayo hatukuwa na uwezo wa kuilipa, bali Yesu alilipa garama hiyo

ili tupate kusamehewa. Vivyo hivyo anataka sisi tuwasamehe wale walio tukosea.

Msamaha ambao Yesu anao tutoleya ni mkubwa zaidi kuliko huo ambao anatuomba tuwatoleye wengine. Hatusemi hapa kama vidonda tulivyo navyo moyoni havituzuru; bali tunasema kwamba tunapashwa kuwasamehe walio tukosea kama vile Yesu alivyo tusamehe sisi.

Kama vile mtumishi katika hadisi hii, Bwana wetu anatarajia sisi kuwasamehe na kuwaacha huru wale walio tukosea. Ikiwa tuna chagua kutokusamehe, tutapata tutahukuwa na Mungu, aliye wa milele na mwamuzi wa haki kwa watu wote.

Kusaidia Kutatuwa Mizozo

Soma kwa sauti: Matayo 18:15-20

Maandiko haya yanatuunesha kwamba ni jambo la maana sana kutenda kazi kwa bidii ili tujaribu kutatua mizozo inayo kuwa kati ya wakristo waishio na kufanya kazi pamoja. Tunahitaji kurudisha maelewano kwa haraka mahali panapokuwa kutokuelewana. Mara, inakuwa vigumu kusamehe ikiwa tumejisikia kutendewa vibaya ama kuumizwa na yale yaliyo semewa ama yaliyo tendewa kwa ajili yatu. Kama vile wakristo ni vizuri kufuata maagizo ya Mungu na kusameheyana sisi kwa sisi pasipo kuhesabu ukubwa wa mabaya yaliyo tendewa kwa ajili yetu.

Pasipo kuwasamehe wale walio tukosea hatuwezi kuwa na amani katika maisha yetu ya kipekee, katika kanisa, ama katika jamii. Kama vile wana wa Mungu, tunahitaji tuwe na maisha ya kusameheyana katika maisha ya kila siku.

Wakolosai 3:12-14 inasema "*Basi kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyeketu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheyana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumia mwenzake; kama Bwana alivyo samehe ninyi, vivyo nanyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu.*"

Ikiwa kuna tatizo ambalo limetushinda kutatuwa wenyewe, tunahitaji kuwatafuta wakristo wengine walio na hekima nyingi kuliko sisi ili watusaidie kupata suluhisho. Ni vizuri kuwaona viongozi wa kanisa na watajaribu kusaidia kupata suluhisho kwa shida mlizo nazo. Biblia inatuelezea pia kwamba, ni vizuri kujaribu kuleta suluhisho kwa matatizo yanayo watenganisha wanamemba katika kanisa, pahali pa kushitakiyana kwenye mahakama, serekali ama kwa wasio amini (1Wakorinto 6:1-10).

Namna ya Kuwasamehe Wengine

- Jaribu kuanza kufikiria kuhusu watu walio kukosea kwa njia moja ama nyingine.
- Ukiwa katika hali ya maombi umuombe Mungu akusaidie ili upate moyo na neema ya kuwasamehe.
- Tangaza kwa sauti msamaha huo kwa watu wale. Sema, "*Nina samehe (taja majina) kwa yale waliyo yatenda.*"
- Ikiwa inahitajika, jaribu kufikiri kama vile unawaweka huru. Ukisema, "*Nina waweka huru, kwa Jina la Yesu.*"
- Umuombe Mungu akupatiye amani yake katika moyo wako.

Biblia inatufundisha kama vile wakristo tunapashwa kuwasamehe wale walio tukosea. Biblia haisemi kwamba, kwa sababu hiki ndicho kitendo chepesi kufanya, ama kwa sababu sisi ni watu walio na damu na nyama hatuwezi kusamehe. Wafilipi 4:13 inasema: “*Nayaweza mambo yote katika yeye (Kristo) anitiaye nguvu.*” Ni kwa nguvu za Mungu pekee ndizo zaweza kutusaidia kusamehe kwa kweli.

Msamaha si Kitu Gani

Msamaha wa ukweli kibiblia si kusahau yale waliyo tendeka, ama kujifanya kama vile hatukuumizwa ama kukwazika na yale waliyo tutendea. Si kwa njia ya kuzuwigia hisia ama kuzificha. Ikiwa tunafanya hivyo, kisha mda mfupi ama mrefu hisia hizo tulizo zizuwia na kuzificha zitarudi na kuonekana wala hazita fichama tena.

Msamaha siyo hisia. Msamaha wa kweli ni chaguo na uamzi tuufanyao; ni tendo la utashi. Ni kusema, “*hata ikiwa nimekosewa na kuumizwa kuhusu yale niliyotendewa, nina chagua kusamehe. Mbele ya Mungu na kwa jina la Yesu ninachagua kuondoa hasira yangu, kujisikia vibaya moyoni na maumivu. Nina amua kuwasamehe wale walio nikosea.*” Ikiwa unaendelea kujaza akili zako na moyo wako na maneno kama haya, utaanza kuwa na amani ya Mungu katika maisha yako.

Ikiwa unaendelea kusikia sauti ya makosa walio kutendea yanarudi katika akili zako, unaweza kukemea sauti hiyo kwa jina la Yesu kwa kusema “*Nina samehe. Nina weka huru watu hawa.*” Hii ndio Yesu alifanya msalabani kwa ajili yako. Hii itakusaidia kujaza akili zako na maandiko ya Biblia, ama umuimbie Yesu nyimbo. Hii itakusaidia kujaza akili zako na mambo mazuri ya Mungu.

Msamaha SIYO ya WAZAIFU

Wazaifu mara nyingi wanachomwa sana na uchungu na hasira na kushindwa hata kusamehe wengine. Ili mtu asamehe inamubidi achukuwe tendo la ushujaa; inambidi mtu huyu awe mwenye nguvu na mwenye neema ya Mungu ili amsamehe mtu mwengine. Kumbuka kwamba msamaha siyo hisia; ni uamzi tunao uchukua kwa kumtii Bwana Yesu Kristo.

Ikiwa unasikia hasira na kuumizwa, unahitaji tena kurudilia maneno haya, “*Nina samehe. Nina weka watu hawa huru.*” Kila mara ufanyapo hivyo hisia zako zita anza kutawaliwa na mamlaka ya Mungu. Jinsi mda unavyoendelea hisia hizo za hasira na uchungu zitakwisha. Kumbuka kwamba hiyo inaweza kutendeka kwa nguvu za Yesu Kristo pekee aishiyе ndani yako. Hauwezi kufanya hiyo kwa uwezo wako mwenyewe.

Lakini, ikiwa unaendelea kufikiri kuhusu yale yaliyo semewa ama yaliyo tendeka kwa ajili yako, utaanza kuishi hali hiyo mbaya, na kujikuta katika hali ya kuto kusamehe. Kutubu, kusamehe, na kuweka huru! Hii ndiyo njia itakayo kusaidia kuishi uhuru wa kweli.

Maswali:

Soma kwa sauti: Matayo 18:23-35

Muzungumze pamoja kuhusu maulizo yafuatayo:

1. Yesu anafundisha nini katika hadisi hii?
2. Ni deni ngapi (zambi na makosa uliyo tenda) Mungu amekusamehe?
3. Jee, unaweza kufikiria kuhusu watu waliyo kukoseya kwa njia moja ama nyingine, ama kuhusu mtu ambaye una uchungu kwa ajili yake? Ni tendo gani unahitaji kutenda kwa sasa?
4. Jee, kuna mtu ambaye unahitaji kumuomba msamaha, mtu ambaye umemkosea kwa njia fulani? Ni tendo gani unahitaji kufanya?
5. Ni wapi tunaweza kupata nguvu za kuwa samehe wengine?

Soma kwa sauti: Wafilipi 4:13 na Matayo 11: 28-30

Pastor/Kiongozi: Uwaongoze watu katika mda wa maombi ili wamuombe Mungu msamaha kwa zambi ambazo hawaja tubu. Uwape watu moyo ili wawasamehe wale walio wakosea na uwape moyo pia kuomba masamaha kwa wale ambao wamekosea.



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi lako kujifunza kwa ufahamu na kuweka vesi moja ama yote mbili:

1 Yohana 1:9

“Tukiziungama zambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote.”

Waefeso 4:32

“Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyo wasamehe ninyi.”

Somo la 15

Ushindi na Uhakika Katika Kristo

Shabaa ya soma hili ni kukusaidia kujua mitego na ujanja ambao adui wetu, Shetani, atumiyao ili aharibu imani yetu. Somo hili litakusaidia kuishi na uhakika utakao kusaidia kushinda mashambulizi ya aina yoyote itokanayo na adui, ili umushinde katika Kristo.

Katika Biblia, Shetani anaitwa "muongo", "adui", "Belzebul", "Nyoka", "Joka", "Ibilisi".

Shetani Alitoka Wapi?

Shetani na malaika wengine wamtumikiao Mungu wote waliumbwa na Mungu, lakini Shetani akaanza uasi huko mbinguni hiyo ikasababisha Mungu amtupe hapa duniani. Yesu anashuhudia hiyo akisema "*Nilimuona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme*". (Luka 10:18)

Shetani alitupwa kutoka mbinguni kwa sababu alitaka kujinua akisema, "Nitajifanya mwenyere kama aliye juu" (kama vile Mungu). Shetani anataka kuongoza ulimwengu tunamo ishi na kuweka ndani mipango yake mibaya.

Mbinu za Shetani

Shetani anataka kuongoza ulimwengu tunamo ishi akiujaza na mipango yake mibaya. Mpango wake ni kuendelea kuinga kusudi la Mungu. Shetani hachoki kutafuta kuharibu, na kobomoa maisha ya watu kwa kuwashambulia, na kushambulia kazi ya Bwana Yesu Kristo pia. Kama vile adui wetu anatafuta kutuharibu na kuapeleka wengi katika zambi na hukumu ya Jehenamu akiwadanganya wengi na kuwatia woga, kama vile alivyofanya kwa Adamu na Eva.

Soma kwa sauti: 1 Petro 5:8

Shetani si muweza yote kama vile Mungu. Shetani hayuko kila mahali kwa mda mmoja, kwa sababu yeye si Mungu. Shetani ana mipaka katika nguvu na ujuzi wake. Hawezi kujua kile ambacho tunacho fikiria wala hawezi kuwa zaidi ya nafasi moja kwa saa moja, bali Mungu yeye anaweza. Kwa sababu ya hiyo, hatupashwi kumuogopa shetani tena tukifikiri kwamba yuko kila nafasi kwa mda wote akitutazama na kujua yale tunayo yafikiria ama kutenda, Shetani hawezi kamwe kujua yale ambayo tunayo yafikiria bali Mungu yeye anaweza kila mara.

Kwa sababu Shetani ana mipaka katika uwezo wake, anaweza kufanya tuu yale ambayo ameruhusiwa na Mungu. Wakati wowote Shetani atendapo kitu kibaya kwa ajili yetu tusiogope, kwa kuwa Mungu ametupatia uwezo wa kumshinda.

Jinsi Shetani Anavyo Tushambulia

Shetani anatumia njia zifuatazo kwa kutushambulia:

1. Majaribu – Shetani anatujaribu tutende zambi kama vile alivyo mjaribu Yesu. **Soma kwa sauti: Matayo 4: 1-11**

2. Ujanja na uongo – Shetani ni muongo na anatumia ujanja ili atudanganye kama vile alivyo wadanganya Adamu na Eva.

Soma kwa sauti: Mwanzo 3:1-7

3. Mashitaka – Shetani anatushitaki mbele za Mungu. Soma kwa sauti: Zakaria 3:1-4

Hata wewe pia Shetani atakushitaki! Atakuelezeya mambo mabaya yote ya kale uliyo yatenda, ili akuondowe katika mapenzi ya Mungu. Shetani anataka usikiye hatia na haya ili upate kujisikia mwenyewe kama wewe ni wa ovyo mbele za Mungu, ijapohiyo, hiyo yote ni uongo. Jibu lako kwake ni kumuelezza kwamba zambi zako zimesamehewa na Yesu amekuosha na damu yake.

Soma kwa sauti: Wakolosai 1:12-14

Yesu alikupatia maisha mapya. Maisha yako ya kale yamepita tayari.

Soma kwa sauti: 2 Wakorinto 5:17.

4. Mateso – Shetani anatafuta kutusumbua na mateso kimwili na magonjwa kiakili, hata magonjwa na kusumbua watu kupitia shida ambazo kwa sasa zipo tayari duniani.

Soma kwa sauti: Matayo 12:22 na Matayo 17:18

5. Upinzani – Shetani na mapepo wachafu wake wanapingana na Mungu na watakatifu wake.

Soma: Ufunuo 12:17

Shetani, Joka, wanapigana na watu wa Mungu.

Soma kwa sauti: Waefeso 6:10-18

Adui wetu atushambulia, sisi tunao amini na sisi tunamupinga kwa njia ya maombi. Tumupingapo adui wetu kwa jina la Yesu, tunamushinda!

6. Kifo – Hii ilikuwa silaha ya nguvu ya Shetani hapo kale, bali Yesu aliondowa hiyo alipofufuka kati ya wafu.

Soma kwa sauti: Waebmania 2:14-15

Mitego ya Shetani

Biblia inatuonesha kwamba kuna njia tatu ambazo Shetani atumiyazo kwa kuwadanganya watu ili watende zambi. Ikiwa tutajua mitego ambayo aiwekayo, hiyo itatusaidia kama vile watu wa Mungu tujuwe mitego hiyo na jinsi tunavyoweza kuiepuka.

Mitego wa kwanza – Tamaa ya macho: Tunahitaji kuwa waangalifu kuhusu vitu tunavyo vitazama na kuvitamani maishani mwetu. Katika amri kumi za Mungu, Mungu anatuomba kufanya angalisho kuhusu tamaa ya vitu vya ulimwengu (maana ya tamaa ni kuwa na msukumo wa zaidi wa kutaka kuwa na kitu fulani, ama kufanya tendo fulani).

Soma kwa sauti: 1Timoteo 6:9-12 na 1 Yohana 2:14-17

Ni vizuri kutaka kuboresha maisha yetu ya hapa duniani na kuboresha pia namna ya kuishi kupitia kufanya kazi kwa bidii, tukifanya uwekezaji, kupitia faida iliyo ya haki. Lakini, tunahitaji kuwa waangalifu ili tusiingie katika majaribu ya Shetani ambaye atakaye tujaribu tutende mambo ya aina hii kwa ajili ya shabaa ya maisha yetu pekee. Shabaa yetu kubwa inapashwa kuwa kumuabudu Mungu na kuishi maisha ya utakatifu tukiwa na ushirika mzuri pamoja na Mungu.

Mitego wa pili – Tamaa ya mwili: Miili yetu yahitaji aina ya vitu fulani vilivyo vya msingi kwa maisha ya binadamu mfano: chakula, maji, mavazi, na nafasi ya kulala. Bali tunahitaji kuwa waangalifu kuhusu mambo mamoa

mamoja ambayo miili yetu na moyo wetu waweza kutamani, kwa kuwa tamaa ya kitu yaweza kutuangusha katika jaribu la Shetani. Ni vizuri tuepuke jaribu la pombe, madawa ya kulevya, uasherati na matendo yoyote yale ambayo yanaweza kutupeleka kutenda zambi ama kuwa watumwa wa kitu kile.

Tendo la ndoa ni kwa wale pekee ambao wameowana. Hiyo ndio shabaa na kusudi ya kuumbwa kwa viungo vya uzazi. Kuwa na tamaa kinyume cha ushirika wa aina hii kunahukumiwa na Mungu.

Soma kwa sauti:1 Watesalonike 4:3-8;1 Petro 2:9-12;Wagalatia 5:16-24

Mtego wa tatu –Tamaa ya mamlaka ama vyeo: Tamaa ya mamlaka inawatesa watu wengi ulimwenguni leo. Watu wako tayari kutenda ubaya wa aina yoyote ili wapate mamlaka, kuwa wasimamizi wa wengine, na kupata heshima. Tamaa ya mamlaka na vyeo hupeleka wengi katika umwangaji wa damu, vita katika inchii, vurugu ndani ya jamii, na hata ndani ya jamaa. Kutaka utawala inaweza kuwapeleka watu katika mafarakano, mabishano, hata vita ndani ya kanisa la Mungu na inchini.

Soma kwa sauti: Yakobo 4:1-4

Soma kwa sauti: Yakobo 1:12-17

Katika maandiko haya tunasoma kwamba Mungu hawezi kumujaribu mtu; lakini tunajaribiwa wakati tunapo jitowa kufikiri kuhusu majaribu na kuanza kutamani majaribu hayo, tunaanza kuyapenda, na kuchukua mda mrefu kuyafikiria. Tamaa mbaya iliyo ndani yetu (msukumo huo wa nguvu za kutamani) unatupeleka kukubali kujaribiwa wakati Shetani ajapo na majaribu yake. Ikiwa tamaa zetu zatawaliwa na Yesu, hatuwezi kuanguka katika jaribu. Bali tutalishinda jaribu kwa jina la Yesu.

Yakobo anatuelezea kwamba msukumo wa zaidi ulio ndani yetu utatupeleka katika majaribu na majaribu yatatusukuma kutenda zambi. Zambi zaleta utengano kati yetu na Mungu.

Zambi zajenga ukuta wa kututenganisha na Mungu na kutuweka katika shida na kusumbua hata wale watuzungukao.

Usimuruhusu Shetani kukudanganya na kukuelezea kwamba zambi hazita mtesa mtu ye yoyote, ama kukuelezea kwamba hakuna mtu atakaye juwa kwamba wewe umetenda zambi---Mungu anajua yote uyatendayo. Na Biblia inasema kwamba zambi zako zitajulikana (Hesabu 32:23 na Luka 12:2).

Kuyapinga Majaribu

Shetani atatujaribu akitumia tamaa ambazo tayari tumezitaja hapo juu. Kutamani si kila mara vibaya ama zambi (kwa mfano: kutamani kuowa, kuwa na watoto, ama kuwa na pesa), ikiwa tamaa hizo zinaweza kutupeleka zambini ni vizuri kufanya bidii ili tuzitawale. Hii inaweza kutendeka kwa kusoma na kutii Neno la Mungu, kwa njia ya maombi ama kuomba kimoyo moyo, na kutumia hekima katika maisha yetu pia.

Kuna mambo matatu ambayo unaweza kutenda unapajaribiwa na zambi ama kujaribiwa na kitu kisicho mpendeza Mungu:

1. Kimbia jaribu. Wende mbali na mambo ambayo yanaweza kukujaribu. Ikiwa unajua nafasi ambayo unaweza kuenda na ukajaribiwe, ni vizuri usiende nafasi hiyo! Ikiwa kuwa pamoja na watu wa aina fulani itakujaribu hata utende zambi, usiende hapo wala usipate mda wa kuwa pamoja na

watu hao! Jiokowe mwenyewe na shida ambayo unaweza kujiletea mwenyewe na kuletea hata jamaa lako pia.

Soma kwa sauti: Mwanzo 39:7-12

Yusufu alikimbia nyumba ya kifalme alipo jaribiwa kutenda zambi za uasherati na mke wa mfalme.

2. Akili zako zitawaliwe na kuongozwa na Neno la Mungu. Neno la Mungu litakuweka nguvu ndani yako.

Soma kwa sauti: Zaburi 119: 7 na vesi ya 9

Kuweka kwa ufahamu maandiko itatusaidia kushinda majaribu.

3. Maombi. Omba kwa luga yako ya Roho Mtakatifu.

Soma kwa sauti: Matayo 26:41

Yesu aliwaelezea wanafunzi wake waombe ili wasiingie majaribuni (na baadaye wakatende zambi).

Soma kwa sauti: Luka 11:4

Yesu aliwafundisha wanafunzi kuomba Mungu ili awasaidie kushinda majaribu. Omba na kuwaalika wengine kukuombea na kuomba pia pamoja nao. Kuomba pamoja na wengine inatusaidia kuwa waaminifu kwa Mungu.

Ushindi Zidi ya Adui

Ili tupate ushindi zidi ya Shetani, tunahitaji kuelewa kwamba Shetani ni roho na pia ni nguvu zifanyazo kazi katika ulimwengu wa kiroho, na hata katika ulimwengu uonekanao kwa macho. Kama vile binadamu hatuwezi kuona kwa macho ya mwili ulimwengu huo wa kiroho ama kuona mitego Shetani ailetayo ili atutese, ulimwengu wa kiroho unaweza kusababisha mambo kutendeka katika ulimwengu uonekanao kwa macho.

Hatupashwi kuishi katika woga wa Shetani ama mapepo wachafu, kwa sababu Mungu ametupatia vyote tunavyo hitaji kujua kuhusu mipango ya Shetani na namna tunavyoweza kumushinda. Tunao ushindi zidi ya mipango michafu ya Shetani kwa nguvu na mamlaka ya Kristo.

Soma kwa sauti: Waefeso 6:12

Kuna vita vya kiroho kati ya watu wa Mungu na nguvu za Shetani zitawalazo maisha ya watu walio amua kumuchagua Shetani.

Silaha za Kiroho

Soma kwa sauti: 2 Wakorinto 10:3-5; Waefeso 4:13-15; na Ufunuo 12:10-11

Biblia inatufundisha kuhusu silaha tatu ambazo waaminio na kuzaliwa mara ya pili walio wanafunzi wa Yesu wanazo. Tunatumia silaha hizi za kiroho ili tujikinge na kushinda mipango ya Shetani. Kwa kuwa vita hivi ni vya kiroho tunahitaji kutumia pia silaha za kiroho. Yesu alitupatia silaha hizi ili tupige vita na kuvishinda, tuwe washindi maishani:

1. Jina la Yesu

Ushindi wa Yesu msalabani ulikuwa kamili na wenyewe kuenea. Alishinda zambi, Shetani, na kifo kwa mara moja. Wakati tuombapo kwa jina la Yesu na kutangaza jina hilo, Shetani anakimbia, shida zapata suluhisho, kuelewana kuna rejeshwa, wagonjwa wapokea uponyaji, walio

fungwa na mapepo wafunguliwa, na uovu unashindwa mbele ya haki. Tutumiyapo jina hilo tunatumia nguvu ambazo Yesu alizo tupatia.

Soma kwa sauti: Marko 16:17-18 na Matendo 4:10-12

Shetani na mapepo wa uovu wakutanapo na nguvu za Yesu wanapoteza uwezo wao na kushindwa kabisa. Hakuna uovu wowote ambao unaweza kuwashinda wana wa Mungu watumiapo jina la Yesu katika maombi na kumutangaza.

Soma kwa sauti: Yakobo 4:7 na 1 Petro 5:8-9

Mpinge Shetani, wakati anakuelezea kitu fulani, usimpe mda wa kuzungumza naye. Unacho hitaji kusema tu ni kifuatacho, "*Ninakupinga Shetani, Kwa jina la Yesu! Ninamukaribia Mungu.*" Shetani ataheshimu amri hiyo kwa kuwa inatolewa kwa jina la Yesu na kwa nguvu za Yesu.

2. Neno la Mungu

Kusoma maandiko ya Biblia Takatifu ndicho chakula chetu cha kiroho. Kulisoma Neno la Mungu kila siku latupatia hekima, uongozi, na nguvu katika maisha yetu. Biblia ndio nuru yetu ambayo yatusaidia kuelewa njia za Mungu na mambo ya kiroho.

Tunapo ujua ukweli kumuhusu Mungu, tunapokea ulinzi zidi ya Shetani na nafasi yoyote ile anayoweza kuipata ili atudanganye yapunguka kwa kiwango cha juu. Tunapo jua ukweli wa Biblia, uongo wa Shetani hautakuwa na nguvu za kutusumbua tena.

Soma kwa sauti: Luka 10: 17-22

Yesu aliwapatia wanafunzi mamlaka ya kumushinda Shetani na kuvunja mipango yake (kumkanyaga na kumzuwia). Wanafunzi walikuwa na nguvu ya kuwafungua watu walio fungwa na mapepo. Wewe pia una nguvu ya kuwafungua watu waliofungwa na mapepo hata nafasi ambazo kumetawaliwa na mapepo. Tuna soma katika Matayo 4:1-11 kwamba Yesu alipata ushindi zidi ya Shetani kwa sababu ya Neno la Mungu.

Shetani atajaribu kuweka ujanja katika Neno la Mungu ili akudanganye. Bali ikiwa tutasoma Neno la Mungu, tulitafakari, kulisema kwa sauti, na kuliweka kwa ufahamu, tunaweza kumshinda Shetani.

Tunaweza kutumia maandiko ya Biblia katika hali tunayo ishi. Tunapo shambuliwa na Shetani tunapashwa kutumia Neno la Mungu ili tumshinde. Umupingapo Shetani kwa kutumia Neno la Mungu, Shetani hawezikukushinda kwa sababu ukweli wa Biblia unatangazwa na kuwekwa katika vitendo.

Ushambuliwapo na Shetani umuelezee: "*Hauna mamlaka yoyote juu yangu lakini mimi nina mamlaka juu yako katika jina la Yesu! Toka! Ondoka ndani mwangu—(ama ndani ya jamaa langu, ndani ya kanisa langu, ama ndani ya mtu huyu)—katika jina la Yesu!*" Baada ya hiyo msifu Mungu na kumushukuru kwa ajili ya damu yake iliyo mwangika kwa ajili yako.

Soma kwa sauti: 2 Wakorinto 10:3-5; Waefeso 4:13-15; Waebrania 5:12-14

Mchungaji/Kiongozi zungumza na kundi: maandiko haya yanasema nini kuhusu kutumia Neno la Mungu kwa kumshinda Shetani?

3. Damu ya Yesu

Ufunuo 12:11 inasema, “*Nao wakamshinda [Shetani] kwa damu ya Mwana Kondoo [Yesu], na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.*”

Sisi ndio hao washindi ambao maandiko haya yanazungumzia. Kama vile wanafunzi walio zaliwa mara ya pili, tunapashwa kuelewa maana ya ufuluko wa Yesu. Kifo cha Yesu msalabani kilivunja kikamilifu nguvu za Shetani na hukumu itokanayo na zambi. Kwa kufufuka na kutoka kati ya wafu, Yesu alionesa mamlaka yake zidi ya Shetani na kazi zake.

Ikiwa sisi tumemukubali Yesu maishani mwetu kama vile Mwokozi, tumeokolewa kikamilifu na damu ya Yesu. Atatupatia ushindi katika kupinga mipango ya adui. Uwe na uhakika kwamba Mungu yuko pamoja nawe na atakupatia nguvu.

Shetani atakuvunja moyo, kwa kukudanganya akisema kwamba hauna nguvu za kumushinda. Atakuelezea kuwa wewe ni mwenye zambi ama atakukumbusha zambi ulizo tenda zamani. Atakapofanya hivyo, umukumbushe kwamba tayari umeoshwa na damu ya Yesu, na kumuamuru aondoke katika jina la Yesu. Shetani aogopa jina la Yesu na anatetemeka tunapo taja damu Hilo.

Ikiwa unasikia kuwa umechanganyikiwa katika mafikiri yako kuhusu jambo lolote, inakubidi kuomba damu ya Yesu ikusaidie maishani na kuomba damu ya Yesu itende kazi kuhusu jambo linalo kusumbua. Hii inamaanisha kwamba unasema, “*Yesu, ninaweka damu yako ya ulinzi kunifunika na kulinda maisha yangu.*” Hapo kalvari Yesu alilipa garama ya zambi (yote kwa jumla pasipo kuacha chochote). Yesu alishinda mipango yote ya Shetani na kukomboa maisha yako na hukumu—ijapo kuwa kama unajishitaki mwenyewe, ama Shetani anakushitaki, ama unashitakiwa na watu wengine. Yesu alikusamehe na kukufanya uwe safi.

Soma kwa sauti: 1 Yohana 2:1-2

Yesu ndiye mtetezi wetu mbele ya Baba tunapo tenda zambi. Yesu, Mwana Kondoo wa Mungu, alikubali damu yake imwangike, na akafa kwa nafasi yetu. Baadaye alifufuka, akashinda nguvu za mauti na kwa sasa anatuombea mbele za Baba pasipo kuchoka kila siku mchana na usiku. Kwa ukweli, huyu ni Mwokozi mzuri!

4. Silaha ya maombi

Maombi ni moja kati ya silaha nzuri tuliyo pewa na Mungu. Yesu alipo karibia kukabiliana na kifo msalabani, alijua kwamba alihitaji kuomba. Yesu akawaalika wanafunzi wake kuomba pamoja naye. Wewe pia, unahitaji kuomba kuhusu mambo mengi ya maisha. Munahitaji kuomba kama vile jamaa ama kama vile kanisa. Maombi ni kitu ambacho unapashwa kufanya kila siku.

Unaweza kuomba kwa luga yako ya kizalikio ama unaweza kuomba kwa luga ya Roho Mtakatifu. Katika kuomba utajifunza mambo mengi. Omba Mungu akupatie tafsiri kwa yale uyaombayo kwa luga. Uombe ukimshukuru Mungu kwa yote aliyo kutetendea. Tumia maandiko ukiwa katika maombi na hiyo itakusaidia kuwa na mamlaka zidi ya adui. Maombi yanaleta nguvu na kuwapa watu hekima katika kujua jinsi ya kumpinga adui wa maisha.

Uhakika

(Mchungaji/Kiongozi: Kuna watu wengi katika kanisa lako walio na matatizo kuhusu kutubu, wokovu, hatia na zambi. Saidia watu hawa wawe na uhakika kuhusu ahadi za Mungu. Labda kuna somo ambazo utahitaji kurudilia pamoja nao katika kitabu hiki, **Kutembea Pamoja na Yesu**, ili uwasadie kushinda shida zao.

Mchungaji/Kiongozi, uliza kundi masawli haya:

“Jee, una matatizo kuamini kwamba umeokoka kweli?”

“Jee, unamatatizo ya kujua ikiwa zambi zako zimesamehewa?

“jee, umesumbuliwa na zambi ambayo umeshindwa kuiacha maishani? ?”

Uwe wazi kwa mchungaji wako na umujulishe kiwazi kuwa una matatizo haya.

Mchungaji/Kiongozi: Uyarudilie maandiko yaliyo katika somo la 1, 2, na la 3 yanayo husu matatizo ya watu ulio nao. Wakati maandiko hayo yasomewapo uwaombe watu hawa kukubali maneno hayo kama yao, wayatumie katika maisha yao. Uwaombe warudilie wenyewe maneno ya Biblia mara kwa mara wao wenyewe. Maandiko yana nguvu ya kushinda shida hizo.

Maswali:

Mchungaji/Kiongozi: chukua mda mkizungumza kuhusu maswali haya.

1. Adui wako ni nani? (Shetani ndiye adui wetu; si watu, kabilia, kikundi fulani, ama serekali,...)
2. Ni nani aliye na nguvu zidi ya kila pepo chafu na mashambulizi yazo? (Yesu)
3. Ni aina ya mtego gani Shetani alitumia katika jamii yetu? Matokeo ya hiyo ni nini?
4. Ni mitego ya aina gani Shetani aliyo itumia katika maisha yako ya kipekee? Hiyo imekusumbua namna gani wewe na jamaa lako?
5. Taja mambo ambayo unaweza kufanya ili upinge na kumshinda adui?
6. **Soma: Mezali 16:18-19.** Tuna elewa kwamba Shetani anataka kuleta vurugu ndani ya kanisa – kwa hiyo ni nini tuna weza kujifunza kupitia andiko hili ?

Andiko kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi kujifunza na kuweka kwa ufahamu andiko hili:

Yakobo 4:7

“*Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia.*”

Somo la 16

Karama za Roho Mtakatifu

Katika somo la 11 ya mafundisho haya tulijifunza kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu na jinsi ubatizo huu unatumiya karama za Roho kwa kuwatia waaminio nguvu za kumushuhudia Yesu kwa ushujaa.

Katika somo hili jipya, tutajifunza mengi kuhusu karama za kiroho na namna Roho Mtakatifu anavyotumia karama hizo ndani ya kanisa na maishani mwetu. Zawadi nzuri ambayo tayari Mungu amemupatia kila mmoja aaminiye ni zawadi ya uzima wa milele kupitia imani tuliyo nayo ndani ya Mwanawe, Yesu Kristo, zaidi ya hiyo kuna vipaji vingi ambavyo Mungu amewapatia waaminio.

Katika somo hili tutajifunze yale ambayo Biblia inasema kuhusu karama hizo.

Mungu Anatupatia Vipaji vya Watu

Soma kwa sauti: Waefeso 4:11-12

Vipaji hivi tano, Mungu avitowavyo kwa kanisa, ni vipaji vya watu: Mtume, Nabii, Mwinjilisti, Mchunjaji, na Mwalimu. Hizo si ofisi ama vyeo, jinsi wamoja wetu wanaweza kufikiria. Vipewa hivyo ni viongozi walio na moyo ya utumishi, kama vile Yesu, wanajitowa ili wapate kuongoza kanisa na kulifundisha jinsi ya kufanya kazi ya Mungu hapa duniani.

Mungu Anatupatia Karama za Kutuwezesha

Soma kwa sauti: Warumi 12:4-9

Horoza hii ya kirama hupewa kwa watu ili wamtumikie Mungu na kulitumikia kanisa lake. Aaminiye anaweza kuwa na karama moja ama nydingi kati ya karama hizo ama vipawa.

Mtu anaweza kuwa na kipaji cha kufanya kazi ofisini kwa kuwasaidia wengine kufanya mpangilio wa kazi na kushugulikia mahitaji mengine mengi na kazi zingine zilizomo kanisani. Aliye na karama ya kutabiri anawaelezea watu mara kwa mara kuhusu mawazo na mipango ya Mungu. Mtu aonyeshaye ukarimu, ama upendo, ni vizuri kumpa moyo aendeleshe kazi hii. Karama zinazotajwa hapa ndizo Mungu amewapa waaminio ili wapate kufanya kazi yake vizuri.

Karama hizi hatuzipewi ili tuwe wenye kiburi ama kujiona kuwa sisi ni bora zaidi kuliko wengine. Tumepewa karama hizo ili kila mmoja wetu alitumikie kanisa, na kuwatumikia watu ulimwenguni. Andiko hilo latupatiya moyo wa kutumikisha karama (vipaji vya Mungu) zetu tofauti, kwa kadiri ya neema tuliyo pewa na Mungu. (Warumi 12:6).

Karama za Miujiza za Roho Mtakatifu

(Mchungaji/Kiongozi: Ikiwa watu wako wana matatizo kusoma maandiko marefu, uwasomeye andiko hili:)

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 12:1-31

Katika somo hili tuna soma kuhusu karama 9 zitolewazo na Roho Mtakatifu kwa kanisa (mwili wa Kristo).

Hii ni horoza ya karama hizo 9 zinazo andikwa katika 1Wakorinto 12:4-10:

Karama za Ufunuo:

Neno la Hekima
Neno la Maarifa
Kupambanua roho

Karama hizi tatu zaonesha mawazo ya Mungu na umuhimu wa kuelewa.

Karama za Luga:

Karama ya unabii
Karama ya kusema kwa Luga
Karama ya tafsiri ya luga

Hizi karama tatu zinazungumzia Neno la Mungu na uongozi wake.

Karama za Nguvu:

Karama ya Imani
Karama ya Miujiza
Karama ya Kuponya

Hizi karama 3 zionyeshazo nguvu za utendaji kazi za Mungu zionezanazo maishani mwetu na katika hali ambazo tunazo ishi.

Tuna elewa karama hizi kama vile alama, zionezanazo, ama kazi za Roho Mtakatifu atendazo kupitia watu wanao mwamini Kristo. Karama hizi zote ni za kimiujiza. Muujiza, maana yake uwezo unao pita mbali zaidi akili za kibinadamu zapita pia uwezo wake za utendaji kazi, na matendo hayo yote yatendeka na Mungu mwenyewe, hayatendeki na nguvu ama uwezo wa kibinadamu. Hayo yaonesha kwamba Mungu yuko na anafanya kazi akitumia nguvu zake.

Mafasiriyo ya Karama

Neno la Maarifa ni karama iletayo ujuzi na kuelewa mtu ama kuelewa mambo ambayo hayawezi kueleweka kwa njia ya kawaida. Huu ni ujuzi ambao Mungu atowao kuhusu mtu fulani ama mambo fulani. Si kitu ambacho mtu amekisoma shuleni ama kitu ambacho tayari kimejulikana. Ni ujuzi ambao unatoka moja kwa moja kwa Mungu. Mungu anajua siri ya miyo wa mtu.

Neno la Hekima ni karama atowayo Mungu kwa wanenaji ili wawe na urahisi wa kutowa ujumbe munamokuwa hekima. Karama hii inatowa ufunuo (ujuzi) wa mwongozo wa Mungu, inatoa pia mwongozo kuhusu mambo fulani. Inatufundisha tufanye nini kuhusu hali hiyo.

Kupambanua Roho ni uwezo wa kuona na kujua roho. Waaminio wamepewa uwezo wa kuona na kutambua mahali ambapo pepo mchafu yuko, na kuelewa ni nini pepo yule anatafuta. Hii karama inaweza pia kupatia aaminiye uwezo wa kutambua uwepo wa malaika. Karama hii inasaidia pia aaminiye utambuzi kuhusu roho wa aina fulani ifanyayo kazi ndani mtu, ikiwa ni Roho wa Mungu, ama Roho wa watu. Roho Mtakatifu anawapatia waaminio ujuzi unaohusu roho.

Karama ya Unabii ni uwezo wa kimaajabu ya kueleza maneno ya Mugu na mawazo yake kwa mtu ama hali fulani iliyoko. Aaminiye awaletea watu ujumbe utokao kwa Mungu. Mara ujumbe huo ni kutabiri kuhusu mambo yajayo, Biblia yasema pia kwamba neno la unabii lawapa watu moyo, lafariji, lajenga watu, wala halileti mafarakano (1 Wakorinto 14:3). Ujumbe wa watu kulaumiana wao kwa wao kwa hali ya kukosa hekima watowapo unabii haitoki kwa Mungu. Unabii haupingani kamwe na maneno ya Biblia unabii wakubaliana kila mara na yale Biblia isemayo.

Karama ya Luga ni luga ya maombi unayo pokeao unapo jazwa na Roho Mtakatifu (ubatizwapo kwa Roho Mtakatifu). Unasema kwa luga usio ijua kwa luga ambayo hujawai kujifunza. Hii ni namna isiyo ya kuwaida ya kuzungumza kwako na Mungu. Wakati huu ni Roho Mtakatifu azungumza kupitia kinywa na sauti yako ***katika maombi kwa Mungu***.

Jambo la pili, karama ya luga yaweza kutumiwa mda ambapo wakristo wanakusanyika pamoja. Mtu anaweza kupata ujumbe ***kutoka kwa Mungu*** na kusema ***kwa luga kati ya watu wanaokusanyika pamoja naye***. Hii ni njia ya pili ya kutumiwa kwa luga siyo maombi kwa Mungu, lakini ni ***ujumbe utokao kwa Mungu kwa ajili ya waaminio*** wakusakapo pamoja.

Wakati karama ya luga utumiwapo katika kusanyiko, Biblia inasema kwamba utafsiri wa ujumbe huo ufanyike kupitia mwamini mwengine. Maana ya hiyo, ni kusema mkristo mmoja atoa ujumbe utokao kwa Mungu kwa luga na mkristo wa pili atapewa tafsiri ya ujumbe huo wa Roho Mtakatifu wa Mungu, na tafsiri ya ujumbe itatolewe kwa luga ya mahali ama luga inayo sikika na kusanyiko lote.

Tafsiri ya Luga inafanyika wakati Roho Mtakatifu ampatia aaminiye tafsiri ya maneno ambayo tayari yamesemeka katika ujumbe kwa luga. Hakuna yejote atakaye elewa ujumbe huo utolewao kwa luga ya Roho Mtakatifu, bali ujumbe huo ulio nenwa kwa luga utaeleweka na wote wakati Roho Mtakatifu atakapo towa tafsiri. Hii ndio sababu ni vizuri tafsiri itolewe kila mara ujumbe utolewapo kwa luga.

Karama ya Uponyaji ni upako wa kimaajabu wa Roho Mtakatifu unao waruhusu waaminio kuwaombea wagonjwa ili wapokeye uponyaji ama kutangaza uponyaji kwa ajili ya wagonjwa. Kuna mara waaminio wanawawekea mikono walio wagonjwa; mara ingine mtu anaomba pasipo kuweka mikono. Mungu ndiye aponyaye kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Karama ya Miujiza ni karama isiyo ya kawaida ipeyayo mamlaka kwa kumupatia aaminiye nguvu za kutenda miujiza kwa jina la Yesu Kristo.

Karama ya Imani hutolewa kwa aaminiye na kumupatiya imani na uhakika wa Mungu pia, kuomba akiamini kwamba mambo yasiyo wezekana yatatendeka. Hiyo hupewa zaidi na Roho Mtakatifu wakati wa mahitaji makubwa kupitia maisha ya maombi ya waaminio.

Karama Zatolewa Kwa Wote Waaminio

Kila moja kati ya karama hizi za kimaajabu hutolewa na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anaweza kukupatia wewe moja kati karama hizi wala ampe mkristo mwengine kwa mda wowote. Biblia inasema kwamba Roho Mtakatifu anatowa karama hizi jinsi atakavyo. Hatuwezi kununua karama hizi. Ni habari nzuri ya kweli kujua kwamba Mungu anataka kukutumia wewe ukitumia karama hizi ili uwasakiwengine!

Mara mkristo akitumiwa na moja kati ya karama hizi za Roho, anaweza kufikiri ama kusema: “*Nina karama ya unabii!*” Tuelewe kwamba hii siyo kweli. Kwa kuwa Roho Mtakatifu unachagua mtu na karama ambayo mtu huyo atakayo itumia (1 Wakorinto 12:11). Karama ni za Mungu na Roho Mtakatifu anazitumia anavyotaka kwa ajili ya faida ya kanisa! Usimutiliye Mungu mipaka ukifikiri kwamba wewe si bora ili upate kutumiwa katika karama za Roho Mtakatifu. Kila aaminiye aweza kutumikishwa katika karama za Roho. Usifikiri kwamba unajua ni karama gani unayo ihitaji ama kuipenda. Tumuachie Mungu uhuru wa kututumia jinsi atakavyo.

Si vizuri kwa yule anaye amini kusema kwamba “*nina karama ya miujiza*”.ni vizuri kusema “*Mungu alinitumia katika karama hiyo, Mungu asifiwe*” Ikiwa Mungu alikutumia katika karama fulani ni vizuri uwe mnyenyeketu kwa kumupatia Mungu utukufu. Karama na nguvu si zako, bali ni za mungu! Jinsi uendeleavyo kumutafuta Mungu, naye ataendelea kukutumikisha.

Kutaka Kutumiwa na Mungu

Biblia inasema, “*Takeni karama zilizo kuu*” (1 Wakorinto 12:31). Si vibaya kutaka kwa moyo wako wote kutumikishwa na Mungu katika karama za Roho. Mungu abariki hali hii. Bali moyo wako unapashwa kuwa safi na uwe wenyewe kukubaliwa na Mungu. (Warumi 12:1-2). Mafikiri yako yanapashwa kuwa yakiyafikiria mambo ya Mungu, na yasiwe na msukumo wa tamaa za ubiniasi ili utazamiwe na watu ama ukitafuta vyeo.

Soma kwa sauti: Wakolosai 3:2; Warumi 8:5-7

Ikiwa mafikiri na moyo wako yatazamia mambo ya Mungu, na kumsikiliza Mungu wakati uombapo, Mungu atakutumikisha katika karama hizo. Anataka akutumikishe katika njia zake za kimaajabu. Kuna mahitaji mengi katika jamii na jamaa lako, na Mungu anataka kujibu mahitaji hayo kupitia utii wako kwake. Usisite kuchukua hatua ya imani. Uamini kuwa Mungu atakutumisha.

Kati ya karama hizi iliyo kubwa ama bora ni gani? Karama ilio kubwa ama bora ni hiyo ambayo inayo hitajika zaidi kwa mda ufaao. Ikiwa mtu ni mgonjwa, labda hauwezi hitaji ujumbe utelewao kwa luga-mdi huu unahitaji karama ya uponyaji. Ikiwa unakutana na hali ngumu ndani ya jamaa, utahitaji neno la hekima pahali pa karama ya tafsiri ya luga. Kitu unacho hitaji kufanya hapa ni kuomba usaidizi wa Mungu; ndipo karama ambayo Roho anataka ifanye kazi itatumia kwa mtu ambaye Roho anataka kumtumia.

Roho Matakatifu Afanya Kazi Kati ya Waamini

Soma kwa sauti: Yohana 16:7; 12-15

Katika andiko hili Yesu anawaelezea mitume wake kuhusu kazi na ujio wa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu aishi ndani yako. Aliingia ndani yako wakati ulipomupatia Yesu maisha yako. Roho Mtakatifu ni Roho wa Yesu, akufundishaye, akupatiyaye moyo, na akupatiaye nguvu za kuishi katika njia nzuri, imupendezayo Mungu. Roho Mtakatifu amuinua na kumupatia Yesu sifa. Roho Mtakatifu yuko pamoja nawe kila saa na kila siku. Unapohitaji kitu kutoka kwa Mungu, umuombe Yesu na Roho Mtakatifu wake ataanza kutenda ndani yako na kukupitia wewe, kwa nguvu na upako. Mda mwengine utahitaji kungojea jibu la Mungu lifike kwa mda wake.

Ikiwa utahitahiji kutumiwa katika nguvu na karama za Roho Mtakatifu, unapashwa kuishi maisha yalio safi. Roho akuoneshapo kwamba unapashwa kubadilika ama kutubu ama kufanya kitu fulani, uwe mnyenyeketu na mwenye kutii. Ikiwa wewe ni mtiifu kwa mapenzi ya Mungu, Roho Mtakatifu atakutumia kwa njia za kimaajabu na nguvu. Yesu alisema: “*Heri wenyе moyo safi; maana wao watamwona Mungu*” (Matayo 5:8). Wale walio safi moyoni wataona nguvu za Mungu maishani mwao.

Kutumia Vizuri Karama za Roho

Paulo aliandika kuhusu karama za kiroho katika 1 Wakorinto 14. Hapo Paulo atupatia mwelekeo ulio wazi kuhusu namna karama zahitaji kutumiwa wakristo wakusanyikapo pamoja:

Mchungaji ama kiongozi wa kundi ama wa kanisa anapashwa kuhukikisha kwamba kila kitu kifanyikacho cha tendeka “*kwa uzuri na kwa utaratibu.*” (1 Wakorinto 14:40). Maana ya hiyi ni kwamba hakupashwi kupigwa kelele ama kuonyesha mambo yafananayo na mambo ya ibada ya sanamu. Mungu anataka karama zake zitumiwe kwa njia iliyo halali na ya utuaratibu na utulivu kanisani. “*Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani, vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu.*” 1 Wakorinto 14:33.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 14:29-33. Watu watoapo unabii, watowe unabii mmoja baada ya mwengine, ili waruhusu wengine kupokea na kuhutubia. Viongozi na wahutubiaji wa maneno ya unabii wachunguze, wapime ikiwa maneno yatolewayo kama unabii ni ya Mungu. Wachungaji/Viongozi watakapo chunguza wataelewa ikiwa unabii huo unatoka kwa Mungu ikiwa wanaulinganisha na mafundisho ya Biblia.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 14:26-28. Ujumbe utolewapo kwa luga kuititia mtu fulani, sote tuombe ili ujumbe huo utafsiriwe na kueleweka na kila mmoja. Mtu aombaye kwa luga ni vizuri pia aombe ili kuwe tafsiri ya maneno. Ikiwa hakuna tafsiri ni vizuru yule asemaye kwa luga acae kimya; anaweza kuomba Mungu kwa luga akiwa katika ukimya.

Kitu cha muhimu sana ni kwamba, kila kitu kitendekacho kuititia karama za kiroho cha tendeka ili lijenge na kupatia kanisa moyo. (1 Wakorinto 14:26).

(Kwa ajili ya Wachunjaji na viongozi:

Ni vizuri kuwapa watu wako moyo ili watafute kuwa na karama za kiroho; umupatiye Roho Mtakatifu mda wa kutumia watu katika karama hizi ndani ya kusanyiko kanisani mwako. Hii si tukio ambayo utakayo tayarisha; utachukua tuu mda wakusikiliza ni nini Mungu anataka kuwaletea watu wako kupitia karama za Roho mtakatifu. Kumbuka kwamba, mtume Paulo anatuelezea: “*Basi, ndugu, imekuaje? Kila mmoja ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo, ana luga, ana tafsiri. Mambo yote yatendeke kwa kusudi la kujenga.*” (1 Wakorinto 14:26).

Amini kwamba Mungu atatumia watu wako. Hii itawasaidia kukomaa kiimani na watakuwa msaada kwa kanisa lako. Wakati aaminiye atumikishwapo na Roho Mtakatifu, katika karama, hii haiwafanyi wawe watakatifu zaidi ama bora kuliko wengine. Ni vizuri wachungaji na viongozi wawapatie watu moyo na kuonesha moyo wa unyenyekevu ili wawe mfano mzuri kwa watu wengine.

Ni vizuri kusaidia mtu atumiwaye katika karama hizi ikiwa anazitumia kwa njia za kibinagsi. Uwe mwenye moyo wa huruma unapo sahihisha mtu kama huyu, na usiwe mwenye jeuri. Watu wako watajifunza kupitia wewe. Watakapoona jinsi ulivyomsaidia yule ambaye hakuwa katika usawa. Watatambua kwamba ni usalama kujifunza na kukomaa katika kutumia karama wakiwa chini ya uongozi wako. Uombe na Mungu atakusaidia kuelewa na kuwaongoza watu wako ili Mungu awatumie katika karama za kiroho. Mungu anataka kulibariki kanisa lako na karama hizi.

Ikiwa unahitaji mafundisho ya zaidi na kuelewa yanayo husu karama za kiroho, uombe ama umtafute mtu wa Mungu mwengine ili akuongoze. Mungu atakupatia yale ambayo unahitaji.)

Njia Iliyo Bora

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 12:31 na sura ya 13

Njia iliyo bora ni ya kutumiwa na Mungu? Ni njia ya upendo, isiyo kuwa na ubinagsi. Ni njia ya Yesu. Kila kitu ambacho Yesu alitenda kwa ajili yetu, kwa ajili ya watu walio umbwa na Mungu. Yesu alikuja kuwatumikia watu (Marko 10:45). Andiko hili latuelezea kwamba tutumiye karama za Roho Mtakatifu katika unyenyekevu na upendo, si kwa shabaa ya kutaka kuonekana bora zaidi kuliko wenginge.

Biblia inatufundisha kwamba **sote** tutafute kutumiwa na Mungu kupitia karama za Roho; bali ni vizuri zaidi kutumiwa katika karama **na** kuwapenda wale watuzungukao. Karama pasipo upendo ni bure; upendo pasipo karama ina maanisha kuwa hakuna nguvu. Mungu anataka tuwe na nguvu na tuwe pia na karama.

Maswali:

Mchungaji/Kiongozi: Soma kwa sauti maandiko na maswali na uombe kundi kuzungumza kuhusu haya maswali.

1. Ni namna gani Roho Mtakatifu afanya kazi katika maisha ya waaminio? (Roho Mtakatifu anatufundisha, anamuinua Yesu kila mara; Anatuongoza, atupatia hekima, na anafanya kazi ndani yetu kupitia karama za kiroho kwa ajili ya ubora wa kanisa)
2. Kwa nini tuna pewa karama za kiroho? (1 Wakorinto 14:12: ili kuwapa wengine moyo, na kujenga watu kanisani.)
3. Mda wakristo wakusanyikapo na mwamini mmoja asema kwa luga ni nini inapashwa kutendeka baadaye? (Wakristo wengine wanapashwa kuomba ili kuweko tafsiri. Ikiwa hakuna mtafiri, ni ujumbe moja ama ujumbe tatu ndizo wahitajika kutolewa. Yule aombaye kwa luga ni vizuri aombe ili tafsiri iwepo. 1 Wakorinto 14:27-28).
4. Jee, unaweza kushirikisha kwa kundi uliyo yaona wakati Roho Mtakatifu alipo kutumikisha wewe ama mtu mwengine katika karama moja ama karama nyingi? Shirikisha uliyo yaona ama uliyo yaishi. Hiyo itawapa wengine moyo wa kujua kuwa wao pia waweza kutumiwa na Roho Mtakatifu.
5. “*Njia iliyo bora zaidi*” ambayo tunapashwa kuonesha katika kutumia karama za kiroho nini gani? (Tunapashwa kuonesha upendo kila mara)

Mchungaji/Kiongozi: kuna maswali ya zaidi ikiwa kuna mda wa kujifunza ambao unaobaki:

Soma kwa sauti baadaye uulize: “*Ni karama gani za Roho Mtakatifu sinazo semeka katika vesi hizi?*”


1. **Soma kwa sauti: Matendo 3:1-7** (Ni karama gani ya Roho Mtakatifu ionekanayo? Karama ya uponyaji.)
2. **Soma kwa sauti: Matendo 16:16-18** (Ni karama gani ya Roho ionekanayo hapa? Kupambanua Roho)
3. **Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 14:27-28** (Ni karama gani za Roho zinazo tajwa hapa? Karama ya kusema kwa luga, na karama ya kutafsiri)
4. **Soma kwa sauti: Matendo 19:11** (Karama gani ya Roho ionekanayo hapa? Karama ya miujiza)
5. **Soma kwa sauti: Matendo 21:10-11** (Karama gani ya Roho ionekanayo hapa? karama ya unabii?)
6. **Soma kwa sauti: Matendo 10:19-20** (Ni karama gani ya Roho Mtakatifu tuionayo hapa? Neno la Ufahamu na Neno la Hekima)
7. **Soma kwa sauti: Matendo 14:8-10** (Karama gani ya kiroho ionekanayo hapa? Karama ya imani, na ya Uponyaji.)

Somo kwa ufupi:

Roho Mtakatifu anatowa Karama za kiroho jinsi anavyotaka (1 Wakorinto 12:11). Karama za kiroho hazitolewi ili kumufanya mkristo mmoja awe bora zaidi kuliko wengine. Karama za kiroho hutolewa ili kulijenga kanisa. 1 wakorinto 14:18-19 inasema "*Namshukuru Mungu ya kuwa nanena kwa luga zaidi ya ninyi nyote; lakini katika kanisa napenda kunena maneno matano kwa akili zangu, nipate kuwafundisha wengine, zaidi ya kunena maneno kumi elfu kwa luga.*" Mtume Paulo yuko anatuelezea kwamba Mungu anataka tuwe na nguvu na tumaini kupitia Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani yetu. Hii ndilo jambo Mungu anatafuta wakati atutumiyapo katika karama hizi.

Kama vile ndani ya sekta zote maishani, inabidi tuwe waangalifu tusiwe wenyе kiburi. Inawezekana, una weza kujisikiya kiburi kuhusu jinsi Mungu anavyo tenda kazi kupitia sisi. Bali tukumbuke kwamba, "*Kiburi hutangulia uangamivu; na roho yenyе kutabakari hutangulia maanguko*" (Mezali 16:18) na "*ninyi nyote jifungeni unyenyekevu mmoja kwa mwengine; kwa sababu Mungu huwapinga wenyе kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema.*"

(1 Petro 5:5). Tuna hitaji kila mara kuwa wanyenyekevu. Karama za Mungu zapewa kwa wale wanataka na walio tayari kutumikishiwa na Mungu. Wale ambaо wanatafuta kuonekana mbele ya watu na kutafuta heshima hawakuchaguliwa kuwasaidia watu wengine.



Andiko kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi lako kujifunza na kuweka kwa ufahamu andiko lifuatalo:

1 Wakorinto 14:12

"Kwa kuwa mnatamani sana kuwa watu wenyе karama za roho, takini kwamba mzidi sana kuwa nazo ili kulijenga kanisa."

Somo la 17

Uwakili, Chakumi, na Sadaka

Zaburi 24:1: “*Inchi na vyote vijazavyo ni mali ya Bwana, Dunia na wote wakao ndani.*”

Soma kwa sauti: Zaburi 50:10-12

Sisi ni mali ya Mungu, vitu, na hata pesa tulizo nazo zote ni mali ya Mungu. Somo hili litatusaidia kujifunza namna imupendezayo Mungu kwa ajili ya kutunza vitu tulivyo navyo hapa ulimwenguni.

Uwakili

Biblia inatufundisha namna ya kutunza, kutumia, na kufanya uwekezaji wa mali tuliyo nayo, hata ikiwa nyingi ama ndogo. Biblia inatufundisha kwamba sisi ni watumishi tuu watunzao, ama mawakili wa vitu ambavyo Mungu alituruhusu tuwe navyo maishani.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 6:20

Sisi si mali yetu wenyewe, sisi ni mali ya Mungu kwa jumla. Yesu alitununua kwa damu yake. Miili yetu, jamaa zetu, vitu vyetu, utajiri wetu na maisha yetu yote ya sasa na ya baadaye yote ni ya Mungu.

Mungu Ametufanya Tuwe Mawakili Wake

Mungu ametupatia kazi ya kuwa mawakili wa vitu ambavyo ameviweka mikononi mwetu.

Soma kwa sauti: Mwanzo 1:27-30

Mungu alipowaumba Adamu na Eva hakuwapa bustani ili iwe yao, bali aliwafanya wawe mawakili wa bustani. Waliwajibika mbele ya Mungu kuhusu namna walitunza bustani **yake**. Adamu na Eva walipashwa kuwa watiifu kuhusu yale Mungu aliwaomba wafanye ndani ya bustani, lakini wakawa waasi. Kwa sababu hiyo walipoteza kazi waliopewa na Mungu humo ndani ya bustani. (Mwanzo 2:15).

Wakili ama Mtumishi atunzaye vitu ni mtu aliye na mamlaka ya kutunza na kuchunga vitu visivyo kuwa vyake. Vyote tulivyo navyo (utajiri wetu, nyumba, gari, shamba, vitu vya nyumbani, mwili, na akili,...) si mali yetu bali hivi vyote ni mali ya Mungu. Tunapashwa kuwa mawakili, ama watumishi watunzao vizuri, vitu vyote tulivyopewa na Mungu.

Soma kwa sauti: 2 Wakorinto 5:10

Tume wajibika mbele ya Bwana wetu, yeye ni Mungu mwenyewe. Tutaulizwa mbele za Mungu kuhusu namna tunavyo ishi maisha yetu na kutunza mali tuliyo pewa na Mungu.

Yesu Afundisha Kuhusu Uwakili

Soma kwa sauti: Matayo 25:14-30

Yesu alieleza hadisi hii, iitwayo “**mfano**”, ili tupate kuelewa ni nini ambayo Mungu anatafuta katika maisha yetu. Wakili anatunza vitu ama vyashara vya bwana wake wa kazi kwa ajili ya faida ya bwana huyo, si kwa ajili ya faida yake yeye mwenyewe kama vile mtumishi. Katika hadisi hii, Bwana alishangaa kuona mmoja kati ya mawakili hakufanya kazi jinsi inavyo stahili kwa kuwa hakuleta faida yoyote. Kama mawakili, tunahitaji

kutumia kwa hekima yote tuliyo pewa na Mungu ili tuyatunze ama tuwe waangalizi, na tusiwe kama huyu wakili aliye tenda kwa ujinga.

Tutazame huu mfano alio utoa Yesu.

Mchungaji/Kiongozi, uliza maulizo yafuatayo:

1. Mtu aliye enda safarini ni nani? (Huyu mtu anawakilisha Yesu)
2. Watumishi ni wa nani? (Watu wa Mungu)
3. Kwa nini watu wawili wakwanza walipewa zawadi? (Walitumia mali na vitu walivyo pewa kwa hekima.)
4. Kwa nini mtumishi wa mwisho ameazibiwa? (Mtu huyu alikuwa mvivu na mzaifu. Mtu huyu aliogopa kuongoza maisha yake vizuri, na hakutumia vizuri uwezo wake ama pesa alizo pewa ili amutumikie Bwana wake.)

Kupitia mfano huu Yesu atufundisha kwamba tunapashwa kuwa mawakili waaminifu wa yote tuliyo pewa na Mungu maishani mwetu. Ikiwa sisi ni mawakili waaminifu, tutaleta faida katika ufalme wa Mungu. Ndipo Bwana wetu atakupo tupatia kazi kubwa tutakayo isimamiya.

Soma kwa sauti: Luka 16:10-13

Ukiwa mwaminifu katika mambo madogo, ndipo Bwana wako atakapo kuweka uwe wakili wa mambo makubwa. Uwaminifu huanza na yale unayo kwa sasa. Ikiwa Mungu haoni kuwa unaweza kutunza vizuri vitu vidogo ama pesa ulizo pewa, anasema kwamba hawezi kuruhusu uwe na mwangalizi wa vitu vingi.

Tunapokuwa waaminifu katika mambo madogo, tutapewa nafasi ya kumutumikia Mungu katika mambo makubwa. Bwana wa kazi mzuri hapani kazi kubwa ya usimamizi kwa mtu ambaye si mwaminifu kwa kazi ndogo.

Labda unaweza kusema, “*Lakini mimi nina kidogo sana!*”

Soma kwa sauti: Marko 12:41-44

Hata aliye maskini anaweza kuwa mwaminifu kwa yale madogo aliyo nayo.

Mawakili Wazuri Katika Sekta Zote za Maisha Yetu

1. Tunapashwa Kuwa Mawakili Wazuri wa Miili na akili Zetu.

Soma kwa sauti: 2 Wakorinto 5:10 na 1 Wakorinto 6:19-20

Kristo alitununua na damu yake, ili tuwe wake: miili, akili, na pumzi. Kwa sababu sisi ni mali ya Kristo, tunapashwa kutunza miili yetu vizuri ili ipate kumtukuza Mungu. Mazowezi mabaya ya mwili, tendo la ndoa ama tamaa inje ya ndoa, tamaa ama matendo mabaya, vitendo vyaya jeuri, vivu, chuki na mambo yafafanayo hayo siyo ya Mungu. Miili yetu na mioyo yetu sherti itawaliwe na Mungu, kwa sababu tutatoa hesabu mbele ya Yesu kuhusu namna tunavyo ishi.

2. Ni Vizuri Tuwe Wenye Hekima Kuhusu Namna Tunavyo Tumia Wakati Wetu na Majira Tuyapatayo.

Saa zote katika maisha yetu tujuwe kuwa tu mali ya Mungu. Tutazame saa zetu kuwa ni za muhimu sana na tuepuke kuzitumia kwa mambo yasiyo faa. Tusipo tumia saa zetu vizuri wakati tungali vijana tunapo kuwa na nguvu, inaweza kuleta matokeo mabaya wakati tunapo

kuwa wazee. Tusipoteze pia katika kazi zetu na kusahau kumpatia Mungu kwa kufanya kazi zake.

Soma kwa sauti: Zaburi 90:12

3. Sherti Tuwe Watunzao Udongo Vizura.

Soma kwa sauti: Mezali 28:19-20

Ikiwa una udongo ama ardhi, waweza kujifunza namna ya kulima ili upate chakula, kwa kulisha jamaa lako na kusaidia pia wasiyo jiweza, na kujibu kwa mahitaji mengine uliyo nayo. Sherti watu watumike na udongo utumiwe kwa njia inayo faa (Kutoka 23:10-12). Mungu anatuomba kulima shamba zetu ili tupate mafanikio.

Waweza kujifunza pia kuwa wakili mzuri wa mazingira kwa kuyalinda vizuri, tutumie udongo kwa akili. Tujifunze kuhusu namna ya kubadilisha mimea, umuhimu wa kupiganisha mafuriko na mimemonyoko ama miporomoko ya udongo ama ardhi, namna ya kupiganisha ukame, na jinsi ya kuepuka magonjwa ya mimea. Mungu anaweza kukuletea watu wakusaidie kujifunza jinsi ya kupata faida itokayo kwenye ufugo na mashamba zako.

4. Tuwe Watu Watunzao Pesa Vizuri

Mambo mazuri mengi kwa ajili yetu na kwa ajili ya wengine yaweza kutendeka ikiwa pesa zetu zatumiwa vizuri. Ni vizuru kuandika matumizi ya pesa zote tunazo zitumia, na kujua pesa ngapi zimetumiwa kwa ajili ya mahitaji gani. Ni vizuri pia kwa viongozi wa kanisa kuweka kwa maandiko jinsi pesa zimeingia na matumizi yazo. Hiyo itasaidia kwa ajili ya kupanga miradi mbalimbali ya kanisa, pia kuepuka mizozo isiyo faa.

Soma kwa sauti: Mezali 17:23

Kutowa rushwa ina katazwa na Mungu, vivyo hivyo wizi unakatazwa ama kutumia vibaya mali ya mtu mwengine. Mungu anaona vyote tufifanyavyo, hata ikiwa watu wengine wao hawawezi kuona. Tutahukumiwa na Mungu ikiwa tuna tumia vibaya mali ya mtu mwengine.

Soma kwa sauti: 1Timoteo 6:10

Vesi hii inatuelezea kwamba kutafuta pesa itatuongoza kwenye uharibiu. Vesi hii haisemi kwamba kuwa na pesa ni vibaya; bali yasema waziwazi kwamba **kupenda pesa** ndilo shina la mabaya yote. Tunapashwa kutumia pesa kwa hekima, si kwa kuzitumia kwa ubinafsi, maishani. Yesu alisema kwamba, “*kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli?*” (Luka 16:11). Yesu ataka tuelewe kwamba pesa si mbaya, bali tuelewe kwamba tamaa ya pesa yaweza kutuharibu. Tuchukuwe uamzi wa kutumia pesa kwa njia ya hekima. Tuchukue uamzi wa kuwa waaminifu katika kazi na ushirika wetu wote.

Biblia yatufundisha kwamba ikiwa tuna muheshimu Mungu kwa pesa na vitu vyetu, hiyo itatusaidia kutosheka na kubarikiwa maishani pia. Shabaa yetu isiwe ya kupata utajiri, bali iwe ya kutumia mali yetu katika njia impendezayo Mungu: kujibu kwa mahitaji ya jamaa zetu na kulisiaidia kanisa la Kristo.

Soma kwa sauti: Warumi 13:5

Tusifungwe na kupenda pesa, tuwe watu wanaotosheka na yale tuliyo nayo. Hii haisemi kwamba tusipende kuishi maisha yalio mazuri; bali

tuwe watu wanao mheshimu Mungu kwa kungojea yale atupatiyayo. Angalisho katika andiko hili la tualika kumtegemea Mungu, si kutazama pato la kibinagsi. Si vibaya kuwa na chakula cha kutosha, mavazi, na nyumba nzuri, ama kuwa na maisha mazuri yanayo weza kutusaidia kumtumikia Mungu vizuri. Matarajio ya namna hiyi ni mazuri, bali yahitaji kutawaliwa na Mungu maishani ili tamaa za ubinagsi zisiingie moyoni mwetu.

Soma kwa sauti: Matayo 6:30-33

Yesu anasema kwamba Baba Mungu aliahidia kutushugulikia. Tumutumainie kwa kujibu kwa mahitaji yetu.

Soma kwa sauti: Wafilipi 4:19

Mungu anawapenda na atawapatia yale munayo yahitaji kwa kuwa ninyi ni wa Yesu.

4. Vyote tulivyo navyo tunapashwa kuvitunza vizuri na kuvitumia kwa hekima.

Kwa mfano, ikiwa mtu anakuazima chombo kama: jembe, mpanga, radio, kinga, pikipiki, gari,... unapashwa kivitunza vizuri ili uvirudishe katika hali nzuri. Mungu anaporuhusu tuwe na kitu, tunapashwa kukitunza vizuri kwa kuwa tunamwakilisha Mungu na tunatunza vitu vyake ulimwenguni.

Chakumi

Neno chakumi maana yake moja ya kumi. Kutowa chakumi maana yake ni kumrudishia Mungu moja ya kumi ya yale tulio pata kwa kuendelesha kazi yake. Biblia inatufundisha kupitia maandiko mengi kwamba moja ya kumi ya chochote tunacho kipata, ikiwa ni vitu ama pesa, ni vya Mungu.

Katika Biblia kuna mifano mingi ya watu waliyo towa chakumi chao kwa Mungu. Watu wa Mungu walitowa chakumi kila mara. Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, kutowa kwao kuliwaleteya mibaraka kutoka kwa Mungu.

Yakobo aliahidiya kutowa chakumi ikiwa atarudi nyumbani kwao kwa usalama (Mwanzo 28:20-22). Kama vile Yakobo, tuna towa chakumi kwa kumushukuru Mungu kwa yale aliyo yatenda kwa ajili yetu.

Kwa Nini Tunatowa Chakumi?

Soma kwa sauti: Malaki 3:10-11

Shabaa ya kwanza ni kuheshimu agizo la Mungu.

Shabaa la pili ni kwamba chakumi chatuleteya mibaraka, katika jamaa, katika miradi, na katika kanisa pia. Chakumi chatuletea mafanikio, kwa sababu tunaishi katika mibaraka ya Mungu, na kwa kuwa hatuishi chini ya laana! Tunapo mheshimu Mungu na kutowa chakumi, Mungu atuondoleya chochote kinacho weza kuiba mibaraka yetu. Ni jambo la maana kuelewa kwamba mafanikio haimaanishi kuwa na utajiri mwingi pekee, lakini maana ya hiyo ni kwamba tutapata yanayo tosha kwa ajili ya mahitaji yetu na ya jamaa letu, na zaidi ya hiyo. Maana ya mafanikio ni kujibiwa kwa mahitaji tulio nayo, na kuongezeka.

Mungu anataka tutowe kwanza sehemu yake kidogo, chakumi, mbele ya matumizi. Si baada ya kutumia yale tulio yapata ndipo tutowapo, bali chakumi kitolewe mbele.

Soma kwa sauti: Mezali 3:9-10

Tunapashwa kumuheshimu Mungu kwa kumutoleya kwanza chakumi ya yote tupokeyayo; ikiwa ni mazao ya shamba zetu, mifugo, kazi yetu, ama mshahara. Pia, tuna soma hapa ahadi za Mungu kuhusu jinsi atakavyo tubariki ikiwa tuna towa chakumi. Mungu ni mwaminifu na ana uwezo wa kuzidisha mali yetu, hata ikiwa tuna sehemu kidogo pekee.

Soma kwa sauti: Nehemia 13:12

Kutowa chakumi si kitu ufanyacho wakati unapotaka ama unapo jisikia kutowa. Kutowa chakumi ni kitu kinachofanyika kila mara, wakati wowote unapopokea mafanikio ya vitu ama pesa, kwa mfano upokeapo pesa baada ya kumaliza kazi uliyo kuwa ukifanya, ama wakati unapovuna mimeya yako.

Ni vizuri kuelewa kwamba chakumi si chetu. Chakumi ni kitu cha Mungu; ni sehemu iliyo ya Mungu.

Soma kwa sauti: Mambo ya Walawi 27:30 na 32

Watu wa Mungu wali amurishwa kutowa moja ya kumu, ama chakumi cha uzao wa shamba na mifugo (pia Kutoka 23:19 na Kumbukumbu 14:2). Waaminio wanaendelea kutowa chakumi hadi leo, watowa chakumi kwa mafanikio yao yote.

(Mchungaji/Mwalimu: utowe maelezo ya chakumi kwa kutumia mfano ambao kila mmoja ataaewa. Chakumi ni moja ya kumi. Tafuta mfano ambao ni mwepesi kwa kuelewa maana ya kutowa chakumi.)

Chakumi cha Endelesha Kazi ya Mungu

Sababu ya tatu ya kutowa chakumi ni kwa sababu chakumi cha msaidia mchungaji/kiongozi (wale wasiokuwa na kazi nyingine isipokuwa kazi ya kanisa pekee) na jamaa zao. Chakumi chako cha saidia pia kazi ya kanisa ili iendelee katika jamii na kusaidia katika umisheni.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 9:13-14

Chakumi cha watu wa Mungu chapewa ili kuwasaidia wale wafundishao Neno la Mungu na wale wafanyao kazi ya Mungu. Ni mpango wa Mungu ili wachungaji na wale wafanyao kazi ya Mungu pasipo kuwa na kazi ingine yoyote wasaidiwe kupitia chakumi. Kutowa chakumi ni shurti, chakumi si kitu tukitoacho wakati tunapotaka, tunatowa kwa sababu hiyo ni mapashwa.

(Mchungaji/Mwalimu: Ikiwa una mda, ama kwa ajili ya majifunzo yako ya kipekee, maandiko yafuatayo yazungumuzia kuhusu wachungaji na watumishi watumiyao mda wao wote kwa kazi ya Mungu: 1Wakorinto 9:11; 1Timoteo 5:17-18; na 1Wakorinto 9:7-11.)

Hatari ya Kutokutowa Chakumi

Soma kwa sauti: Malaki 3:8-12

Maandiko haya ni maneno ya Mungu mwenyewe! Mkristo ajuaye kwamba anapashwa kutowa chakumi lakini hatowi, huyo anajiletea laana mwenyewe. Biblia yasema katika maandiko haya kwamba yule asiyé towa chakumi ni ***mwizi***; mtu huyu hamuiibi mtu bali aiba Mungu!

Kutowa chakumi yaweza kuleta mabadiliko katika kazi zisizo tembea vizuri. Mahali ambapo wakristo hawatowi chakumi, mchungaji ama

mtumishi wao hatakuwa na uwezo wa kujibu mahitaji yake msingi na ya jamaa lake. Kanisa halitaweza kujibu kwa mahitaji yayo, kwa mfano kulipa malipo ya kupanga nyumba, kuwasaidia wasio jiweza, kujibu mahitaji ya ofisini, kulipia mchungaji nauli ya safari, na mawasiliano,... Mahitaji haya yanapashwa kipata jibu kuitia waamini kutowa chakumi. Kutowa chakumi ni wajibu wa kila mkristo. Kutokuheshimu agizo hili latukanisha jina la Yesu.

Katika inchi zimoja, dini ya kikristo yajulikana kama vile “dini ya umaskini” kwa sababu wakristo hawatowi chakumi kwa sababu ya hiyo mibaraka ni kidogo. Katika inchi zimoja zimoja hekalu za miungu zinapambwa na zahabu na feza—kwa sababu hata walio maskini watowa kwa utashi wao kwa miungu! Kwa nini sisi tumuaminio Mungu wa kweli tuisitende zaidi ya hayo kwa kutowa kwa kazi ya Mungu?

Jee, wataka kupokea mibaraka ya Mungu maishani mwako ama katika jamaa lako? Jee, wataka kumuona mchungaji wako na kanisa lako likifanya kazi nzuri katika jamii yako? Ikiwa unataka kuona hiyo inafanyika inakubidi uwe mwaminifu kwa kutowa chakumi.

Ni Wapi Utowapo Chakumi Chako?

Biblia yatufundisha kwamba tupeleke chakumi chetu katika “nyumba ya Mungu” (Malaki 3:10). Maana ya hiyi ni kwamba tunapeleka chakumi chetu kwa kanisa letu, mahali ambapo tunapokea mafundisho na usaidizi. Kila aaminiye atapeleka chakumi chake ndani ya kanisa lake (ama huduma), pasipo kujali udogo wa chakumi utakayo itowa, ili Mungu abariki watu kanisani inabidi waanze kutowa chakumi chao.

Mchungaji/Kiongozi, uliza maswali haya:

“Jee, umewai kusikia mahali ambapo mchungaji ameacha kanisa kwa sababu ya kukosa usaidizi ki maisha kwa ajili yake na jamaa lake? Jibu la Mungu kwa hiyo ni nini?” (Watu wanapashwa kuanza kutowa chakumi. Jinsi Mungu awabariki katika mafanikio, usaidizi na utajiri wa watu na kanisa vitaongezeka.)

Woga wa Kutowa Chakumi na Sadaka

Moja kati ya sababu ifanyao kanisa lisiwe nzuri, lisiwe kanisa linalo komaa ni kwa sababu watu hawatowi chakumi. Chakumi ni ahadi ya Mungu kwa ajili ya kuwabariki waaminio wote, bali wengi hawatowi chakumi kwa kufikiria kwamba hawatapata chakula cha kutosha ama hawata weza kujibu kwa mahitaji ya jamaa zao. Waishi katika woga kwa sababu ya yale walio jifunza kuitia maisha yao.

Waaminio watakao anza kutowa chakumi wataanza kuona mibaraka ya Mungu, na kuona Mungu akiwasaidia. Ikiwa utataka kuendelea kuona mibaraka na kukomaa, unapashwa kutowa chakumi. Umutwike Mungu woga wako. Atakuondolea woga huo; na atakuweka huru kwa kuondoa woga ukiomba na kumutumainia siku baada ya siku. Tuwe na uhakika kwamba tunapo mtii Mungu atatushugulikia kwa njia iliyo nzuri ziaidi na inayofaa.

Woga unapingana na imani. Biblia inasema, “*pasipo imani ni vigumu kumpendeza Mungu*” (Waebrania 11:6) pia “*twaenenda kwa imani, si kwa kuona*” (2 Wakorinto 5:7). Mungu anakupatia zawadi kwa ajili ya imani yako, maana ya hiyo, umuoneshe imani yako kwake kwa kumtolea chakumi chako na kungojea akubariki.

Uanzapo kutowa chakumi unaweza kupimwa, bali baadaye utaona matokeo ya mibaraka ya Mungu. Kwa kuitia hiyo utawapa watu wengine moyo wa kuanza kutowa chakumi.

Kuhusu Sadaka

Sadaka ni zawadi ya pesa ama vitu, itolewayo wakati usaidiyapo mtu ama umutumikiyapo mtu kazi fulani pasipo kutarajia kulipiwa bali wapokea zawadi. Kwa maneno mengine watowa sehemu ya mda wako, pesa zako, ama vitu vyako ama kazi yako kama vile zawadi kwa kazi ya Mungu. Sadaka siyo chakumi—sadaka yatolewa kwa utashi wa mtu, pia hutolewa **baada ya** kutowa chakumi. Sadaka si kitu ambacho tunacho shurutishwa kutowa kama vile chakumi, bali ni chaguo ambalo tulifanyalo pasipo kushurutishwa; waamuwa mwenyewe ni nini utakayo itowa, unachukuwa uamzi mwenyewe kuhusu kile utakacho kitowa. Sadaka ni zawadi itolewayo kwa ajili ya kusaidia, kujibu kwa hitaji fulani, kusaidia kwa kazi ya Mungu, ama kwa sababu unataka kumushukuru Mungu.

Biblia yatupatia moyo kutowa sadaka kwa sababu hii ni njia nzuri kwa ajili ya kujibu mahitaji, na kwa kutowa tuna barikiwa pia na Mungu.

Soma kwa sauti: Luka 6:38

Mungu hurudisha kila mara mibaraka tutowapo kwa moyo mwema. Kumbuka kwamba mibaraka Mungu atakayo kubariki nayo yaweza kuwa tofauti ni ile unayo itarajia. Mungu wetu ni mwema na atakurudishia mambo mazuri unayo yahitaji ikiwa tunawatoleya wengine!

Kutowa kwa Moyo Mwema

Soma kwa sauti: 2 Wakorinto 9:6-7

Mungu anampenda mtu atowaye kwa furaha na kwa moyo mwema! Kutowa ni uamzi wako, unatowa kile ukusudiacho moyoni. Mungu atakulipa kwa uwingi, bali kwa kutowa yakubidi uwe na moyo mwema wa kutaka kumubariki mwengine. Hatupashwi kutowa kwa sababu tuna tafuta kupokeya vitu vingi kutoka kwa Mungu.

Unapo towa, mibaraka inakujia, kwa mfano huo wa uhakika mtu anao apandapo mbegu, mbegu hiyo itatowa mmea utakaotowa matunda baadaye.

Tuna towa sadaka Kama Vile Tendo la Kuabudu

Watu wa Mungu walimtolea kila mara sadaka, na Biblia yajaa mifano mingi ya watu waliyo mpenda Mungu na waliomutolea sadaka ya pesa na vitu. Mfalme Daudi anasema, “*sita mtolea Bwana, Mungu wangu, sadaka za kuteketezwa nisizozigaramia.*” (2 Samueli 24:24).

Watu wa Mungu walimutoleya sadaka za wanyama na mazao ya mashamba (Mwanzo 4:3; Mambo ya Walawi 4:2). Ibrahimu alimutoleya Mungu, na wafalme pia, hata manabii na watu wote wa Mungu walimtolea pia. Tunaweza kumtolea Mungu sadaka itokayo kwa pesa zetu ama kutoka kwa chochote ambacho ni chetu. Sadaka siyo ushuru, ama kitu kinacho shurutishwa, bali ni kutowa zawadi kwa Mungu kwa moyo wa upendo.

Tuna Towa Sadaka Kama vile Shukurani kwa Mungu

Baada ya kuokolewa na garika Nuhu alimtolea Mungu sadaka (Mwanzo 8:20). Sisi pia tuna weza kumutolea Mungu sadaka kwa ajili ya kumushukuru.

Soma kwa sauti: Luka 21:1-4

Yesu alimusifu mjane huyu kwa kutoa zaidi kuliko watu wote kwa sababu alitowa yote aliyokuwa nayo. Hii ni mfano wa kutowa kwa moyo mwema kwa ajili ya kazi ya Bwana. Mungu abariki namna hiyi ya kutowa. Si kiwango kikubwa cha pesa utowacho ndicho kiletacho mibaraka, bali kinacho hesabiwa ni huo upendo na shukurani unaokuwa nao utonapo towa sakaka yako.

Tunatowa Sadaka ili Isaidia Kazi ya Mungu Kuendelea Mbele

Soma kwa sauti: Wafilipi 4:16-17

Mtume Paulo anaandikia kanisa kwa kuwashukuru kwa ajili ya sadaka walioituma ili imsaidie katika huduma.

Sadaka yaweza kutolewa kwa ajili ya kujenga kanisa, ama kwa ajili ya kutunza jengo la kukusanyikiya. Wakati mwengine mchungaji anaweza kuhitaji kulipa nyumba ya kupanga, na pia kuna garama zingine kwa kutunza majengo ya kanisa, hata garama zingine kama vile usafiri, mawasiliano ya simu na ya posta, hata kununua vitabu na vinginevyo.

Soma kwa sauti: Ezekiel 44:30

Watu walitowa chakumi na sadaka yao kwa ajili ya kujenga na kutunza hekalu. Wakati wowote tunapo towa sadaka ya kutunza jengo la kukusanyikia ama kwa ajili ya kazi ya kanisa, tuna mutoleya Mungu.

Tunatowa Sadaka kwa Kuwasaidia Wengine

Mahali tunapo kaa, katika jamaa na jamii zetu, ndani ya kanisa, na ulimwenguni tunamoishi kuna mahitaji. Labda sehemu fulani kuna watu wanao tesaka kwa sababu ya njaa, magonjwa, ama vita. Wakristo wanaweza kutuma zawadi kwa ajili ya kuwasaidia watu hao. Mara sadaka zaweza kukusanya ili kuwasaidiya hawa ndugu na dada katika Kristo. Kuna mda mwengine sadaka zakusanya ili zipate kusaidiya katika kazi za kutangaza Injili ama umisheni, ama kwa ajili ya kazi zingine za kanisa.

Soma kwa sauti: 2 Wakorinto 8:1-5

Katika andiko hili Kiongozi wa kanisa (Paulo) alikusanya sadaka kutoka makanisa mbalimbali kwa kulisaidia kanisa la Yudea, ambalo likiteswa na njaa. Paulo aliwapa moyo wakristo ili watowe kwa moyo wa ukarimu ili wote watowe na kanisa la Yudea libarikiwe na Mungu.

Ahadi Zingine kwa Wale Watowao

Tuna juwa kwamba Mungu atowa ahadi ya kuwazidishiya mapato wale watowao. Biblia yatufundisha pia kwamba utowapo wajivekea hazina mbinguni. (Matayo 6:20 na 1Timoteo 6:18-19).

Mambo ya Kutazama Wakati Tunawapo Sadaka

Kabla ya kutowa, haya ni mambo ambayo utahitaji kuyafikiria:

1. Ni kitu gani ambacho moyo wako wataka kutowa?

2. Uliza Mungu ikiwa anataka utowe. Baadaye uliza ni kitu gani anataka utowe. Baadaye umuulize kwa nini anataka utowe. Utowe kufuatana na yale uliyo nayo.

3. Towa kwa moyo wa furaha. Usitowe ikiwa moyo wako wajaa chuki ama woga. Ombo ili Mungu abadilishe moyo wako ili utowe kwa furaha.

4. Kusiwe mtu atakaye kushurutisha kutowa, kwa kuwa huyo atahukumiwa na Mungu ikiwa anafanya hivyo. Ombo Roho Mtakatifu azungumuze na miyo ya watu wako kwa ajili ya kutowa.

Somo kwa ufupi:

Chakumi cha tolewa ndani ya kanisa tunamo fundishwa na kulelewa, tunaleta humo chakumi cha yale tunayo yapata. Chakumi ni agizo la Mungu, si kitu tunacho amuwa kutowa sisi wenyewe. Mchungaji anaye pokeya sehemu ya chakumi naye pia anapashwa kutowa chakumi.

Chakumi ni moja wapo wa njia Mungu aitumiayo kwa kujenga ufalme wake duniani. Ni moja wapo wa njia aitumiayo kwa kuwashugulikiya wachungaji, kulijenga kanisa, na kujibu kwa mahitaji mengine ya kanisa.

Chakumi ni alama ya shukurani zetu mbele ya Mungu. Mungu awabariki wale watowao chakumi. Kila mara tunapashwa kutowa kwa shabaa nzuri tukiwa na moyo wa shukurani.

Sadaka zasaidia kujibu kwa mahitaji ya kanisa na kuwasaidia wale walio katika mateso. Kutowa sadaka kwa ajili ya umisheni yapanua ufalme wa Mungu zaidi na kanisa letu la mahali.

Kutowa chakumi na sadaka ni mojawapo wa njia Mungu atumiyazo ili ajibu mahitaji ya watu wake. Tutowapo kwa ukarimu mbele za Mungu tunapokea kwa ukarimu pia kutoka kwa Mungu.

Maswali:

1. Kwa nini tutowe chakumi kwenye nyumba ya Mungu? (Chakumi cha wasaidia watumishi wa Mungu, cha saidia pia kwa mahitaji ya kanisa la mahali.)

2. Mwenye chakumi ni nani? (Chakumi ni cha Mungu. Moja ya kumi ya faida yako yote ni ya Mungu, siyo yako.)

3. Eleza sababu zimoja zimoja ambazo za sababisha tutowe chakumi? (Kusaidia kazi ya kanisa ama kusaidia wale wanaofanya kazi kanisani, kutowa msaada kwa ajili ya mahitaji ya watu, kuonesha upendo tulio nao kwa ajili ya Mungu na kumshukuru, kusaidia kazi za umisheni, na kazalika.)

4. Mungu ana ahidia kufanya nini tunapo towa? (Luka 6:38: Tunapotowa chakumi na sadaka, Mungu pia atubariki)



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi lako kujifunza na kuweka kwa ufahamu andiko hili:

Mezali 3:9-10

"Mheshimu Bwana kwa mali yako, na malimbuko yako yote; ndipo gala zako zitajazwa kwa wingi, na mashinikizo yako yatajazwa divai mpya."

Somo la 18

Umoja wa Kikristo

Jamaa yenyе nguvu, kanisa lenye nguvu, na jamii yenyе nguvu inajengwa juu ya msingi wa **umoja** kati ya watu wao. Mambo makubwa, amani na mafanikio yanapatikana pekee kati ya wale wanao taka kufanya kazi pasipo mapigano, wale waikumbatiyao amani na kutaka kuishi kwa umoja. Jamii na jamaa watafutao amani kwa bidii walijifunza namna ya kutatua mizozo kwa njia inayofaa.

Mateso yaonekanayo ulimwenguni leo yajinua wakati watu wazara u moja ama wanapo ona kuwa umoja hauna faida yoyote. Umoja ni wa muhimu kwa ajili ya kujenga amani na maendeleo ya jamaa, ya kanisa, na hata ya taifa lote pia.

Mhubiri 4:9-12 anasema "*Afazali kuwa wawili kuliko mmoja; Maana wapata ijara njema kwa kazi yao. Kwa maana wakianguka mmoja wao atamwinua mwenzake; lakini ole wake aliye peke yake aangukapo, wala hana mwengine wa kumwinua. Tena wawili wakilala pamoja, hapo watapata moto; lakini mmoja aliye peke yake tuu awezaje kuona moto? Hata mtu ataweza kumshinda yule aliye peke yake, wawili watampinga; wala kamba ya nyuzi tatu haikatiki upesi.*" Tuunganapo kwa shabaa ya tumutumikia Mungu kuna mengi ambayo yanaweza kutendeka. Tuoneshapo umoja kila mmoja apokea faida kuititia ushirika huo.

Ni Nini Illetayo Matengano?

Katika Matayo 12:25 Yesu anasema "*kila ufalme ukifitinika juu na nafsi yake, hufanyika ukiwa; tena mji au nyumba yoyote ikifitinika juu ya nafsi yake; haita simamama.*" Tuangaliye vita na mafarakano yaliyomo ulimwenguni leo. Maeneo mengi na mataifa mengi yako katika hali ya vita na mikokotano. Katika ufalme kukizuka mapigano na watu wa taifa moja washindwe kuelewana na kuanza kupigane wao kwa wao. Ufalme unao jigawanya na taifa lanalo jigawanya wao kwa wao watashindwa. Kukiwa matengano ndani ya jamaa mambo mabaya mengi yanajitokeza. Ikiwa tutataka kuona kanisa likikomaa, amani na mafanikio katika taifa letu, kanisa, na maishani mwetu, tunahitaji kujifunza; ni nini Neno la Mungu latufundisha kuhusu hitaji la **upendo, amani na umoja**.

Soma kwa sauti: Yakobo 3:14-18

Matengano huonekana mahali ambapo mipango ya kipekee ama mahitaji ya kipekee yageuka kuwa ya muhimu sana kuliko mahitaji ya kundi lote. Matengano yaonekana mahali mtu asikiya kuwa ana chukiliwa ama anazarauliwa, ama kubaguliwa. Yesu anasema kwamba amri kubwa ya Mungu ni **kumpenda Mungu na kumpenda jirani yako** (Matayo 22:37-39). Ikiwa tuna peana samani sisi kwa sisi kama vile Mungu ana tupatia samani, hiyo itatuongoza kupendana na kusaidiana kwa amani. Hiyo itafanya pia tuwatakiye marafiki wetu mazuri, jamaa, kanisa, na hata majirani nao.

Ili tuwe na amani, kila mtu anahitaji kufikiri na kutenda kwa unyenyekevu, pasipo kufikiri kwamba sisi ni bora zaidi kuliko wengine. Katika Agano Jipya maandiko mengi yatuomba kuishi katika unyenyekevu

Yesu Aomba kwa Ajili ya Umoja

Kabla Yesu ashikwe na kusulubiwa, aliwaombea wanafunzi wake na kuwaombea pia watu watakao kuja baadaye, ambao watakao muamini (hata na wewe pia uko mwanafunzi wa Yesu siku ya leo). Yesu alitaka wanafunzi wake wawe na umoja. Yesu alielewa kwamba umoja ndani ya kundi la waninio ni jambo la maana sana ili ulimwengu uongozwe kwa kumuamini Yeye kama vile Bwana na Mwokozi.

Katika Yohana 17:21-23 Yesu alimuomba Baba yake, kwa maneno yafuatayo, “*wote wawe na umoja; kama wewe, Baba ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki kwamba ni wewe ndiwe uliyete nituma. Nami utukufu ule ulio nipa nawapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa wewe ndiwe ulinituma, ukawapenda wao kama ulivyo nipenda mimi.*”

Ikiwa Yesu anaona kuwa umoja ni wa maana, kwa nini sisi tusione hivyo?

Umoja Ndani ya Kanisa

Mapigano na matengano ndani ya mwili wa Kristo (kanisa) inapatia kanisa jina mbaya sana ndani ya jamii na kuwachanganya akili za wanao amini. Mafarakano kanisani yanaweza kuwazuwia watu wasimuamini Yesu kama vile mwokozi kwa sababu wanaona kanisa kama vile nafasi ya matengano, mizozo na vurugu.

Soma kwa sauti: Yohana 13:34-35 na Waefeso 4:3

Ikiwa sisi kama vile mwili wa Kristo tunataka kuwfikia kwa injili wale walio potea mahali tunapo ishi tunahitaji kufanya bidii ili kuwe umoja kati ya wale waaminio. Tusimpatie Shetani nafasi ya kuleta matengano kati yetu.

Biblia yatuelezea kwamba Mungu ana mpatia kila mtu samani na kila mmoja yuko sawa sawa na mwengine. Mungu anataka kila mmoja wetu aokoke; kwa ajili ya hiyo kusiwe mtu kati yetu atakaye fikiri kuwa yeye ni bora zaidi ya wengine katika mwili wa Kristo. Tunapo ishi tukifanya kazi kwa umoja, watu wanajisikia kuwa wameungana pamoja na kwa umoja. Kwa njia hiyo, kanisa litaonekana lenye kuzaa matunda likiwafikia watu waishio pamoja nasi.

Ni huzuni kubwa, kuona kwamba mafarakano kanisani yana anzia kwa viongozi na baadaye yaingia kati ya wanamemba wa kanisa. Wachungaji, wazee, mashemasi, na viongozi wa makundi mbali mbali wanapashwa kuonesha mfano mzuri wa unyenyekevu na umoja, kufanya kazi kwa umoja ili wafikiye maono ambayo Mungu aliyo ipatia kanisa la mahali. Wanamemba wote zaidi viongozi, wanapashwa acha faida na mipango za ubinafsi kwa ajili ya faida ya kanisa lote kwa jumla. Wachungaji na wazee wawe mfano wa amani, wakitafuta amani na kujenga umoja katika mwili wa Kristo.

Agizo kwa Wakristo Kanisani

Soma kwa sauti: Wagalatia 5:14-26

Ili kuwepo umoja kanisani, Yesu alitupatiya amri ambayo tunapashwa kuheshimu. Ni vigumu sana kwa yule asiye mfahamu Yesu kuheshimu

maagizo ya Mungu; bali tumpokeapo Kristo, tunapokea Roho wa Mungu, atusaidiaye kumheshimu Mungu. Tunapokea nguvu za Kristo ndani yetu, zitusaidiazo kumtii Mungu. Tunapokea nguvu za Yesu zibadilishazo namna yetu ya kufikiri na kutenda. Tuna uwezo wa kumtii Mungu ikiwa tuna chagua hiyo.

Mchungaji/Kiongozi, soma maandiko haya na baadaye uombe kundi kujibu maswali haya:

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 1:10-13

Maandiko haya yatuelezea nini kuhusu umoja?

Soma kwa sauti: 1 Yohana 3:14-18

Ni namna gani tunaweza kuonesha kimatendo umoja wetu kwa wenzetu wakristo?

Soma kwa sauti: Waefeso 4:1-2

Maandiko haya yana waelezea nini? Maana ya kuvumiliana ni nini?

Soma kwa sauti: Wafilipi 2:2-5

Utatii namna gani yale ambayo Biblia yasema katika maandiko haya?

Soma kwa sauti: 1 Petro 3:8-9

Ili ulete umoja ndani ya jamaa lako ama kanisa lako utafanya nini?

Kutatua Mizozo

Soma kwa sauti: Mwanzo 13:5-17

Mchungaji/Kiongozi, uliza: “*ni nini Ibrahimu alifanya ili atatuwe mzozo uliyo kuweko kati ya watumishi wake na watumishi wa ndugu yake, Lutu?*”

Haya yafuatayo ni majibu mamoja mamoja:

1. Ibrahimu hakuzarau shida hiyo. Hakuzungumzia wengine kuhusu shida hiyo. Alienda moja kwa moja hadi kwa Lutu na kuzungumza naye.
2. Ibrahimu hakutumia maneno ya hasira, bali maneno ya Amani.
3. Ibrahimu alitafuta makubaliyano kwa ajili ya sehemu zote mbili.
4. Ibrahimu hakugangania haki yake ama kutazama ukubwa wake ama heshima kubwa ambayo aliyo stahili kupewa kwa sababu ya ukubwa wake.
5. Ibrahimu alikuwa mwaminifu na alimtumainia Mungu. Akamruhusu huyu kijana mdogo kuchaguwa kwa sababu ya imani aliyo kuwa nayo kwa Mungu, haku aminiya kazi ya mwanadamu ama mawazo yake. Kwa sababu ya yale Ibrahimu aliyo yafanya, Mungu alimubariki.

Kwa kuwa katika Biblia kuna mafundisho mengi yatufundishayo kuishi mmoja na wengine kwa amani, tuwe tayari kusikiliza na kumtii Mungu!

Umoja Katika Utofauti

Kanisa ni mwili wa Kristo Yesu Mwenyewe akiwa ndiye kichwa.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 12:12-27

Biblia yatowa maelezo kuhusu kanisa ikilifananisha na mwili wa mtu. Mwili wa Kristo unaundwa na viungo vingi kila kiungo kikiwa tofauti na vingine na cha kipekee, kwa jumla vyauunda mwili mmoja. Mwili wahitaji

viungo vyake vyote kwa jumla ili ueneye na utumike vizuri. Hakuna sehemu yoyote ile iliyo na samani ndogo kuliko ingine. 1Wakorinto 12:27 yasema "*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila mmoja peke yake.*" Neno la Mungu latueleza kwamba kila mmoja katika kanisa ana samani sawa na wenzake, na kila mmoja anahitajika katika mwili wa Kristo, kanisani.

Kazi ya Karama Katika Kanisa

Kristo aliwaita watu wamoja kufanya kazi ya aina fulani katika uongozi wa kanisa.

Soma kwa sauti: 1 Wakorinto 12:28-31

Andiko hili lawataja watu ambao wamepewa kazi na majukumu ndani ya kanisa. Yesu, kichwa cha kanisa, aliwapatia wanamemba mbalimbali karama za kiroho ndani ya kanisa---ili mwili wa Kristo kwa ujumla upewe moyo na kujengwa kiroho.

Soma kuhusu karama hizi ambazo Mungu amezipatia kanisa.

1 Wakorinto 12:7-12 na Warumi 12: 4-8

Kama vile waaminio kila mmoja ana kazi na huduma ya kufanya kanisani. Mungu amempatia kila mmoja wetu karama kwa njia ya kipekee. Karama zetu zahitaji kutumiwa ili kulijenga kanisa na kulitia nguvu katika jamii. Karama hizi si zetu, ni karama za Mungu. Ijapokuwa si zetu, twazitumia ili tumtumikie Bwana kwa kutumia yale aliyoyaweka ndani yetu kwa ajili ya ubora wa kanisa lote.

Kila mmoja wetu ana alikwa kuonesha picha ya Yesu Kristo kwa watu watuzungukao, sisi tukiwa kila mmoja kiungo cha mwili wake. Kwa hiyo, ni jambo la mhimu sana tuwe kwa umoja kila mtu na mwanzake, ili tuepuke kuweka uzaifu mwili wa Kristo kwa jumla.

Matokeo ya Umoja

1. Umoja waleta kukomaa na nguvu ndani ya kanisa.

Soma kwa sauti: Waefeso 4:14-16; Matendo 2:43-47; na Matayo 12:25

2. Umoja waleta kunia mamoja na upendo katika mwili wa Kristo.

Soma kwa sauti: Yohana 17:21-23 na Yohana 13:34-35

3. Umoja unaleta mibaraka.

Soma kwa sauti: Zaburi 133:1-3

4. Umoja kati ya wakristo haumupatiyi Shetani nafasi kuingia na kufanya kazi.

Soma kwa sauti: 2 Wakorinto 2:10-11

Maswali:

1. Matengano yamekutesa namna gani wewe, yametesa jamaa lako namna gani, kanisa lako, na jamii yako?
2. Kwa kuyatazama yale uliyo jifunza, utafanyaje ili ulete suluhisho kwa matatizo hayo?
3. Angalia karama unajisikia kuwa umepewa na Mungu. Karama hizo wazitumiaje katika mwili wa Kristo?

Mchungaji/Kiongozi: Baada ya kufikiria maswali haya, uwaongoze watu katika njia ya kuwapatanisha, ikifuatana na maombi.



Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi kujifunza kwa maandiko haya na kuyaweka kwa ufahamu:

Wafilipi 2:2

“ijazeni furaha yangu, ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja, wenye roho mmoja, mkinia mamoja.”

Somo la 19

Garama ya Kumfuata Yesu

Kuwa mfuasi wa Yesu ina maana kubwa tofauti na kujifunza mambo yanayo mhusu Yesu. Kuwa mfuasi ina maanisha kumfuata Yesu. Mara nyingi si vyepesi kumfuata Yesu kwa sababu ya misukumo ya maisha na misukumo ya ulimwengu utuzungukao. Kuna mambo mengi ambayo yanaturudisha nyuma ili tusimfuate Yesu, Shetani naye anatumia ujanja mwingi ili atuzuwiye kumfuata Yesu. Ndugu na dada zetu katika historia ya ukristo waliteswa kwa sababu waliamua kumfuata Yesu na kuwatangazia wengine habari njema.

Tunapo amuwa kumfuata Yesu, maisha hayatakuwa mepesi kwetu kila mara. Watu wa ulimwengu huu watajaribu kutusukuma ili tuwe na tabia kama zao. Tunapokataa kuwafanana wanatuchekelewa ama wanatutesa. Kuna hatari ya kutaka kuwa kama wao, kwa sababu watatupeleka katika njia zao mbaya na kutuzuwia kumfuata Yesu.

Katika inchi nyingi za waisilamu, ikiwa Muisilamu mmoja ana amini Yesu hapo hapo huyo anakataliwa na jamaa lake, na jamii yake pia. Wakati mwengine hawa waamini wapya wana azibiwa ama wanafungwa magerezani, wanafikia hata wakati mwengine kuuwawa. Katika inchi zimoja, wakristo wanafungwa kwa sababu wanakuwa na Biblia; wengine wame uwawa kwa sababu ya kuamini Yesu Kristo. Mishonari wamefungwa hata wengine kuuwawa sababu ya kutangaza habari njema. Kuna jeuri ifanyikayo na wale waupingao ukristo na mateso yaendelea hadi sasa katika inchi nyingi ulimwenguni, zaidi katika inchi zile zinazokuwa chini ya utawala wa kiisilamu. Ni vizuri tuelewe kwamba kila mmoja katika maisha yetu atafurahi kwa sababu amemupokea Yesu, ni vizuri tuelewa pia kwamba kuna garama ya kuwa mfuasi wa Yesu.

Yesu alitujulisha kwamba mateso ya aina hii yatatufikia na kutusumbua:

Soma kwa Sauti: Matayo 24:9 na Yohana 16:2

Yesu anatuelezea kwamba si kila mtu atakaye kuwa na raha kwa sababu amemfuata Yeye, tuelewe kwamba kuna aina mbalimbali za mateso ambayo yaweza kutokeya.

Soma kwa Sauti: Matayo 5:10-11

Kwa sababu aina zimoja, za mateso zatoka katika jamaa; aina zingine za mateso zinatoka katika jamii tunamo ishi, ama sehemu ambazo tunafanya kazi. Mateso mengine ya wakristo, yanaweza kutokea kwa viongozi walio madarakani ama serekalini. Kumbuka kwamba yule muovu, Shetani, anawatumia watu ama matokeo ya aina tofauti kwa kuleta vurugu kwa wale waaminio Yesu Kristo.

Soma kwa Sauti: Waefeso 6:10-13

Tuelewe kwamba adui wetu ni Shetani, bali si watu ambao wanatutesa. Tunahitaji kufanya vita kwa maombi ili tuvishinde vita hivyo tunahitaji kutumia hekima wakati mateso yanapotujia.

Ulimwengu na Tabia zake Hazipatani na Ufalme wa Mungu

Ulimwengu na njia zake zote zimeharibika leo hii. Unaweza kuteswa kwa sababu umekataa kuijunga na maovu. Unavyo viona kwamba ni vya maana ama vya samani kama vile mkristo havitafurahisha wengi kwa sababu maisha unayo yaishi haya ambatani na vitu wanavyo ona kuwa ni vya samani, ama na vitu wanavyo visifu. Kwa mfano wakati unapopinga rushwa kazini, wafanya kazi wenzako watakuona kama vile wewe niadui wao; ikiwa bwana wa kazi ni mtu achukwaye rushwa utateswa hata kufikia kufukuzwa kazini.

Ikiwa wewe ni mfanya siasa na unafanya kazi kwa kuwasaidiya watu, wana siasa wenzako wanaweza kukuchukia na kukutazama kama vile adui pia, ama kukuona kama vile kitisho kwa mipango yao isiyo ya haki.

Katika inchi nyingi ulimwenguni vyombo vya sheria, sekta mbalimbali za kuheshimisha sheria, na vitengo mbalimbali vya serekali vimetawaliwa na rushwa, kunaonekana uchukuaji na utowaji wa rushwa kwa ngazi zote. Kwa mahakama mamoja mamoja rushwa hufanya walio na haki wahukumiwe na wasio na haki waachwe huru. Ulimwengu wa leo unatawaliwa sana na rushwa na watendao haki wanachukiliwa kabisa.

Soma kwa Sauti: 1 Yohana 5:19

Andiko hili linatuonesha kwamba watu wasio mjua Kristo wako chini ya mamlaka ya Shetani na wamefungwa chini ya uwezo wa zambi. Uovu mwingi ulimwenguni unatokana na hiyo.

Soma kwa Sauti: 2 Wakorinto 4:4

Watu wanatutesa kwa sababu wamefungwa macho na Shetani ili wasione ukweli, adui wetu wa kweli ni shetani. Maombi yako yana nguvu ya kuweka huru mafikiri ya watu ili yasiendelee kutawaliwa na nguvu za giza.

Uwe Tayari Kulipa Garama

Unapo amua kumfuata Yesu utapata shida nyingi. Kuna garama ambayo utahitaji kulipa kwa sababu ya imani yako kwa Kristo. Uamuzi wako wa kumfuata Yesu unaweza kusababisha upoteze kazi yako; sehemu zimoja ulimwenguni inawezekana hata kufungwa, wala kufukuzwa nyumbani ama kufukuzwa katika inchi, inawezekana hata kuuwawa. Hiyo ilifanyika kwa wanafunzi wa Yesu na kwa wakristo wengi katika historia ya kanisa, hata kwa sasa mambo kama hayo yanaendelea kutendeka. Wakati shida zitakapo wafikia wakristo, kuna wale ambao watakao mkana Yesu, kama Petro alivyofanya.

Soma kwa Sauti: Luka 9:62

Kuna watu ambao wanao acha kumfuata Yesu kwa sababu ya shida. Haiwezekani kumfuata Yesu ukiambatana na tabia za kidunia. Usipatie nafasi mambo mengine yatakayo kuzuviya kumfuata Yesu kila siku. Yesu anasema watu wanao tazama nyuma hawastahili kuingia katika ufalme wake. Jee, utarudi nyuma usimfuate Yesu kwa sababu ya shida?

Yesu Alilipa Garama Kubwa Kwa Ajili Yetu

Yesu alilipa garama kubwa kwa kujitowa afe ili tupate kuokoka sisi. Yohana 3:16 inasema: ‘*kwa maana jinsi Mungu alivyoupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipote, bali awe*

na uzima wa milele." Yesu alipokuwa akitundikwa msalabani alifikiri kuhususisi, hakujifikiria yeye mwenyewe.

Soma kwa sauti: Waembrania 12:2

Kwa kuja ulimwenguni Yesu aliachaa utukufu aliokuwa nao huko mbinguni. Akakubali kuja kuishi nasi hapa duniani, ili awe kama sisi na kuteswa jinsi tunavyo teseka. Alipata njaa, kiu, majaribu, na mateso kama jinsi tunavyo teseka. Ijapo ni Mungu alikubali kugeuka damu na nyama ili tupate kuokolewa (Wafilipi 2:6-8).

Yesu alilipa garama kubwa sana: kwanza alizaliwa katika hori la ngombe katika mazingira mlimo jaa wanyama na uchafu. Yesu aliishi bila nyumba, siku baada ya siku alikuwa akihubiri na kusafiri kila mara mchana mzima. Jioni alikuwa akijitenga kwenda nafasi ya ukimya ili aombe. Hakuwa na mke ama jamaa. Alikuwa msimamizi wa watu wote walio mfuata. Hakuwa na utajiri wala mshahara ama cheo. Yesu aliwakubali watu walio mchukia na kutafuta hata kumuua. Hata wakuu wa dini walimchukia kwa sababu alikuwa mwana wa Mungu.

Mambo Haya Yaonesha Jinsi Yesu Aliteswa kwa Ajili Yetu:

- Yesu alikubali kufungwa na kushitakiwa, akapelekwa hadi mahakamani (Luka 22:63-71 na Luka 23:1-5).
- Yesu alichekelewa na kuzihakiwa msalabani (Matayo 27:39-42).
- Watu walisema kuwa amerukwa na akili na ana wazimu pia (Marko 3:21; Yohana 10:20).
- Wakubwa wa dini walisema ana mapepo (Yohana 10:20 na Matayo 9:34).
- Maeneo mamoja watu walimuomba Yesu awaondokee katika maeneo yao kwa sababu watu waliogopa nguvu zake na hawakusamini kazi yake. (Marko 5:13-17).
- Alishambuliwa na kufukuzwa katika mji alimo zaliwa (Luka 4:28-30). Wale walio mfahamu walimchekelea na walimzarau na kumtupilia (Matayo 13:54-58).
- Yesu aliachaa raha ya nyumbani kwao, akimuacha mama na ndugu zake ili aweze kutembea kila siku akifundisha. Kuna mara hata amelala nje, alikuwa katika hatari kwa sababu ya majambazi na wanyama wa mwituni (Luka 9:57-58).
- Jamaa lake halikumuamini (Yohana 7:5), na walimtzama kama vile hana akili timamu (Marko 3:21).
- Alikataliwa na watu ambao walio mjua vizuri (Marko 6:1-3).

Haya yote yalitendeka kwa Yesu! Tunao moyo wa shukura kwake!

Soma kwa sauti: Yohana 15:20

Yesu anatuelezea kwamba sisi, kama vile wakristo, tutatendewa mambo kama yale aliyo tendewa (Yohana 15:20), kwa kuwa ulimwengu unajaa na masumbuko. Tunapashwa kukubali hiyo ikiwa sisi ni wafuasi wa kweli wa Yesu Kristo.

Soma kwa sauti: Waembrania 12:1-4

Yesu alivumiliya mateso ya ajabu, alitundikwa msalabani na kupigwa misumari mikononi na miguuni, akavikwa taji ya miiba kichwani mwake.

Damu yake yote ikamwangika na baadaye akafa. Aliruhusu hiyo ifanyike kwa sababu alikuwa akitufikiria kuhusu jinsi tutakuwa wake kupitia njia hiyo ya kusulubiwa.

Andiko hili la kitabu cha Waebrania latuelezea tuwe wenyewe uhodari katika Bwana, tukijua pia kwamba yawezekana kutesaka kwa sababu ya kumtumikia Yesu, lakini mateso yetu madogo sana tukiyalinganisha na mateso yale ambayo Yesu aliyo yapata msalabani.

Kuhesabu Garama ya Kumfuata Yesu

Ijapokuwa tunaweza kuteseka kwa ajili ya kusimama upande wa Yesu, tunapashwa kuendelea kuwa watu wa ukweli na kusimama upande wake na katika njia zake siku zote.

Soma kwa sauti: Matayo 10:21-23, 28 na Matayo 10:37-39

Kwa waamini wamoja waweza kufikia mda ambao jamaa zao zina kataa yale wayafanyayo kwa sababu hawaelewi. Wanaweza kujaribu kuturudisha nyuma ili tusimfuate Yesu. Wanaweza kujaribu katuondoa katika yale ambayo Mungu ametuita tuyafanye. Yesu anatuomba tuhesabu garama: itawezekana hata tutengane na jamaa zetu kwa mda kwa sababu ya Yesu; ama tunaweza kuvumilia hasira yao na msukumo kutoka kwao tukiishi pamoja nao.

Yesu Atufundisha Kubeba Msalaba

Yesu alichukua msalaba wake mwenyewe na akakubali kusulubiwa juu yao kwa ajili yako wewe na mimi. Anatuomba pia tuwe tayari kubeba msalaba wetu wa mateso na masumbuko ambayo yajayo kwa ajili ya kumfuata Yeye.

Soma kwa sauti: Luka 14:27

Mfuasi wa kweli atamfuata Yesu hata kukiwa magumu na mateso.

Soma kwa sauti: Marko 8:34-38

Yesu alisema kwamba kuna mambo ya maana kuliko maisha yetu ya sasa. Ikiwa tunamkana naye pia atatukana.

Soma kwa sauti: Matayo 10:38-39

Kuubeba msalaba maana yake ni kukubali kuteseka kwa ajili ya Yesu. Tusiweke maisha yetu kwenye mstari wa mbele bali tumuweke Yesu. Ikiwa kwa kupitia kutenda mabaya tunataka kuokowa maisha yetu, kwa mwisho, tutayapoteza.

Kumfuata Yesu ina maanisha kuwa uko tayari kuubeba msalaba wako siku baada ya siku (Matayo 16:24). Kuubeba msalaba si kitu chepesi; ni mateso kabisa. Hauta shangilia kwa kubeba msalaba, bali Yesu asema kwamba tunapashwa kuubeba msalaba kila siku, tuwe tayari kukataa kile ambacho tungeli kitaka maishani, bali tuchague utii na ufalme wa Mungu. Biblia inatupatia maandiko mengi yatupatiayo moyo kwa kutuonesha kuwa Mungu yuko pamoja nasi. (Zaburi 16:11 na zaburi 34:7-8). Ahadi hizi zatupatia tumaini na nguvu.

Ubaki Mkweli Kwa Yesu

Wakati upokeapo msukumo wa watu ama njia za ulimwengu, unaweza kujaribiwa ili umuache Yesu. Shetani anataka kukusukuma umkane Yesu, kama vile Petro alivyo mkana (Luka 22:54-57).

Soma kwa sauti: 1Petro 1:6-7

Mungu ana shabaa kwa kuruhusu mateso: inakufanya uwe mwenye nguvu na mkamilifu. Inawezekana uwe na furaha ya Kristo mda wa mateso.

Soma kwa sauti: Matayo 10:32-33 na 37

Ikiwa tuna mkana Yesu naye anasema pia kuwa atatukana. Yesu aelewa kwamba maisha ya ulimwenguni ni magumu na unapo amua kumfuata kutakuwa mda wa majoribu utakao hakikisha kuwa kweli unampenda Yesu. Ikiwa hausimami imara ndani ya Kristo unaweza kuiptoteza imani yako.

Ikiwa tunateswa na jamaa zetu, tunapashwa kuendelea kuwapenda na kuwa saidia, hata ikiwa wana hasira ama wanatutesa. Kumbuka kwamba, Yesu anataka aokowe wanamemba wa jamaa lako. Unaweza kuwaombea ukiamini kuwa Mungu anafanya kazi maishani mwao ili awalete mwenyewe kwake. Wakristo wengi waliotheswa na jamaa zao walipata furaha walipo ona wale jamaa zao zampokea Kristo.

Ahadi tulizo nazo mda wa mateso

(Mchungaji/Kiongozi, baada ya kusoma kila vesi uliza swali hili: "Ahadi gani Yesu atupatiyayo tunapo kuwa katika mateso kwa ajili yake?")

Soma kwa sauti: Yohana 16:33 (Yesu anatuahidia kutupatia amani.)

Soma kwa sauti: Matayo 11:28 (Mapumziko.)

Soma kwa sauti: Waembrania 13:5-6 (Yesu hata tuachilia kamwe. Atatusaidia.)

Soma kwa sauti: Marko 10:29-31 (Ndugu, Dada,...)

Soma kwa sauti: Warumi 16:20 (Kwa mda ufaao, Mungu atamuharibu adui wetu na kazi yake.)

Namna gani tunaweza kuwasaidia wengine walio katika mateso kwa sababu ya kumfuata Yesu ama kwa sababu ya kuhubiri injili

- Kuwaombea na kuwasaidia wakati wanapokuwa katika magumu.
- Kuwasaidia na chakula na mahitaji mengine na kuwatemebelea pia. Labda wanaweza kuhitaji nyumba mahali ambapo wanaweza kuishi.
- Kushugulikia afya yao.
- Kuwaalika wakristo wengine ulimwengu kuwaombea.

Namna gani Mkrito Anaye Teswa kwa njia Isiyo ya Haki Awatazame wale Wamtesao?

(Mchungaji/Kiongozi: Soma oroza hiyi; soma pia maandiko haya ikiwa kuna mda.)

- Uwasamehe watesi wako kama vile Yesu aliovyo fanya.. **Luka 23:34**
- Uwaombee wale wanao kutesa. **Matayo 5:44 na Luka 6:27-29**
- Uoneshe upendo bali isiwachukiye. **Matayo 5:44**
- Uwatangazie watesi wako habari njema kwa ushujaa. **Matendo4:1-13**
- Usirudishe mabaya kwa mabaya. **Warumi 12:17**
- Utende mema kwa wale wanao kutesa. **Luka 6:27-28**

- Umuachie Mungu kisasi. **Warumi 12:19-21**

Yale Mungu Anayoweza Kutenda Wakati wa Mda wa Mateso

1. Mungu anauwezo kukuokoa mikononi mwa maadui wako.

Soma kwa sauti: Matendo 12:6-18 (Mchungaji/Kiongozi: unaweza kusoma andiko hili ikiwa ni ndefu zaidi ama ngumu kusoma kwa watu wako.) 2 Wakorinto 1:8-10 (Paulo aliokolewa katika mikono ya watu wabaya na kuokolewa kwa kuepuka kifo mara kwa mara.)

2. Mungu anatupatia amani mda wa mateso.

Soma kwa sauti: Yohana 16:33

3. Mungu anatupatia uvumilivu.

Soma kwa sauti: Yakobo 1:3-4 na 2 watesalonike 1:4

4. Mungu anatufundisha kuwapenda wale wanao tuchukia.

Soma kwa sauti: Matendo 7:59-60 (Stefano aliwaombea wale walio mpinga mawe na kumuua.)

5. Mungu aweza kutenda miujiza wakati wa mateso makubwa.

(Eliya nabii, akiwindwa na mfalme muovu, aliletewa chakula na kunguru walio tumiwa na Mungu **1Wafalme 17:1-6.**)

6. Mungu atumia mda wetu wa magumu kwa kutangazia wengine Habari Njema ya Yesu. Hii ina maanisha kwamba mateso yako yanaweza kuwalettea wengine furaha ya wokovu na uzima wa milele katika Kristo.

Soma kwa sauti: Wafilipi 1:12-14 (Paulo alifungwa gerezani na kwa sababu ya hiyo watu wengi wakaanza kuliskia Neno la Mungu.)

Somo kwa ufupi:

Si jambo rahisi kumfuata Yesu. Kutakuweko mda wa msukumo mwangi na mateso. Mateso yaja si kwa sababu Yesu anataka tuteseke, bali ni kwa sababu ulimwengu hautaki tumfuate Yesu.

Mda wa mateso tunapashwa kusimama hima na kujua kwamba Mungu yuko pamoja nasi. Tunahitaji kumtegemea Yesu na ahadi ambazo Biblia itupeyazo. Tunaweza kuomba ili Mungu atutiye nguvu na kutuokowa katika ubaya huu, na pia kuwaombea watesi wetu.

Tuvumilipo masumbuko kwa ajili ya Yesu, tunapokea nguvu na kupitia yale tulio yaishi tunaweza pia kuwapa wengine moyo.

Vesi kwa ufahamu

Mchungaji/Kiongozi: Saidia kundi kujifunza na kuweka kwa ufahamu andiko hili:

Mathayo 10:32-33

“Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni.”

Maneno unahitaji Kuelewa: Kamusi

Agano Jipyä: Kitabu cha hadisi za Yesu na mpango wa Mungu kwa ajili ya wale wamuaminio Yesu.

Agano la Kale: Kitabu cha hadisi za Mungu kilicho andikwa kisemacho kuhusu habari za ushirika kati Mungu na wanadamu walioumba kabla ya kuzaliwa kwa Yesu.

Chakumi: Moja ya kumi ya mapato yako yote.

Farao: Jina la mfalme wa Misri.

Hesabiwa haki, Kuhesabiwa haki, kukubaliwa: Mungu atangaza kwamba “hatuna hatia” kwa ajili ya mabaya tulio ya yatenda.

Hukumu: Kuchunguzwa kwa kesi mahakamani na kuonekana kuwa na hatia. Baada ya uamzi wa mahakama kuonekana kuwa mtu amekosa.

Imani: Kuweka tumaini lako lote ndani ya Yesu.

Injili: Habari Njema, ama habari za Yesu. Biblia ina vitabu vine vya injili vilivyo andikwa na waandishi hawa: Matayo, Marko, Luka na Yohana.

Jehenamu: nafasi ya mateso kwa ajili ya wale waliokufa pasipo kumuamini Yesu.

Kalvari: Jina la mlima ambako Yesu alisulubishwa msalabani.

Kiungu: chochote kilicho na ushirika na Mungu ana miungu ya uongo.

Korinto: Mji mmoja ambao kwa wakati wa Yesu, mji huo ulionekana kuwa na miungu mingi.

Kristo: yule aliye tabiriwa ili aondowe zambi za wanadamu na kuturejesha kwa Mungu.

Kuacha: kujitenga kabisa na kitu, roho, ama mtu.

Kuchukuliwa: Kuondoka ulimwenguni na kwenda mbinguni; kuchukuliwa kutoka duniani hadi mawinguni/mbinguni.

Kuharibika: mbaya, ubinafsi, kujaa na mipango mibaya, mambo yasiyo pendeza ama yanayo oza

Kujenga, kujengwa: kujenga kitu, kumtia mtu nguvu ama kumufariji.

Kukana: Kutangaza hazarani kwamba hautakuwa tena na ushirika wowote na tabia fulani, watu, ama roho fulani.

Kukiri: neno la maana linalo semeka na mtu kwa sauti.

Kukombowa (Mkombozi): kununua mara tena kile kilicho paniwa ama kuibiwa; kumuokowa mtu kutoka katika hatari ama kumurudisha awe na ushirika pamoja na Mungu.

Kuokoka: Kusafishwa zambi zako na kurudi kuwa na ushirika na mara tena pamoja na Mungu, kwa sababu ya kifo cha Yesu msalabani kwa ajili yako. Umeokolewa kutoka zambini na kuepuka hukumu ya milele.

Kuomba kwa Roho: Kuomba kwa lugha ambayo umepewa na Roho Mtakatifu. Hii si luga yako ama luga ambayo tayari unazungumza, bali karama ya luga uliyo pewa na Mungu.

Kupotea: Hapa tunasema kuhusu wale ambao hawakumkubali Yesu kama vile Bwana na Mwokozi hao wamepotea, kwa sababu hao wataenda Jehenamu kwa kuwa wamemkataa Yesu Kristo ; na kwa kuwa zambi zao hazikusamehewa.

Kusulubiwa: kubambwa kwa misumari msalabani hadi kufikia kufa.

Kutafakari, kuchunguza mambo: Kujua, kuelewa; kuwa na uwezo wa kulinganisha na kuamua kuhusu kitu fulani.

Kutangaza, tangazo: Kusema kwa sauti mbele ya kundi; kusema kwa sauti kubwa na kwa ushujaa hazaranı.

Kuteswa, Mateso: kuazibiwa, kuuwawa ama kufukuzwa kwa sababu ya kuto kumuamini Yesu.

Kuto kusamehe: kukataa kumsamehe mtu mwengine, ukiweka moyoni hasira, kinyongo na hisia mbaya kwa ajili yake.

Kutubu: kuacha zambi na kumuelekea Mungu.

Kutukuza: kueleza mambo makubwa, kubariki, kuinua.

Kuvunja sheria: Kuasi sheria, kuvuka hadi nafasi ya ubaya.

Kuzaliwa mara ya pili: kuzaliwa na Roho Mtakatifu na kukubaliwa katika jamaa ya Mungu. Kuwa mzima katika ushirika na Yesu Kristo. **Soma Yohona 3:3.** (Yesu alisema kwamba tunapashwa kuzaliwa mara ya pili)

Maandiko: Biblia, ama Maandiko Matakatifu ya Mungu. Mara tunatumia andiko hili pahali pa kusema "Vesi za Biblia".

Mafundisho: maagizo, ama yale tunayo yaamini.

Malaika: kiumbe cha kiroho kimtumikiacho Mungu mchana na usiku; kuna pia malaika walio tupiwa ama malaika wabaya walio muasi Mungu, wanaitwa pia pepo wachafu, mashetani, ama mizimu.

Maneno ya Unabii, Unabii: Maneno ambayo Mungu ampatia mtu ili atangazie kundi ama amuelezee mtu fulani. Hii ni kazi ya Mungu, na haitoki katika mawazo yetu ama utashi wetu.

Mapepo: pepo wachafu wafanyao kazi kwa kumpinga Mungu na kazi zake, pepo hao wawatesa watu na kusumbua ulimwengu.

Mataifa: Wale wasio kuwa wayahudi; wasio kuwa katika ukoo wa Yesu. Wayahudi wengi walifikiri kuwa mataifa hawakuwa bora kuliko umbwa.

Yesu hakuwa na maoni hayo, bali anapenda wote na alikufa kwa ajili ya kila mtu, pasipo kujali kabilia, ukoo, ama rangi.

Mateso: Maneno/matendo ya hasira ama jeuri zidi ya wale wanao amini Kristo, hiyo yanenwa ama yatendekayo na wale wasio amini.

Mchungaji Mwema: Jina ambalo Yesu anajiita yeymwenyewe. Awashugulikia wale walio wake.

Mfano: Hadisi inayo husu maisha iliyo na maana ya kiroho.

Mfuasi: Mtu ambaye anataka kumfuata kiongozi wake na kujifunza kwa kuwa karibu sana naye. Wakristo ni wafuasi wa Yesu.

Miujiza: Yatoka kwa Mungu pekee. Uwezo upitao akili ya binadamu, ujuzi, na elimu yake. Maneno ama matendo ayafanyayo Mungu, si kuitia mashirika ya kibinadamu. Hakuna mtu anayeweza kujidai kwamba ni yeche aliye tenda ishara hizo. Kila mtu atajua kwamba ni Mungu aliye tenda ama kusema.

Miungu: Sanamu iwakilishayo roho ya mungu; miungu inaweza kuwa kitu chochote ambacho unakipenda sana, unacho abudu, ama unacho kitumainia sana. Kuabudu miungu ni chukizo na yamuletea Mungu hasira.

Msamaria: Mtu aliye Myahudi-nusu. Wasamaria walichukiwa na wayahudi. Ikiwa myahudi angemgusa msamaria myahudi huyu angetazamiwa kuwa si safi ama mchafu, na ilimubidi ajioshe ili atazamiye kuwa safi tena.

Mtume: Kiongozi wa kanisa, zaidi huyo aliye kuwa karibu na wanafunzi wa Yesu.

Mwinjilisti: mtu aliye itwa na Mungu ili aihubiri habari njema ya Yesu, kifo chake, na ufufuko (kufufuka kutoka wafu).

Mwongozo, kuongozwa: mwaliko kuitia mafundisho ili watu watende mema; ama kumfundisha mtu kutembea katika njia ya haki ili afikiye mipango ya Mungu.

Neema: Usaidizi ambao hatustahili tulio upewa na Mungu na msamaha kwa zambi zetu. Msahaha huu umetufikia kwa sababu ya yale Yesu aliyo yatenda msalabani.

Petro: Mmoja kati ya watu wa kwanza walio mwamini Yesu. Rafiki na mfuasi wa Yesu. Petro aligeuka baadaye mchungaji katika kanisa katika mji wa Yerusalemu.

Sadaka: Zawadi itolewayo kwa Mungu ili kumshukuru ama itolewayo kwa ajili ya kusaidia hitaji fulani kanisani.

Sadaka ya kuteketeza: Sadaka ya mnyama atolewaye kwa jumla kwa Mungu kwa njia ya kuteketezwa; watu wa Mungu walitowa kwa njia hiyo katika Agano la Kale, kabla Yesu aje.

Ubatizo: kuwekwa ndani ya maji kwa jumla na baadaye kuondolewa tena humo, ili mtu aoneshe kwamba amekufa kwa zambi na kuishi kwa ajili ya Kristo.

Udanganyifu, uongo: Kuto kuwa mwaminifu, muongo, kufunika ukweli, ama kubadilisha sehemu ya ukweli.

Ufunuo: kufunuliwa kwa kitu kilicho fichwa, ama kuoneshewa. Mfano kitu kilicho funikwa na shuka; baadaye shuka hiyo yafunuliwa na kitu cha onekana wazi.

Uhakika: kuto kuwa na mashaka kuhusu kitu ama jambo fulani.

Upako: Uwepo wa Roho Mtakatifu ndani ya mtu ni nguvu ya kusema ama kutenda jambo kwa nguvu kwa jina la Yesu. Tunasoma katika Agano la Kale kwamba watu walipakwa mafuta kwa kuonesha uwepo wa Mungu ndani yao. Tangu Yesu alipo kuja, kila aaminiye anaweza kupokea upako wa Roho Mtakatifu wa Mungu, kwa kutenda yale ambayo Mungu asema.

Ushuhuda, shuhuda, kuushuhudia: Kuwaelezea wengine kuhusu yale Mungu aliyo tutendea.

Utakatifu: maisha pasipo kutenda zambi yanayo kuwa na shabaa ya kumpendeza Mungu.

Utatu wa Mungu: Asili ya Kiungu; Mungu wa wakristo; Utatu Utakatifu; Mungu Mmoja katika utatu.

Waisraeli, Wayahudi: Kizazi cha mtu aliye itwa Israeli (aliye itwa Yakobo). Watu hawa waligeuka wachaguliwa wa Mungu. Katika kizazi hiki ndimo mlimo Yesu aliwaliwa.

Yerusalem: Mji mkuu wa Israeli, Inchi alimo ishi Yesu.

Kutembea Pamoja na Yesu

Yesu akasema, "Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi"; bali wengi wasemao kwamba wanamuata Yesu hawaelewi kabisa maana ya kweli ya neno kuwafanya watu wawe wanafunzi.

"*Kutembea Pamoja na Yesu*" ni mfululizo wa mafundisho, kila somo linakusudia kulenga nukta muhimu fulani kwa ajili ya wale wanao amini Kristo. Jinsi ambavyo mafundisho haya yatakuwa yakifundishwa na kuwekwa katika vitendo ama kuyaishi, ukweli na utajiri wa kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa Yesu utaonekana wazi katika maisha ya wale wanao shiriki mafundisho haya.

Mafundisho haya, yameandikwa ili yapate kusomewa kwa sauti kwa ajili ya kundi na mchungaji ama kiongozi, mafundisho haya yawapa moyo watu kuyashiriki kwa kuwapatiya changa moto kuitia maswali na nukta mbalimbali za kuzungumzia na kufikiri pamoja katika kundi, wakati wa kujifunza kila mmoja atowa mawazo aliyo nayo katika kundi. Mafundisho haya yanaweza kutumiwa pia vyepesi katika mafundisho ya makundi madogo madogo, na hata kwa ajili ya majifunzo ya kipekee.

Mafundisho haya yameandikwa na kuandalisha ili yajibu mahitaji maalumu ya waamini wanaoishi katika inchi za Africa ya kati na Afrika ya mashariki.

Waandishi wameandika kitabu wakielewa kwamba labda wamoja wanao shiriki mafundisho haya, katika kundi watakuwa hawana Biblia, na wengine labda watakuwa hawana elimu ya juu.

YMG International

E-mail: ymgrdc@aol.com

Kimeandikwa & Kutafsiriwa na
Mana Shemahambà Rostand & Julie Young

